Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Tisa – Terehe 1 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA BUNGENI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTUMISHI):**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa kazi katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 178

### Hospatali ya Wilaya ya Same

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa hospitali ya Wilaya ya Same ilijengwa mwaka 1946 na sasa iko katika hali ya uchakavu sana kuanzia na wodi za wagonjwa, vifaa vingi ni chakavu, hakuna jiko, hakuna chumba cha kuhifadhi maiti, na kwa kuwa hospitali hiyo inahudumia eneo kubwa la Wilaya hiyo lenye kilometa za mraba zaidi ya 5,000 kwenye eneo tambarare na milimani, na kwa kuwa pia inahudumia majeruhi wa ajali zinazotokea katika barabara ya Dar es Salaam – Arusha:-

(a) Je, Serikali itatenga katika bajeti yake fedha kwa ajili ya kuondoa kasoro nilizoeleza?

(b) Je, Serikali iko tayari kupitisha Hospitali ya Kilutheri Gonja – Bombo iwe hospitali teule *(DDH)* ili iweze kuhudumia wananchi wa milimani ambako usafiri wa barabara ni duni na hakuna mawasiliano ya simu?

(c) Je, Kwa kuzingatia sababu za kijiografia, miundombinu, idadi ya watu na ukubwa wa Wilaya. Je, kwa nini Serikali inachukua muda mrefu kuipatia Wilaya ya Same hospitali teule ya Gonja – Bombo wakati uongozi wa KKKT wameridhia kimaandishi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA ( K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hospitali ya Wilaya ya Same ni chakavu na itaendelea kutengewa fedha kwenye Bajeti ya Serikali kwa ajili ya ukarabati wa kawaida kama inavyofanyika kwa hospitali nyingine za Wilaya. Kwa sasa baadhi ya majengo ya hospitali hiyo yanakarabatiwa kwa msaada wa wafadhili kutoka Uholanzi kupitia Kanisa Katoliki Jimbo la Same. Kwa upande wa chumba cha maiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na madawa kupitia *Medical Stores Department* na baadhi ya vifaa hununuliwa kwa fedha za ruzuku itolewayo kwa ajili ya Idara ya Afya. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 jumla ya Sh.4,000,000/= zimetengwa kwa madhumuni haya.

(b) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Gonja ambayo ipo chini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, ilianzishwa mwaka 1929. Hospitali hii ipo umbali wa kilometa 50 kutoka Same mjini na hutoa huduma kwa zaidi ya wakazi 150,000 wa Wilaya ya Same. Hadi sasa hospitali hii bado ina matatizo ya kiundeshaji kutokana na ukosefu wa fedha. Wamiliki wa hospitali hii wamekubali iwe teule kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi tofauti na ilivyo sasa. Hata hivyo ili hospitali hii iwe teule Serikali itabidi ichangie Sh.110,270,000/= zitakazotumika kugharamia mishahara ya watumishi, madawa na gharama za uendeshaji na wamiliki wa KKKT wachangie Sh.181,000,000 zitakazotumika kugharamia ukarabati wa majengo, ununuzi wa gari la wagonjwa, madawa na kulipia madeni yatokanayo na mishahara, umeme na pensheni. Hivi sasa Serikali huchangia Sh.24, 450,000/= kwa ajili ya hospitali hii.

(c) Mheshimiwa Spika, lengo kubwa la Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata huduma bora na kwa wakati. Tatizo kubwa linaloikabili Serikali ni ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti yake ili kuendelea kuzihudumia hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuimarisha huduma zitolewazo. Pamoja na uongozi wa KKKT kuridhia hospitali ya Gonja – Bombo iwe hospitali teule, kabla ya uamuzi huu kuafikiwa na Serikali ni muhimu kwanza kutatua matatizo ya kiuendeshaji yaliyopo hivi sasa katika hospitali hii.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Ningependa kufahamu Wizara ambayo ina jukumu la kuweza kutupatia hospitali ya Bombo - Gonja kuwa teule, kwa sababu tukienda Wizara ya Afya wanasema twenda TAMISEMI. Sasa hii kutupiana mpira TAMISEMI na Wizara ya Afya itakwisha lini?

(b) Katika mwaka huu wa fedha hospitali ya Wilaya ya Same imepangiwa kiasi gani cha kuikarabati? Kwa sababu majengo yake yana hali mbali kiasi kwamba inaweza kuharisha usalama wagonjwa waliolazwa pale kuta kuangukia wagonjwa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA ( K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba kuna kutupiana mpira kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI kwa kuwa majukumu yako bayana na ninapenda tu katika hili nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu la kuifanya Hospitali iwe teule mwanzo lilikuwa chini ya Wizara ya Afya. Baada ya kuona matatizo yanayojitokeza imeamuliwa rasmi kwamba sasa suala hili lifanywe na Halmashauri za Wilaya. Kwa maana nyingine ni kwamba sasa ili Hospitali iwe teule basi mkataba uwekwe baina ya hospitali hiyo inayotaka kuwa teule na Halmashauri husika. Wizara ya Afya baada ya mkataba baaada ya mkataba huo kuwekwa ndio itatoa huduma kwa maana ya dawa na kulipia mishahara.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la juu ya ukarabati wa Hospitali hii kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, fedha zilizotengwa mwaka huu ni shilingi milioni 4. Lakini bado kuna uwezekano wa kupata fedha za ziada kutokana na malipo ya fedha zinazoingia katika hospitali hii kwa njia nyingine, kwa maana ya *cost sharing* na vitu kama hivyo. Lakini vile vile kama kuna ombi maalum kwa Wizara basi hata kibali kinaweza kikatolewa kwa kutumia *basket fund* ili kufanya ukarabati. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza, kwa sababu hospitali ya Bombo haina tofauti na Hospitali ya Bumbuli chini ya Dhehebu hilo hilo la Kilutheri na kwa kuwa sera iliyopo ni ile ya *DDH* kwa maana *District Designated Hospital*. Lakini sasa kwa hali inavyokwenda je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kupitia sera hiyo na kuondoa ile *D* moja baada ya kusema *District* iwe *Designated Hospital*. Kwa maana *Hospital* hizi ya Bumbuli inahudumia watu karibu 150,000 na kuna Hospitali za Wilaya zinahudumia watu 50,000. Je, Waziri anasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA ( K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, awali kulikuwa kuna hospitali zinazoitwa *DDH* kwa maana ya *District Designated Hospital* na hospitali hizi zilikuwa ni katika maeneo ambayo hayana hospitali za Wilaya za Serikali. Kwa hivyo, hivi karibuni umeanzishwa Mkao wa Manyara ambao wenyewe hauna hospitali ya mkoa na tulikuwa tayari kama Wizara kuweza kuwapatia *Designated Hospital* kama anayosema Mheshimiwa Williuma Shellukindo katika ngazi ya Mkoa. Kwa hivyo hii *District Designated Hospital* siyo kitu kwamba ni lazima iwe katika *District level,* inaweza ikawa katika *level* nyingine kutegemeana na mahitaji.

Na. 179

**Barabara za Awali Kutoka Butundwe na Busanda Kwenda Geita.**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Tarafa ya Butundwe na Busanda wanategemea kupata mahitaji yao ya lazima na huduma za kijamii katika mji wa Geita na kwa kuwa barabara za awali za mkato kwenda Geita zimepindishwa ili kukwepa migodi ya dhahabu jambo limesababisha ongezeko la umbali wa Km.22, ongezeko ambalo limekuwa na mateso makubwa kwa wananchi husika kutembea umbali huo wote:-

(a) Je, Serikali haioni huruma kwa wazalendo hao wanavyoteseka kwa mwendo mrefu kwa sababu ya kuwepo kwa dhahabu Wilayani kwao?

(b) Kwa kuwa sehemu ambayo barabara inaweza kupita bila kuingilia shughuli za migodi na vile vile kupunguza umbali wa km.22; Je, kwa nini Serikali isiwashinikize wenye migodi wakatengeneza barabara kupitia Kijiji cha Nyamalengo, Magema hadi Samina *(Nyanza Road Camp)* na barabara toka Geita – Bugurula?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba jibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sio dhamira ya Serikali kuwatesa wananchi wake, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma nzuri katika kila sekta ikiwepo sekta ya barabara, hivyo lengo kubwa la Serikali katika suala zima la usafiri ni kuboresha huduma hiyo ikiwemo barabara ili wananchi wa maeneo hayo na sehemu nyingine wanufaike na huduma ya barabara hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati shughuli za mgodi wa Geita zinaanzishwa, uongozi wa Mgodi uliomba kurekebisha sehemu ya barabara za Mkoa na Wilaya zilizokuwa zinapita ndani ya eneo la mgodi ili zipitie nje ya eneo hilo. Kwa kutambua umuhimu wa mgodi huu kwa Taifa, Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ulikubali ombi hili na kuruhusu barabara ya Geita – Katoro, Geita – Nzega na Geita – *Port* Nungwe zifanyiwe marekebisho yaliyoombwa na uongozi wa mgodi kwa gharama ya mgodi wenyewe. Kazi hii ilikamilika mwaka 2002. Baada ya kuona kuwa kuna sehemu ambayo barabara inaweza kupita bila kuingilia shughuli za migodi na vile vile kupunguza umbali wa km. 22 unaosababishwa na kupindishwa kwa barabara za awali na za mkato ili kukwepa migodi ya dhahabu, Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji wa Geita *Gold Mines* mwaka 2004 waliweza kufanya matengenezo ya barabara ya Nyamalembo kupitia Magema (Nyanza *Road*) Samina umbali wa kilometa 6. Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ni miongoni mwa viongozi wa Wilaya waliotembelea barabara hii wakati inafanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa barabara hii inaweza kupunguza umbali uliopo kati ya Butundwe na Busanda kwenda Geita, barabara hii ina mto mkubwa wenye upana wa mita 40 na kina cha mita 1.6 na haukauki kwa kipindi chote cha mwaka. Kazi iliyokuwa ikifanyika ya ujenzi wa daraja *(vented drift)* ya gharama ya Tshs. Milioni 25 ilisimama baada ya mto kujaa. Kazi hii itaanza tena wakati wa kiangazi baada ya maji kupungua.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ni kitu gani hasa kinachofanya wazalengo hao wateseke kwa kuwa miaka mingi wameisha na dhahabu hizi. Sasa ni kigezo gani cha kufanya

wafungiwe njia kwa ajili ya migodi ambayo waliishi nayo siku nyingi, sasa wanafungiwa wakiwa maeneo yao wanapita porini na eneo kubwa la Geita lina mapori. Serikali wanieleze ni kitu kipi kipya hasa kinachosababisha wafungiwe wazalendo hao?

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni kuwa, kwa sababu eneo analolitaja Mheshimiwa Waziri halipiti maeneo ambapo kwenye swali la msingi la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ulieleza kwamba wapunguziwe adha ya kuzunguka kwenye mapori. Sasa Serikali haioni sasa umuhimu, kwa sababu wana ulinzi salama hao wenye migodi kwa nini wasiwaachie wazalendo wakapita maeneo hayo, wakapita kwa urahisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio nia ya Serikali hata kidogo kuwapa matatizo ya njia au barabara watu wa eneo hili. Ndio maana hata kabla ya uamuzi huo kufanywa Serikali kwa maana ya Wizara ya Ujenzi ilishirikiana kwa ukamilifu kabisa na uongozi wa wilaya juu ya hatua za kupindisha barabara ile na hata ilipoonekana barabara ya kilomita 22 ni ndefu, bado uongozi huo ulikaa na kuhakikisha kwamba barabara hii sasa inatengenezwa eneo lingine ambayo itakuwa na urefu wa kilomita 6. Tayari tumeshatumia milioni 15.6 kwa ajili ya barabara hii ya mgodi, lakini na milioni 25 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kujenga daraja, ujenzi huu wa daraja umesimama tu kwa sababu kina cha maji ni kikubwa hivi sasa ni mita 1.6. Bila shaka kiangazi kitakapofika barabara hii itajengwa na umbali wa kilomita 22 utakuwa umepungua mpaka kufikia kilomita 6. Juu ya swali lake la pili, kwamba hii dhahabu ilikuwepo muda wote wananchi hawa kwa nini wasipite wakati mgodi una ulinzi. Tatizo hapa sio tu kwamba mgodi unafikiri labda wataibiwa dhahabu zao, lakini hata usalama wa wananchi wenyewe kwa sababu kwenye migodi kuna milipuko, kwenye migodi kuna kila aina ya hatari. Kwa hivyo hii si maana tu ya kulinda dhahabu zao, lakini ni kulinda vilevile usalama na maisha wa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tunajua jinsi Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba anavyolisimamia suala hili. Ndio maana hata juzi tarehe 13 mwezi Mei kupitia Wizara ya Ujenzi aliuliza juu ya swali hili hili na tukampa majibu yanayofanana na haya. Kwa hivyo ningependa kuwaomba wananchi waliomchagua Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, wafahamu kwamba kazi anayoifanya juu ya kuondosha matatizo yao ni kubwa ndani ya sayari. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Na kazi anayoifanya Mheshimiwa James Musalika nayo tuisikie. *(Kicheko)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye jibu la msingi la Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali na wawekezaji wameshirikiana kujenga barabara ya Nyamalembo, Magema hadi Samina taarifa ambazo mimi nafahamu kwamba ni wawekezaji peke yao wamejenga hicho kipande, barabara

ambayo inaitwa *Kabuzi Road*. Je, Serikali nayo iko tayari kujenga kile kipande cha Geita hadi Bugurula kwa sababu wanachukua pesa ya dhahabu lakini hawapendi kurudisha huko Maziwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kama alikuwa anafuatilia vizuri nilipokuwa najibu jibu la swali la msingi. Nilichosema ni kwamba Serikali ilishirikiana na mgodi kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa. Lakini waliotoa gharama za ujenzi huu kama makubaliano ya awali yalivyokuwa, ni Mgodi wenyewe wa Geita. Kwa hivyo suala la kujenga kipande kingine ambacho Mheshimiwa James Musalika amekitaja hivi sasa, ambacho kipo nje ya barabara inayozungumzwa na muuliza swali la msingi. Ningeomba alipeleke kwa utaratibu unaotakiwa kupita Halmashauri yake ili liweze kushughulikiwa kama barabara nyingine.

Na. 180

**Bwawa la Manchira**

**MHE. DR. JAMES WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Mkapa alipotembela Wilaya ya Serengeti hapo tarehe 4/10/2000 aliahidi kuwa Bwawa la Manchira litachimbwa na kukamilika kabla ya kumalizika kwa kipindi chake cha uongozi, lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika na baada yake panafanyika njia ya kupitishia maji *(spillway)* na bado hata tuta la kukinga maji hakuna:-

(a) Je, kazi ya kuchimba Bwawa hilo itakamilika lini na itagharimu fedha kiasi gani?

(b) Je, hadi sasa ni kiasi gani kimeshatumika kwa ajili ya uchimbaji wa Bwawa hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Bwawa la Manchira ama Bwawa la Mugumu ulianza katika kipindi cha mwaka 2003/2004 baada ya kazi hiyo kusimama kutokana na tatizo la upatikanaji wa fedha. Kazi ambazo zimekwishafanyika kwenye eneo la Bwawa la Manchira ni pamoja na uchimbaji wa udongo na ulipuaji wa mawe kwenye utoro wa maji, ambayo imekamilika kwa asilimia 95. Aidha, uchimbaji na uondoaji wa mawe katika sehemu litakapojengwa tuta la bwawa *(core trench)* umekwishakamilika na ujenzi wa tuta dogo la kuelekeza maji kujaa kwenye bwawa *(guide bund)* nao umekamilika kwa asilimia 75. Ujenzi wa Bwawa la Manchira ulikadiriwa kuchukua muda wa miezi 18 kuanzia mwezi Februari 2004 na hivyo bwawa lilitarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2005. Hata hivyo

kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha kwenye Bajeti ikilinganishwa na mahitaji, mradi hautaweza kukamilika mwezi Julai 2005 kama tulivyotegemea. Ni matarajio yetu kuwa ujenzi wa Bwawa utakamilika katika kipindi cha mwaka 2005/2006 kama fedha tulizoomba Serikalini kwa kazi hii zitatolewa. Hadi mradi wa ujenzi wa Bwawa la Manchira utakapokamilika, inakadiriwa kwamba kiasi cha Shilingi bilioni 1.5 zitatumika.

(b) Hadi sasa, kiasi cha Shilingi milioni 580 kimekwishatumika kwa ajili ya uchimbaji, ulipuaji na uondoaji wa mawe kwenye utoro wa maji na kwenye eneo la kujenga tuta la Bwawa la Manchira.

**MHE. DR. JAMES WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inafahamika wazi kwamba Mheshimiwa Rais alipokuja aliahidi na kwamba kazi ikamilike kabla hajamaliza kipindi chake. Lakini Serikali ikaendelea kuwa inatoa milioni 2 tu kufanya hiyo kazi kwa mwaka.

(a) Je, huoni kwamba kwa makusudi kabisa hii kazi iweze kumalizika itachukua miaka saba, sasa Serikali ina mpango gani wa kukamilisha juu ya ahadi ya Rais kwa muda unaotakiwa?

(b) Kwa sababu tatizo la maji sasa hivi ni tatizo kubwa sana katika mji wa Mgumu, basi kama hela ni chache kwa nini Serikali isituchimbie visima virefu kama hatua ya dharura halafu kazi ya kukamilika hilo bwawa iendelee wakati hela zinatafutwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kwa kiasi kikubwa kabisa kuitekeleza ahadi hii iliyotolewa na kiongozi wa Kitaifa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini Mheshimiwa Dr. James Wanyancha bila shaka anatambua kwamba ili ahadi ya Rais au hata Waziri iweze kutekelezeka, lazima na upatikanaji wa fedha uwe unapatikana kwa urahisi na hali yetu inafahamika ilivyo. Lakini kwa kawaida tunapojenga bwawa tunaanza na tuta ili kutengeneza sehemu ya kuhifadhia maji na ujenzi wa ule utoro wa maji yaani *spillway,* ili kuhakikisha utoaji salama wa maji bila kuathiri tuta lenyewe wakati maji yanapojaa unapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mazingira ya bwawa hili la Manchira kipaumbele kilikuwa lazima kwanza tuanze kuchimba na utoro wa maji kabla ya kujenga lile tuta kwa sababu kulihusika vile vile na ulipuaji, kama tungeanza na tuta bila shaka tuta lingepata mtikisiko mkubwa. Hata hivyo mwaka 2002/2003 Serikali ilitenga milioni 200 tulizozipata, mwaka 2003/2004 tulitenga tena milioni 200, mwaka 2004/2005 tulipata milioni 180, mwaka huu 2005/2006 Waziri wa Maji ataomba tena milioni 400. Sasa hii inaonyesha kabisa kwamba Wizara ya Maji inajitahidi kutekeleza ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, basi kama hilo haliwezekani kuchimbwa visima virefu. Sasa tutakuwa tunaongeza mzigo kabla ule wa mwanzo hatujafanikiwa nao. Mimi ningeomba kwamba tuwe kama wale wazazi ambao mtoto mmoja akipata kiatu badala ya kumnunulia soksi kwanza, anahakikisha na wa pili anapata kiatu ndio ananza kutafuta soksi kwa wote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ningeomba tumalizie hii habari ya bwawa halafu ndio tufikirie visima.

Na. 181

**Mahitaji ya Maji Himo Njia Panda**

**MHE. MEJA JESSE MAKUNDI:** Kwa kuwa, kilio kikubwa cha Uhitaji wa Maji kwa wananchi wa Himo – Njiapanda pamoja na taasisi, shule ambao wanaona kwa macho yao chemchem na mifereji ya maji yakibubujika huko Kilema Kaskazini kwa miaka mingi tangu tupate uhuru, lakini hadi leo wananchi wa maeneo hayo hawafikishiwi maji ya bomba licha ya kuwepo na chemchem hizo zenye maji mengi:-

(a) Je, adha na shida hiyo inaweza kuondolewa kwenye awamu hii ya tatu ya uongozi au wananchi wabaki wakimwomba Mungu uongozi unaofuata uje utatue tatizo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeshapelekwa kwenye Idara ya Maji Wilaya ya Moshi kwa lengo la kutengeneza vyanzo (*intakes*) vya maji kutoka Kilema Kaskazini kwa nia ya kufikisha maji safi na salama ya bomba kwa wananchi wa Himo – Njiapanda?

(c) Je, wananchi wa maeneo hayo walishirikishwa vipi katika kuchimba mitaro, kulaza mabomba ili kurahisisha upatikanaji wa maji kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Katika kutatua tatizo la upungufu wa maji Himo – Njiapanda, Serikali iliamua kuchukua hatua ya haraka na ya muda mfupi kwa kuchimba visima vinne vya maji katika eneo la Kilototoni na visima hivi vinatumika kwa sasa. Sambamba na jitihada hizo, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani imeanza kutekeleza mpango wa muda mrefu kwa kupanua na kukarabati miradi yote ya maji katika eneo lote la Mashariki mwa Wilaya ya Moshi Vijijini likiwemo eneo la Himo – Njiapanda. Upembuzi yakinifu wa mradi huu umekwishakamilika. Kwa sasa, Serikali inafanya majadiliano na Serikali ya Ujerumani juu ya namna ya kutekeleza ujenzi wa mradi huu.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali haijapeleka fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini kwa ajili ya mradi wa maji kutoka Kilema Kaskazini hadi Himo – Njiapanda kwa sababu hatuna mradi wa aina hiyo. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa aina hiyo umefanyika hivi karibuni tu kama nilivyojibu kwenye kepengele (a). Hata hivyo Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imekuwa ikitenga fedha kwa ajili

ya kutatua tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika eneo la Himo – Njiapanda kama ifuatavyo: Mwaka 2002/2003 shilingi milioni 10, kwa ajili ya kuchimba kisima kirefu. Mwaka 2004/2005 shilingi milioni 10 kwa ajili ya kujenga kibanda cha pampu na kuweka umeme. Karibu kazi zote hizi zimekamilika isipokuwa ujenzi wa kibanda ambao unaendelea na utakamilika hivi karibuni.

(c)Mheshimiwa Spika, wananchi wa eneo hilo bado hawajashirikishwa katika kazi za kushimba mtaro wala kulaza mabomba kwa sababu mradi huo haujaanza kujengwa. Wananchi walishirikishwa katika shughuli za upembuzi yakinifu zilizofanyika kuanzia mwezi Machi 2004 hadi Februari 2005. Napenda kuwashukuru wananchi wa eneo la Himo – Njiapanda, kupitia kwa Mheshimiwa Mbunge, kwa ushirikiano wao mzuri wakati wa upembuzi yakinifu.

**MHE. MEJA JESSE MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini kwa kuwa fedha zote hizi za kuchimba visima zimeweza kutumika kwa kutengeneza *intake* kule juu Kilema Kaskazini kwenye chemchem ya maji mengi mno na *intake* yenyewe haigharimu zaidi ya milioni 3. Je, haoni ni vema sasa bila kutoa tena mafungu mengine kutengeneza hiyo *intake* ya chini ya milioni 3 kulaza hayo mabomba na maji safi na salama yapatikane kuliko kuja kupata maji taka ya visima ambavyo jinsi mji unavyojengwa inakuwa ni maji taka?

Kwa kuwa kuna Diwani makini sana Marangu Mashariki, Ndugu Robert Mushi, tumeenda nae *Pangani Basin Authority* wakatupa kibali cha kutoa maji kwenye chemchem ya Kisumbe *intake* inayopeleka maji *Ashira Girls Secondary School* na hivi sasa iko tayari *intake* hiyo. Je, Waziri anaweza kutoa kibali yale mabomba yaliyoko kwa *Drift Engineer* yaweze kutumika na viungio vyake kufikisha maji Himo - Njiapanda kwa kuwa maji hayo ni maji mengi sana?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO):** Mheshimiwa Spika, tuliona si vizuri kutumia fedha hizi za visima kwenda kufanyia kazi nyingine ya kuvuta maji kutoka kule juu, kwa sababu ukichukua gharama ya mabomba peke yake ni zaidi ya shilingi milioni 3 anayoisema.

Lakini tunajua mtu mwenye kiu hahitaji kuonyeshwa pesa anachohitaji ni kuonyeshwa maji. Lakini ningeomba wavute subira kwa sababu mradi huu wa visima ulikuwa ni hatua za muda mfupi tu. Hatua za muda mrefu ni huu ambao umeshirikisha Serikali ya Ujerumani ambayo mimi naamini maji yale yakifika pale haya matatizo mengine yanayomwumiza kichwa sasa hivi Mheshimiwa Meja Makundi na Diwani muadilifu Robert Mushi itakuwa ni historia tu ndani ya vichwa vyao.

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya (b), hatua ambazo zimechukuliwa na Mheshimiwa Mbunge na Diwani Robert Mushi, mimi ningewashauri mabomba yale

yabakie kufanya kazi iliyokusudiwa badala ya kupeleka Kisumbe ili maji yaweze kufikishwa *Ashira Secondary School* na Mandaka na kadhalika kwa sababu mabomba yale tayari yamefanyiwa mahesabu juu ya mradi huu mkubwa ambao kama Serikali ya Ujerumani na Tanzania mazungumzo yetu yatakwenda vile vile, tunategemea mradi huu kuanza mwishoni mwa mwaka ujao 2006/2007. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Himo njia panda wavute subira na bila shaka wanamsikia jitihada zake anazozifanya katika kuwatafutia maji wananchi hao. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 182

**Chama Kikuu Cha Ushirika Dodoma.**

**MHE. JOB Y. NDUGAI (K.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Dodoma umeunda Vyama Vingi vya Ushirika, lakini Mkoa hauna Chama Kikuu cha Ushirika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunda Chama Kikuu cha Ushirika katika Mkoa wa Dodoma?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuwapo kwa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Dodoma kutasaidia sana wananchi wa Dodoma kupata soko la uhakika kwa mazao yao kama vile Karanga, Alizeti, Ufuta , Mahindi, Mtama na kadhalika?

(c) Je, Serikali inaweza kueleza ni Vyama vingapi vya Ushirika vimeundwa Mkoani Dodoma hadi sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mudhihir ana majibu yote. Kwa hiyo endelea kujibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YAVIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma umeunda Vyama vingi vya Ushirika vya Msingi vya aina mbalimbali, vingi vya Vyama hivyo ni vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)*. Lakini pamoja na kuwepo kwa Vyama hivyo bado hakijaundwa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa Dodoma kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003, kifungu cha 14, kinatambua Muundo rasmi wa ngazi mbili za Ushirika nchini ambazo ni ngazi ya Vyama vya Msingi na ile ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika Kitaifa. Kwa mujibu wa Sheria hiyo ngazi nyingine za katikati ikiwemo ya Chama Kikuu inaweza kuundwa kwa kutegemea matakwa ya wanachama iwapo wataona kuna haja ya kuunda chama kikuu na kama ipo kazi ya kufanywa na chama hicho kikuu kitakachoundwa bila ya kuongeza gharama zinazoweza kuwapunguzia wananchi mapato yao.

Ni kutokana na matakwa hayo ya kisheria, Mkoa wa Dodoma bado haujaunda Chama Kikuu cha Ushirika kwa sababu wanachama wa Vyama vya Ushirika vilivyopo hawajaamua kufanya hivyo. Hata hivyo baadhi ya Vyama vya Akiba na Mikopo yaani *SACCOS* vilivyopo Mkoani Dodoma vimejiunga na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo – Tanzania yaani *SCCULT* chenye Makao yake Makuu Mjini Dar es Salaam na Ofisi yake ya Kanda ya Kati iko Dodoma kwa ajili ya kuwahudumia wanachama wake.

Baada ya maelezo haya, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kuweka mazingira yanayohamasisha wanaushirika kuanzisha Vyama ambavyo wanavihitaji na kuhakikisha kuwa Vyama hivyo ni imara, vyenye uhai wa kiuchumi na vinavyoweza kuwaongezea tija. Hatua za kuboresha mazingira hayo zimekwishachukuliwa, hivyo jukumu la kuanzisha Vyama katika ngazi yoyote kulingana na mahitaji sasa ni jukumu la wananchi wenyewe. Kwa hiyo, Serikali itakuwa tayari kuwapa ushauri unaohitajika wanaushirika wa Mkoa wa Dodoma pale watakapoamua wao wenyewe kuunda Chama Kikuu cha Ushirika watakachokihitaji kwa madhumuni watakayokuwa wamekusudia.

(b) Serikali inatambua kwamba kuwepo kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi vilivyo na nguvu za kiuchumi kutasaidia sana wananchi kupata soko la uhakika la mazao yao. Ndiyo sababu Serikali inaendelea kuhimiza uanzishaji wa shughuli za kibiashara katika ngazi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuhamasisha Vyama vya ngazi ya juu kuwa na majukumu ya kuratibu na kushauri kuhusu hali ya soko pale itakapokuwa inahitajika.

Hivyo ni jukumu la Vyama vya Ushirika vya Msingi kuamua ni muundo gani wa ushirikiano wanaoutaka na kuainisha majukumu yake katika kujiimarisha zaidi kwenye biashara zao.

(c) Hadi mwaka huu wa 2005, Mkoa wa Dodoma unavyo jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi 127 vya aina mbalimbali vikiwemo Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* 99, Ufugaji kimoja, Uvuvi kimoja, Madini kimoja, Viwanda kimoja, Umwagiliaji sita, Usafirishaji vitano na vinginevyo 13.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa uliyonipa na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kutia moyo.

Kwa kuwa Wizara ya Ushirika na Masoko Makao yake Makuu yapo hapa Dodoma na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni jukumu la wanachama wa Vyama vya Ushirika vidogo vidogo kujiunga ili kutengeneza Chama cha Ushirika kwa Mkoa wa Dodoma, lakini kwa vile Wizara ipo hapa Dodoma na Vyama hivi vidogo vidogo ni 127.

Je, isingekuwa ni vema basi Wizara ikasaidia kuwaweka pamoja wanaushirika hawa na kuwaongoza ili waweze kuunda Chama hicho cha Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ilishatolewa ahadi na Wizara hii mara kadhaa ya kuunda Bodi itakayoshughulika na mazao madogo madogo ya alizeti, karanga, mahindi na kadhalika mpaka sasa hivi Bodi hiyo haijaundwa. Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hilo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Makao Makuu ya Wizara hii yapo Dodoma na ni kweli anayekaa jikoni hakosi kunukia nukia viungo. Lakini kuundwa kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa, hitaji la msingi. Je, wanachama wenyewe wa Chama cha Msingi wanahitaji? Kwa sababu Chama Kikuu cha Ushirika kazi yake kubwa ni kuratibu, lakini ndio kinachotumia gharama kubwa zaidi kuliko Vyama vyenyewe vya Msingi. Ukiangalia mseto wa Vyama hivi vya

Msingi katika Mkoa huu vingine vinajihusisha na *SACCOS,* vingine uvuvi na vingine kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, mseto huu mpaka kukubaliana kuunda Chama kimoja cha Ushirika cha Mkoa ambacho kazi yake ni kuratibu tu, lazima wanachama wa Vyama vya Msingi kwanza wawe na imani kwamba Chama hicho hakitowapunguzia mapato yao pia wawe na imani kwamba Chama hicho kitawajengea yale wanayohitaji. Sasa mimi bado nasema, pamoja na kwamba Wizara hii Makao yake yapo hapa Dodoma lakini bado ni jukumu la wanachama wenyewe wa vikundi hivyo 127 pamoja na kikundi kilichoundwa jana cha walimu wastaafu ambacho kinakuwa cha 128, waone kama wanahitaji Chama hicho.

Mheshimiwa Spika, la pili, juu ya Bodi ya Mazao, mimi nafikiri tungeendelea kuchukua zile hatua za kupitia Halmashauri zetu ambazo zimeshaanza najua, lakini Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko atakapokuwa anatoa hoja yake hapa ya Bajeti nafikiri utakuwa ni wakati mzuri zaidi wa kutaka maelezo fasaha juu ya suala hili.

Na. 183

**Uimarishaji wa Kituo cha Polisi Busisi na Kigongo**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa kivuko cha Kigongo –Busisi Mkoani Mwanza kinapitisha magari mengi ya mizigo, mabasi na magari mengine ya abiria na kusababisha misururu mirefu ya magari yanayoegeshwa Busisi na Kigongo usiku baada ya saa za kazi na kwa kuwa katika vituo hivyo kuna vituo vya Polisi kwa ajili ya ulinzi na usalama wa wasafiri na mali zao:-

Je, Serikali itakuwa tayari kujenga vituo vipya na bora vya Polisi Busisi na Kigongo kuweka vyombo vya mawasiliano kama vile Redio, kuongeza askari na kuwapa silaha na usafiri ili kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa vituo vidogo vya Polisi vya Kigongo *Ferry* na Busisi ni vituo muhimu kwa ajili ya ulinzi wa eneo la kivuko cha Kigongo-Busisi Mkoani Mwanza hasa ulinzi wa kivuko (*ferry*) kinachohudumia maelfu ya wasafiri kila siku na kusafirisha magari mengi ya mizigo. Vile vile, hutoa ulinzi kwa wasafiri na mali zao. Pia nakubaliana na Mbunge kwamba vituo hivyo kwa sasa havina hadhi inayotakiwa kwa kuwa havina majengo yenye uwezo wa kutunza silaha na mazingira bora ya kuwawezesha askari kufanya kazi kwa ufanisi. Serikali inauona umuhimu wa kujenga majengo bora zaidi katika vituo hivyo vya Polisi, lakini tatizo letu ni ufinyu wa Bajeti. Tumeanza kuzungumza na wadau wa kivuko hicho, hasa Wizara ya Ujenzi na Halmashauri ya Wilaya husika ili tuunganishe nguvu katika kuboresha vituo hivyo.

Kuhusu vitendea kazi kwa ajili ya vituo hivyo hasa *radio call* na usafiri vitapatikana kadri hali ya Bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini napenda niulize maswali mawili madogo kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa kivuko cha Busisi ni njia rahisi ya kutorokea wahalifu na majambazi kutoka maeneo ya wakimbizi Wilaya za Ngara, Sengerema, Biharamulo, Muleba na kadhalika na kwa kuwa askari waliopo pale Busisi kwa mifano halisi wamewahi kukumbana na majambazi Ukomando bila silaha yoyote. Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka angalau kwa bajeti ya mwaka huu vifaa vya kuanzia vya redio na kuongeza askari?

La pili, kwa kuwa matukio ya ujambazi ni mengi sana sasa hivi kati ya Uhongwa na Kigongo na kati ya Nyitundu na Busisi na kwa kuwa wale wasafiri wanaovuka jioni wanaokwenda Mwanza wanasindikizwa na askari wenye silaha lakini wale wanaovuka kwenda Geita na Sengerema hawasindikizwi. Je, Serikali inatumia vigezo gani katika kufanya hivyo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba tupo tayari na tutafanya hivyo kupeleka vifaa mbalimbali vinavyohitajika kwa ajili ya kazi za Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na silaha. Lakini silaha zina masharti yake huwezi kupeleka silaha kwenye kituo kama cha Busisi kwa jinsi kilivyo ni jengo la udongo na pale tuna *share* na watumiaji wengine wa Kijiji mpaka tupate jengo la kudumu na la uhakika ambalo linajengwa, likiwekewa na hizo *facilities* za kuweka silaha ndio tutapeleka hizo silaha, lakini hivi sasa tunazidi kuimarisha mawasiliano, hivi sasa askari wetu kule tayari wana redio angalau za mkononi za kurahisisha mawasiliano na wenzao kutaka msaada wakati wowote unapohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usindikizaji wa mabasi katika kukabiliana na ujambazi, kigezo kinachotumika ni ukubwa wa tatizo kwa wakati ule uamuzi unapotolewa. Nadhani ulipotoka uamuzi wa kuwasafirisha wale wa Geita ilikuwa tatizo ni kubwa zaidi kwa wakati ule wakati huku kwingine tatizo lilikuwa bado si kubwa. Lakini kama huku kwingine nako tatizo limeanza kuwa kubwa nadhani tutalitazama na tutawasiliana na wenzetu Mkoani kuona uwezekano wa kuanzisha hiyo huduma. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwanza, namshukuru sana mwuliza swali Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyangh'wale, maana ametaja maeneo ya Wilaya yangu na Jimbo langu, lakini swali ni kwamba, kwa kuwa maeneo haya ya Kanda ya Ziwa yamekuwa yakiathirika sana katika shughuli zao za kiuchumi kwa ujumla kutokana na wimbi la kukosekana amani kwa sababu ya kuzagaa kwa wakimbizi na silaha ndogo ndogo na kwa kuwa unakuta Wilaya kama za Sengerema, Geita, Biharamulo, Ngara pamoja na Ukerewe zinaathirika sana. Inabidi wananchi walale mapema badala ya kuendelea na shughuli. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ni vizuri fungu la fedha maalum litafutwe ikiwa ni pamoja na kuomba misaada kutoka kwenye Shirika la Wakimbizi *(UNHCR)* ili tuweze kuwa na vifaa vya kutosha vya kulinda amani ya wananchi katika Kanda ya Ziwa ili wafanye shughuli za kiuchumi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Shija, Mbunge wa Sengerema, kwamba huo ushauri aliotoa tayari tunaufanyia kazi. Hivi sasa tunashirikiana na *UNHCR* (Shirika la Wakimbizi Duniani) kutafuta mahitaji kwa mujibu wa kila mahali kwa Mikoa yote ambayo inaathirika na ujio wa wakimbizi na hasa ukiwemo Mkoa wa Kagera, Kigoma na hata Mwanza ambao unaathirika kwa mbali. Kwa hiyo, nilitaka kumhakikishia hilo kwamba tunalifanyia kazi. (*Makofi*)

Na. 184

## Uraia wa Watu wa Kigoma

**MHE. FRANK G. MAGHOBA (k.n.y. MHE. DR. AMAN W. KABOUROU)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi Mkoani Kigoma, hususan Kigoma Mjini juu ya uraia wao hasa kwa kuzingatia kauli ya kutatanisha aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alipotembelea Mkoa wa Kigoma mwezi wa Pili mwaka huu kuhusu uraia wa watu wa Kigoma na kwa kuwa suala la uraia ni nguzo muhimu sana katika mchakato mzima wa amani na utulivu wa nchi zote:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu uraia wa wenyeji wa Kigoma wakiwemo Wamanyema?

(b) Je, Serikali inasemaje kuhusu uraia wa watu wa kabila la Waha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, suala la uraia wa Tanzania unaongozwa na Sheria ya Uraia Na. 6 ya Mwaka 1995 pamoja na kanuni zake za mwaka 1997. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, kifungu cha 4(i), 5(ii), 6,9 na 11 mtu anakuwa raia wa Tanzania aidha kwa kuzaliwa, kurithi au kwa Tajinisi (kuandikishwa).

Mtu atakuwa raia kwa kuzaliwa iwapo:-

(a) Atakuwa amezaliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Wakati wa kuzaliwa mmoja wa wazazi wake awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu atakuwa raia wa kurithi iwapo:-

(i) Atakuwa amezaliwa nje ya nchi na wazazi raia wa Tanzania.

(ii) Wakati wa kuzaliwa angalau mmoja wa wazazi wake ni raia wa kuzaliwa au wa kuandikishwa lakini sio wa kurithi.

Uraia wa Tajinisi (wa kuandikishwa) unapatikana iwapo mwombaji atakuwa amekidhi masharti ya kupata uraia kwa mujibu wa Sheria ya Uraia.

Baada ya ufafanuzi huu, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Walid Kabourou lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya awali, mtu yeyote anayekidhi sifa zilizoainishwa hapo juu ambazo nimezitaja ni raia wa Tanzania bila kujali kabila, dini wala rangi yake. Hivyo, makabila yote ya Mkoa wa Kigoma yanahusika na Sheria hii kama inavyoyahusu makabila mengine yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kauli za viongozi wa Serikali kikiwemo Chama Tawala na Vyama vya Upinzani wamekuwa wakitumia lugha za kusema baadhi ya Mikoa ni watu wa kuja na hawahusiki hata kupiga kura. Pamoja na sheria aliyoisema Mheshimiwa Waziri, sasa Serikali inatamka nini kuhusu kauli hizo na mambo kama hayo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pia ni Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi. Wala sijawahi kumsikia kiongozi wa Chama cha Mapinduzi akiwaambia Wapinzani ni wa kuja. Ila najua katika maeneo mengi ikiwemo na Kigoma, unapofika wakati wa uchaguzi katika homa zile za uchaguzi na kutafuta njia za kumwengua mwingine, vinatafutwa visingizio vingi na katika maeneo yetu ya mipakani suala la uraia huwa linatumika sana.

Hivi sasa tayari tunazo kesi nyingi za kila mmoja kumtuhumu mwenzie kuwa si raia. Hii inaweza kuwa ndani ya Chama kimoja au inaweza kuwa baina ya Vyama. Kule Kigoma ninayo malalamiko ya Wapinzani wanaowatuhumu wale wanaojitokeza kutaka kugombea kwa CCM kwamba si raia. Ninayo malalamiko pia ya CCM nao wanaowatuhumu wanaojitokeza Upinzani kuwa si raia, pia wamo miongoni mwa CCM wenyewe na miongoni mwa Wapinzani wenyewe. Sasa hiyo ndio hali halisi na ndio ukweli wenyewe na katika mazingira hayo nadhani si halali kukionyesha mkono Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Angalieni saa Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na mimi niongezee swali dogo tu kwenye hili swali la Mheshimiwa Kabourou. Kwa kweli hii hoja ya uraia wa Watanzania hasa wanaokaa pembezoni limekuwa linajitokeza mara kwa mara na unaweza kukumbuka hata akina Jenerali Ulimwengu waliwahi kuambiwa sio Watanzania wakati ni Watanzania na sio yeye peke yake na wengine wengi. Kwa nini sasa Serikali kwa kutumia daftari la kudumu la wapiga kura isiwe kama ndio chombo maalum cha kuwatambua Watanzania halisi wa nchi hii na Serikali itoe tamko kuwa kuanzia sasa ya zamani labda yaachwe ili Watanzania wajulikane ni akina nani na akina nani sio Watanzania? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, nadhani nimeeleza kwa ufasaha nani raia na masharti ya kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunalo tatizo hasa katika maeneo ya mipakani, mzazi mmoja au wazazi wanakuja ndani ya nchi, wanaoa au kuolewa.

Sasa mtoto anapozaliwa, tuliwahi kujibu nadhani hivi karibuni kwamba, mtoto akizaliwa na mmoja wa wazazi wake ni raia wa Tanzania na mwingine ni raia wa nje,

anakuwa na uraia wa nchi mbili mpaka anapotimiza umri wa miaka kumi na nane ambapo ni lazima aukane uraia wa nchi moja.

Sasa tatizo letu tulilonalo ni kwamba, tunao wengi ambao wanatimiza miaka kumi na nane au wanazidi hapo hawaukani uraia wa ile nchi ya nje bali wanajihesabu ni raia na wanataka wapate haki za kiraia. Sasa wanapogunduliwa ndio kunakuwa na matatizo haya kwamba, ameonewa, ameonewa, lakini sheria ipo wazi katika hili. Mimi nadhani sheria zetu zipo wazi na hazina haja ya marekebisho kwa sasa hivi angalau kwa eneo hili. (*Makofi*)

Na. 185

**Ujenzi wa Madarasa**

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa kati ya madarasa yaliyojengwa mwaka 2002 hadi 2004 ni 29,992 kati ya madarasa 41,467 ambayo ni asilimia 72:-

(a) Je, ni madarasa mangapi ambayo angalau yamejengwa kukidhi haja ya watoto wenye ulemavu na ni katika Mikoa ipi kama yapo?

(b) Kama hakuna: Je, ni vipi Serikali itatueleza juu ya utekelezaji wa tamko lake kuwa watoto wote wana haki ya kupata elimu sawa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, watoto wote wana haki ya kupata elimu sawa wakiwemo wenye ulemavu na mahitaji maalum. Katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa MMEM 2002-2006 tathmini iliyofanywa ilibaini kuwa ujenzi wa madarasa katika Halmashauri nyingi haukuzingatia mahitaji ya wenye ulemavu.

Ili kurekebisha kasoro hiyo Wizara yangu iliziagiza Halmashauri zote kuwa katika ujenzi wa madarasa ni lazima kuzingatia vipimo sahihi na michoro maalum iliyoandaliwa na wataalam wa majengo wa Wizara yangu, kwa lengo la kuhakikisha kuwa majengo ya shule yanakidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu kuweza kusoma bila matatizo.

Aidha, kupitia MMEM jumla ya madarasa sita yamejengwa katika shule maalum za wenye ulemavu. Madarasa matatu yamejengwa katika shule ya msingi Mramba, Wilayani Mwanga na mengine matatu katika Shule ya msingi Tumaini Wilaya ya Singida Mjini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inao Mpango wa Elimu Jumuishi. Mpango huu unaziwezesha shule za msingi za kawaida kuandikisha na kuhudumia watoto wenye ulemavu katika madarasa ya kawaida. Katika kutekeleza mpango huu, mwaka 2004/2005 jumla ya walimu 576 wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kufundisha elimu jumuishi ikiwa ni pamoja na kuwafanya waelewe kuwa ni lazima majengo ya madarasa yazingatie malengo na mahitaji ya elimu jumuishi.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametufahamisha kwamba ni madarasa sita tu kwa Tanzania nzima na kwa vile ninafahamu kwamba kuna *standard* za michoro ambayo madarasa yanatakiwa yajengwe. Je, sasa kutakuwa na utaratibu gani wa kufuatilia ili madarasa mengine sasa ambayo yanajengwa katika shule zote yaweze kukidhi haja za hawa walemavu na kuyafuatilia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa vile suala la madarasa linakwenda pamoja na matundu ya vyoo katika vyoo vinavyojengwa katika shule zote hapa nchini. Je, kuna *standard* yoyote ambayo imewekwa katika ujenzi wa hivi vyoo mbali ya kuhesabu tu matundu lakini kuangalia kwamba ni lazima yaweze kuendana pia na wale ambao wana matatizo ya ulemavu na si ulemavu tu na wale wanafunzi wa kike ambao wanatumia hivi vyoo ili wakati wanapojisaidia *at least* waweze kupata mahali labda pa kutundika mabegi yao ili kuweza kutumia vyoo hivi vizuri? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwamba madarasa sita ni machache, hayatoshi, tufanye nini kufuatilia na kusimamia ili yaongezeke madarasa ambayo yamezingatia hali halisi ya wanafunzi walemavu. Nakubaliana naye kabisa kwamba madarasa sita hayo kama anavyosema ni machache, tunahitaji kufuatilia na namshukuru sana yeye mwenyewe hata kuuliza swali hili ni ufuatiliaji mzuri.

Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuhimiza tena kwamba Halmashauri za Wilaya katika kusimamia ujenzi wa madarasa wazingatie michoro iliyotolewa na Wizara yangu hasa katika zile shule zinazotoa elimu jumuishi ambazo zinapokea pia watoto walio walemavu.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwamba sio madarasa tu pia na majengo ya maliwato nayo tuyaangalie kwamba yaangalie hali halisi ya wanafunzi wenye ulemavu pamoja na hali halisi ya wanafunzi wasichana. Kwa huilo namshukuru sana kwa kutukumbusha na napenda kuchukua nafasi hii tena kuhimiza jambo hili.

Kwa kiwango fulani tayari jambo hili linafanyika kwa sababu kwa kweli ukienda kwenye choo cha wavulana na wasichana utakuta kuna hali tofauti. Inawezekana kabisa haviko vile vitu vya kuning'iniza mabegi, lakini ukienda kwenye choo cha wavulana siku hizi tunasisitiza kuweka pia sio matundu tu lakini pia mahali pa kujisaidia ambapo wanasimama ambapo kwa wasichana haiwezekani kuweka, tunaongeza zaidi matundu. Kwa hiyo, upande wa wasichana utakuta matundu ni mengi zaidi na upande wa wavulana utakuta matundu ni machache. Kwa hiyo, yote hiyo ni kuzingatia hali halisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nikiri kwamba, kwa ujumla hata mimi mwenyewe sijaridhika kwa fursa tunazozitoa kwa elimu ya walemavu katika shule zetu, tunahitaji kuziboresha zaidi. Ndiyo maana mkakati mmojawapo ambao Serikali inautumia kwa kugundua kwamba wenzetu wa madhehebu wanaendesha elimu kwa walemavu vizuri zaidi na kwa moyo wa kujituma zaidi, tunatoa ile ruzuku ya maendeleo kwa madhehebu au watu binafsi wanaojenga shule za walemavu.

Tunatoa ruzuku ya maendeleo ya shilingi milioni saba kwa darasa na shilingi milioni tisa kwa nyumba ya mwalimu ili kuwavutia zaidi wanaofanya kazi ya utoaji wa elimu kwa ufasaha zaidi waweze kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tusaidiane kuhimiza jambo hili ili tupate watoaji wa elimu kwa walemavu wengine zaidi ya Serikali ambapo bado tunahitaji kuboresha kile tunachofanya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ili tusiibe muda wa hoja inayofuata, naona saa nne tayari, kwa hiyo, muda wa maswali umekwisha, maswali mawili yaliyobaki yatawekewa utaratibu wa kuyapatia nafasi nyingine. Sasa matangazo ya vikao vya leo ni kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba Wajumbe wake wakutane leo tarehe 1 Julai 2005 katika Ukumbi Namba 219 saa 5.00 asubuhi.

Kamati ya pili, ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Wajumbe wa Kamati hiyo, wanaombwa na Mwenyekiti wao wakutane saa 4.00 asubuhi hii katika chumba Namba 231.

Kamati ya mwisho, ni Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake anawaomba Wajumbe wakutane saa 6.30 mchana ili wakutane na Ujumbe wa *PSRC* na kikao kitafanyika katika Ukumbi Namba 227. Hivyo ndiyo Vikao vya Kamati.

Kuna taarifa kwamba kesho kutakuwa na semina inayohusu kurudusu Sera ya Madini na kama kawaida itaanza saa tatu asubuhi. Mwisho wa Matangazo. Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, tunaomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais - Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Aidha, tunaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, tunapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, akisaidiwa na Makamu wake, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa ushirikiano, ushauri na maelekezo mazuri ya kuboresha bajeti ya mwaka 2005/2006, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu katika kipindi cha miaka kumi ya siasa ya demokrasia ya vyama vingi. Mheshimiwa Rais ametekeleza vema ibara ya 88 ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, kwa kusimamia na kuimarisha Utawala Bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa, kwa mafanikio makubwa sana.

Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha wawekezaji, nchi zilizoendelea na wafadhili mbalimbali, kujenga imani na Serikali yetu, hivyo, kuendelea kutoa misaada pamoja na kutufutia baadhi ya madeni yetu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aendelee kumjalia afya njema kwa kipindi hiki kilichosalia cha Serikali ya Awamu ya Tatu kabla ya kuanza mapumziko yake kama Rais Mstaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tunapenda tumpongeze Mheshimiwa Rais, kwa wadhifa wake wa Uenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, kwa kusimamia kwa umakini mkubwa zoezi la kumtafuta mgombea wa Urais kwa tiketi ya CCM, ambapo Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alichaguliwa kugombea Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, umedhihirisha kuwepo kwa demokrasia ya kweli ndani ya Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzetu, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM,

kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa tiketi ya CCM. Pia, tunawapongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wa Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Tunawatakia ushindi mkubwa katika uchaguzi ujao na tunawapongeza vilevile wagombea wa vyama vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake yenye upeo mpana, ambayo imetoa dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2005/2006. Hotuba yake ni kielelezo kuhusu upevu wake katika uongozi kama mmojawapo wa Washauri Wakuu wa Rais kwa miaka 10 mfululizo chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi. Aidha, tunawapongeza, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao ambazo zimebainisha misingi na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, tunaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzetu, kutoa salamu za rambi rambi kwa ndugu, jamaa, marafiki na Wananchi wa Majimbo ya Uchaguzi ya Mbeya Vijijini, Ulanga Mashariki, Kasulu Mashariki, Rahaleo na Kilombero, kwa kuwapoteza wawakilishi wao, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria na Marehemu Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga.

Aidha, tunatoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha ghafla cha Marehemu Mheshimiwa Margareth James Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, kilichotokea tarehe 23 Juni 2005. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, hotuba yetu itazungumzia maeneo manne, yaani mafanikio ya shughuli za Serikali zinazotekelezwa chini ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu; mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2000; mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2004/2005 na maelezo ya mpango wetu wa mwaka 2005/2006 pamoja na maombi yetu ya fedha za kuutekelezea mpango huo.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 10 ya Serikali ya Awamu ya Tatu, Ofisi ya Rais - Ikulu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuongoza, kufuatilia na kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Rais mwenyewe na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, kitengo cha kuratibu masuala ya Utawala Bora katika Ofisi ya Rais Ikulu, kilichoanzishwa mwaka 2001 kwa lengo la kuratibu programu za Utawala Bora nchini, kimefanya kazi nzuri. Tangu mwaka 2001 hadi 2005, Serikali imeimarisha

utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Utawala Bora na vita dhidi ya rushwa katika sekta zote. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni kuwepo mwamko na uelewa mkubwa miongoni mwa Wananchi kuhusu athari za rushwa kwa jamii; ongezeko la nidhamu katika matumizi ya fedha za umma; ongezeko katika uwekezaji kutoka nje na ndani ya nchi; mikakati ya kupambana na rushwa ya kila Wizara/Idara zinazojitegemea na wakala na uwazi katika mjadala wa tatizo la rushwa hivi sasa kuliko ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Serikali ilitoa mafunzo kwa vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya Kiserikali kuhusu utekelezaji wa mkakati wa kupambana na rushwa. Lengo ni kuongeza uelewa wa umma juu ya tatizo la rushwa ili kutoa ushirikiano katika vita hii. Aidha, katika kipindi hiki, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, liliridhia Mikataba miwili ya Kimataifa ya kupambana na rushwa ambayo ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa *(United Nations Convention Against Corruption, 2003)* na Mkataba wa Umoja wa Nchi za Afrika wa Kupambana na Rushwa *(African Union Convention on Preventing and Combating Corruption, 2003).*

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa Mikataba hii ya Kimataifa kutasaidia Tanzania kushirikiana na Mataifa mengine katika kupambana kikamilifu na kwa ufanisi zaidi dhidi ya rushwa. Faida nyingine zitakazopatikana ni pamoja na kuwa na utaratibu wa kurejesha nchini wahalifu wanaotuhumiwa kwa rushwa, kusaidiana kisheria na kuwa na uwezo wa kuhamisha mashitaka, kuwa na ushirikiano wa taasisi zinazohusika na vita dhidi ya rushwa katika nyanja za uchunguzi na upelelezi wa pamoja, kubadilishana habari na ujuzi. Pia, nchi yetu itaweza kushirikiana na nchi nyingine katika kurejesha nchini mali zilizotoroshwa nje kwa njia ya rushwa, kuwajua watu wanaoishi nje wanaofanya vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia Rushwa nchini (TAKURU), ilianzishwa mwaka 1975 kwa Sheria Namba 2 ya mwaka 1974, wakati huo ilianzishwa kama Kikosi cha Kuzuia Rushwa. Kiliendelea kuitwa Kikosi cha Kuzuia Rushwa hadi 1993 kilipobadilishwa jina na kuitwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Majukumu ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa kama yalivyoainishwa katika Sheria Namba 16 ya mwaka 1971 ni matatu:-

- Kuchunguza na kufikisha mahakamani watuhumiwa wa makosa ya Rushwa;

- Kuelimisha Umma juu na maana na athari zitokanazo na kujihusisha na vitendo vya Rushwa; na

- Kushauri Serikali, taasisi binafsi na Idara zingine juu ya kuziba mianya ya Rushwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ufanisi katika vita dhidi ya rushwa, pamoja na mambo mengine, unategemea utashi wa kisiasa na uadilifu wa kila raia ikiwa ni pamoja na Viongozi na Wananchi wa kawaida. Serikali ya Awamu ya Tatu kwa dhana yake ya Uwazi, Ukweli na Uwajibikaji imeiwezesha TAKURU kuwa na mafanikio yafuatayo:-

- TAKURU imepewa nyenzo za kazi na rasilimali watu wa kutosha katika kukabiliana na tatizo la rushwa. Kutokana na sababu hii TAKURU imeweza kufungua ofisi 123 kuanzia ngazi ya mkoa hadi wilaya zote nchini kutoka ofisi tano za kanda zilizokuwepo mwaka 1995;

- TAKURU imeweza kuchunguza na kufikisha Mahakamani jumla ya kesi 393 toka kesi nane mwaka 1995 kufikia Aprili 2005 ambapo washtakiwa 48 walifungwa vifungo mbalimbali na zaidi ya watumishi 190 wa Serikali walichukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuwasimamisha kazi;

- Katika kutekeleza wajibu wake kupitia chunguzi mbalimbali zilizohusu Wizara ya Ujenzi, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Fedha, Elimu na Utamaduni, TAMISEMI na Mamlaka ya Mapato *(Tanzania Revenue Authority - TRA),* kuhusu mianya ya rushwa, kwa mfano, ukwepaji wa kulipa kodi ya mafuta, vitenge, matairi na betri *(Dry Batteries),* Serikali iliokoa kiasi cha shilingi bilioni 50;

- Uwezo wa TAKURU wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya vitendo vya rushwa umeongezeka kutoka kupokea malalamiko 261 mwaka 1995 na kufikia jumla ya malalamiko 11,434 mwaka 2005 ambapo kwa sasa inaweza kufikisha kesi 60 mahakamani kwa mwaka kutoka kesi nane kwa mwaka 1995;

- Katika uchunguzi na tathmini inayoendelea katika mikoa yote nchini kuhusu matumizi ya shilingi bilioni 241 zilizotolewa na wafadhili kwa serikali chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) tayari mafanikio makubwa yamekwishapatikana katika baadhi ya maeneo; na

- TAKURU imeweza kufanya tafiti katika Shirika la Nyumba la Taifa, Halmashauri za Wilaya na Miji, utoaji wa leseni, usimamizi na utekelezaji wa MMEM, udhibiti wa rushwa katika vituo vya mizani kwenye barabara kuu, udhibiti wa viwango vya ubora wa madawa ya mifugo, ajira za wakurugenzi na ongezeko la vituo vya afya. Matokeo ya tafiti hizo yaliwasilishwa kwenye mamlaka husika na kasoro zilizokuwa kikwazo hapo awali ziliweza kurekebishwa.

Katika miaka kumi ya Awamu ya Tatu, jumla ya mikutano 1,315 ya hadhara ya kuelimisha jamii kuhusu madhara ya rushwa iliendeshwa; mafunzo kwa walimu wakufunzi *(Training of Trainers)* 2,687, vipindi 857 vya "Rushwa Adui wa Haki" na matangazo 502 yanayohusu uelimishaji umma juu ya tatizo sugu la rushwa yalitolewa. Sambamba na hili, machapisho 763,200 yenye ujumbe wa kukemea rushwa yalisambazwa nchini kote. Uelewa wa jamii kuhusu madhara ya rushwa umeongezeka kutokana na programu za kuelimisha jamii. Kwa mfano, idadi ya tuhuma ambazo awali zilikuwa hazifikishwi TAKURU na Wananchi kutokana na kutoelewa haki zao sasa zinafikishwa na kufanyiwa kazi. Wananchi wengi sasa wanatoa ushirikiano kwa TAKURU katika kutoa taarifa kuwa, tayari kutoa ushahidi mahakamani katika kesi zinazoendeshwa na TAKURU na pia kuendelea kukataa kutoa au kupokea rushwa. Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa umekuwa ni dira katika kuwashirikisha

wadau mbalimbali katika maeneo yao kuhusu vita hii kuanzia ngazi ya Wizara, Idara hadi kufikia Mikoa yote nchini na kwa sasa unaendelea katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa jengo la Ikulu ulianza mwaka 1999 na ulikamilika mwaka 2001. Awamu ya pili ulihusu ujenzi wa jengo la mapokezi pamoja na ukarabati wa nyumba kwa ajili ya matumizi ya askari wa ulinzi na kukamilika katika mwaka wa fedha 2004/2005. Vifaa muhimu vya kazi vimewekwa kwenye majengo haya. Kutokana na ukarabati huo, kwa sasa jengo la Ikulu liko katika hali nzuri inayostahili kuwa mahali pa kuishi na kufanyia kazi nzito na nyeti ambazo Taifa letu limemkabidhi Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kama utakavyokumbuka Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alizindua Awamu ya Kwanza ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* tarehe 30 Machi 2000. Miradi ya *TASAF* imelenga kuisaidia jamii katika kujenga uwezo wa Wananchi kujitegemea na kuondoa kero kwao katika maeneo ya elimu, afya, maji, barabara na miundombinu mbalimbali vijijini. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya *TASAF,* pamoja na mambo mengine, umekuwa na mafanikio makubwa kama ifuatavyo: Jumla ya miradi 1,704 imepitishwa na kupewa fedha; miradi 1,338 ikiwa ya Huduma za Jamii, 61 ya makundi maalum na 305 ya ujenzi. Jumla ya miradi 1,431 imekamilika; 1,129 ikiwa ya huduma za jamii, 42 ya makundi maalum na 260 ya ujenzi. Miradi iliyobaki iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Miradi ya ujenzi imeongezeka au kuboreka kwa barabara za vijijini, mabwawa na mifumo ya maji imejengwa/kuboreshwa pamoja na uimarishaji na ujenzi wa miundombinu mbalimbali vijijini. Miradi ya makundi maalum imetoa huduma kwa yatima 1,262, wajane 875, wazee 472 na watoto wengi walio chini ya miaka mitano. Aidha, uhamasishaji juu ya kudhibiti UKIMWI umetolewa kwa Wananchi 30,015. Mafunzo ya usimamizi na uendeshaji bora wa miradi yametolewa kwa Wananchi wapatao 22,230.

Mheshimiwa Spika, mara Serikali ya Awamu ya Tatu ilipoingia madarakani, Novemba 1995 kufuatia Uchaguzi Mkuu wa kwanza ulioshirikisha vyama vingi vya siasa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliahidi kusimamia na kusukuma maboresho yaliyokuwa yakiendeshwa Serikalini ili kujenga utendaji thabiti katika utumishi wa umma. Wakati akiingia madarakani hali ya utumishi Serikalini ilikuwa na upungufu mkubwa uliojidhihirisha katika nyanja zifuatazo:-

- Idadi kubwa ya watumishi ambayo haikujulikana kwa usahihi, ila ilikadiriwa kuwepo kwa watumishi wapatao 360,000;

- Muundo mkubwa wa Serikali uliotokana na Serikali kufanya majukumu mengi yakiwemo yale ambayo siyo ya msingi *(Non-core Functions);*

- Watumishi ambao utendaji wao ulikuwa hafifu kutokana na kukosekana kwa motisha ya kazi, uduni wa maslahi na urasimu usio wa lazima;

- Matumizi makubwa ya Serikali ambayo hayakuzingatia hali halisi ya mapato yake;

- Ukusanyaji hafifu wa kodi na madeni makubwa kwa taasisi zilizokuwa zikitoa huduma Serikalini; na

- Kutozingatiwa kikamilifu kwa matakwa ya katiba ya nchi, sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na hali hii, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Kuboresha Utumishi Serikalini *(Civil Service Reform Program - CSRP)* mwaka 1993 - 1999. Baada ya hapo utekelezaji uliendelea kuongozwa na programu ambayo ilipanuliwa kwa upeo, maudhui na malengo kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1998 na kuitwa Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma *(Public Service Reform Programme)* iliyoanza mwaka 2000 na itatekelezwa hadi mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma ndio nguzo ya Taifa letu. Watumishi wa Umma wanatoa mchango mkubwa katika kulinda na kujenga heshima ya nchi, kudumisha usalama, amani na utulivu na kuiwezesha Serikali kutekeleza shughuli zake ipasavyo. Hivyo, dira yetu ni kuufanya utumishi wa umma kuwa chombo chenye kutukuka, kitakachoiwezesha Tanzania kuwa na uchumi endelevu wenye kuleta matumaini na unaoweza kutokomeza umaskini katika karne hii.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu hii umewezesha sifa na hadhi ya Utumishi wa Umma katika jamii kuongezeka na mazingira ya kazi na vitendea kazi katika Taasisi za Umma kuendelea kuboreka. Mifumo na miundo inaendelea kuimarishwa. Aidha, kiwango cha huduma zitolewazo na watumishi kwa umma zinaendelea kuboreshwa. Mikataba ya huduma kwa mteja imeanza kutekelezwa na Wizara na Idara mbalimbali, ikiwa ni mbinu ya kuhamasisha ufanisi, kuongeza tija na ubora wa huduma na kuimarisha uwajibikaji. Mikataba ya kazi *(Performance Contracts)* na upimaji wa utendaji kazi kwa uwazi kwa kuzingatia vigezo vinavyopimika *(Open Performance Review and Appraisal System - OPRAS),* imeanza kujenga utamaduni mpya wa utendaji kazi unaozingatia matokeo ya kazi na uwajibikaji. Ajira katika utumishi wa umma hivi sasa ni ya ushindani wa wazi na unaozingatia sifa na kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume.

Maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi yanaendelea kuboreshwa. Yote haya yamewezekana kutokana na dhamira ya dhati ya Serikali ya kutekeleza maboresho haya. Aidha, Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi na Utoaji Huduma katika Utumishi wa Umma imejipatia sifa kutoka kwa wadau ndani na nje ya nchi na imeweza kuvutia wahisani mbalimbali kuendelea kutoa misaada kufanikisha malengo ya mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua za marekebisho ya kuboresha utumishi wa umma ili uweze kutoa huduma kwa Wananchi kwa ufanisi zaidi. Kwa

upande wa uendeshaji na menejimenti ya utumishi wa umma, Serikali ilitunga Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya 1998, pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002. Lengo kuu la Sera na Sheria ni kuimarisha uwajibikaji kwa kiwango cha juu wa Taasisi na Watumishi wote katika sehemu zao za kazi. Mfumo ambao umetumika katika kujenga yote haya ni ule ambao unaitwa *Performance Management System (PMS),* utendaji unaojali matokeo ambao umeweka utaratibu thabiti wa uwajibikaji kwa ngazi ya taasisi na kwa ngazi ya mtumishi binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kila mfanyakazi anatimiza wajibu wake, tangu mwaka 2004 Serikali imeanzisha mfumo wa kutathmini na kupima utendaji kazi kwa uwazi kwa watumishi wote *(Open Performance Review & Appraisal System - OPRAS).* Utaratibu huu umeboresha mahusiano kati ya wasimamizi na watumishi walio chini yao na utawezesha kuongeza tija katika utoaji huduma kwani kila mtumishi anatakiwa kuwa na malengo mahsusi ya kazi kulingana na mpango wa kimkakati *(Strategic Plan)* wa Taasisi husika. Aidha, utaratibu huu unaondoa upendeleo katika upandishwaji vyeo, unabainisha misingi ya kutoa mafunzo kwa watendaji kazi na kuweka bayana misingi ya kulipa nyongeza ya mishahara na marupurupu mengine kwa watendaji wazuri.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa mipango ya kimkakati kumewezesha Taasisi za Serikali kuwajibika zaidi katika kufikia malengo makuu ya Kitaifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mkakakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) nchini. Aidha, Serikali imeanzisha mfumo wa kutathmini na kufuatilia utekelezaji wa mipango *(Monitoring and Evaluation System)* katika kila Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali. Hali hii inafanya taasisi zitumie rasilimali (fedha, watumishi, vifaa) kwa mipango thabiti na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Jumla ya Wizara 25 na Idara zinazojitegemea 10 zimeshaanza kutumia mfumo huu na unatarajiwa kukamilika katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali zote ifikapo Novemba 2005.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine unaolenga kuimarisha dhana ya uwajibikaji na kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi na unaotoa kipaumbele kwa wadau ni kuanzishwa kwa Mikataba ya Huduma kwa Mteja *(Clients' Service Charter).* Mikataba hii ni ahadi za taasisi husika kuhusu aina na kiwango cha huduma itakayotolewa kwa Wananchi na pia, inalenga kuboresha utoaji wa huduma. Kutokana na hatua hii, matatizo ya rushwa, ucheleweshaji na kutowajibika, yameweza kupunguzwa. Utaratibu huu mpya ulianza mwaka 2001 na hadi sasa jumla ya Wizara 25, Idara zinazojitegemea 10 na Wakala wa Serikali tatu zina Mikataba hii ambayo inaelezea aina ya huduma inayotolewa, kiwango na muda wa upatikanaji wa huduma husika.

Mheshimiwa Spika, ili kuhahikisha kunakuwepo na kumbukumbu za watumishi zenye uhakika, Serikali imefanikiwa kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za watumishi kulingana na orodha ya malipo ya mshahara *(Integrated Human Resource and Payroll System).* Mfumo huu umewezesha kuwepo kwa kumbukumbu sahihi za watumishi zinazohitajika katika kutayarisha mafao ya kustaafu pamoja na kuhakiki ajira na malipo ya mishahara. Pia, matumizi ya Serikali yaliyotokana na udanganyifu, wizi au ubadhirifu

wa fedha za mishahara kwa watumishi hewa yamepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, kutokana na hatua hizo, imewezekana kugundua na kuwafuta watumishi hewa 15,000 na hivyo kuokoa kiasi cha shilingi 3.0 bilioni kwa mwaka. Aidha, waajiri wamepata uwezo wa kuandaa kwa usahihi zaidi makisio ya watumishi na mishahara na watumishi kulipwa mshahara katika muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha na kuimarisha uhusiano wa kazi kati ya mwajiri na waajiriwa na kuimarisha mazingira ya utawala katika sehemu za kazi za utumishi wa umma, Ofisi hii imesimamia uundwaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi na kuhakikisha yanafanya kazi zake ipasavyo. Pia, ofisi imehakikisha kuwa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini linafanya vikao vyake kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ofisi hii imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma Na.19 ya mwaka 2003. Sheria hii imeyapa nguvu za kisheria Mabaraza ya Wafanyakazi katika sehemu za kazi na imeanzisha Mabaraza ya Majadiliano ya Pamoja katika makundi ya Utumishi mbalimbali katika Utumishi wa Umma *(Service Joint Staff Councils)* na Baraza la Majadiliano ya Pamoja la Utumishi wa Umma *(Public Service Joint Staff Council).* Pia, sheria imetoa fursa kwa waajiriwa na waajiri kujadiliana kuhusu masuala ya ustawi na maslahi ya waajiriwa katika Utumishi wa Umma na hivyo kuepusha migogoro ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Utawala Bora katika Utumishi wa Umma, Ofisi imeweka utaratibu wa kisheria wa namna ya kushughulikia rufaa za watumishi na waajiri hususan katika masuala ya ajira, nidhamu na upimaji wa utendaji kazi. Utaratibu huu umewekwa bayana katika Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, pamoja na Kanuni na taratibu zake za mwaka 2003. Hivi sasa mtumishi yeyote mwenye manung'uniko au malalamiko, ana fursa ya kukata rufaa kuanzia ngazi ya mwajiri wake, Tume ya Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu Kiongozi na hatimaye kwa Rais, ambaye ndiye mamlaka ya mwisho ya rufaa katika ngazi za utawala. Pamoja na misingi hiyo ya kisheria pia kuna taratibu nyingine kama vile taratibu za kushughulikia manung'uniko na malalamiko *(Grievances and Complaints Handling Mechanisms),* ambazo zipo katika hatua za awali za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeweza kwa kiasi kikubwa kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kwa kutunga Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mshahara *(Medium Term Pay Policy)* na Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma Na.2 ya mwaka 1999. Katika uboreshaji huo kima cha chini cha mshahara kimepanda kutoka shilingi 17,500.00/= kwa mwezi mnamo mwaka 1995/96 hadi shilingi 60,000.00/= kwa mwezi mwaka 2004/2005. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 242.9 katika kipindi ambacho mfumuko wa bei umeshuka kutoka zaidi ya asilimia 35 hadi asilimia 4.4. Wastani mishahara imepanda kwa zaidi ya asilimia 300 kutoka shilingi 31,200.00 kwa mwezi mwaka 1995 hadi kufikia shilingi 132,483.00 mwaka 2004/2005. Hali hii imeweza kuwavutia watumishi kujiunga na kubakia katika utumishi wa umma kinyume na ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mfumo wa ulipaji wa mishahara, zoezi la Tathmini na Uchambuzi wa Kazi *(Job-evaluation and Re-grading)* kwa kazi zote muhimu *(Strategic Positions)* katika utumishi wa umma lilifanyika kati ya mwaka 1998 hadi mwaka 2000. Zoezi hili lilituwezesha pia kuhuisha Miundo ya Utumishi *(Schemes of Service)* kutoka 260 iliyokuwepo hadi 163 na kuzipanga kazi katika muundo wa mshahara kwa kuzingatia uzito wa majukumu. Hatua hii imeimarisha uwajibikaji katika utendaji kazi na uwazi katika taratibu za kazi na malipo ya mshahara pamoja na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapa motisha watendaji wazuri, utaratibu wa upandishwaji vyeo, uteuzi wa kushika nafasi za ngazi za juu, kuruhusiwa kujiunga na mashirika mengine ya Kitaifa na Kimataifa kwa utaratibu wa kuazimwa, kushikizwa na likizo bila malipo, ulitumika. Kuanzia mwaka 1995 jumla ya watumishi 1,762 walipandishwa vyeo na kuteuliwa kushika nyadhifa za juu, watumishi 88,599 walipandishwa vyeo kulingana na Miundo ya Utumishi na 2,247 walishikizwa na kuazimwa kwenye taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa maslahi ya Watumishi wa Umma pia umeenda sambamba na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi. Maeneo yaliyotiliwa maanani katika maboresho haya ni pamoja na mazingira ya ofisini ambapo ofisi za Serikali zinaendelea kuboreshwa ili zikidhi kiafya na kikazi. Pia, jitihada zinaendelea kufanywa kuhakikisha kwamba, kila mfanyakazi ana vitendea kazi vya kutosha na vinavyofaa. Kwa ujumla watumishi wa umma hivi sasa wanafanya kazi katika mazingira bora zaidi yanayokidhi mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea kote duniani.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya mwaka 1996 ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Kero za Rushwa ilibainisha kuwa rushwa ni kero kubwa inayotokana na kuporomoka kwa maadili ya utendaji kazi. Kutokana na hali hii, Serikali ilichukua hatua za makusudi ili kuimarisha usimamizi wa maadili kwa kiwango kikubwa na kupunguza vitendo vya rushwa. Hatua hizi zilisaidia kurejesha maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa umma. Mafanikio haya yanathibitishwa na ripoti ya Shirika lisilo la Kiserikali la *Transparency International,* ambayo linaonyesha kuwa viwango vya rushwa vimeendelea kushuka kutoka kiwango cha 1.9 mwaka 1998 na kufikia kiwango cha 3.5 mwaka 2003 (kiwango cha ubora ni 10). Aidha, taarifa ya hivi karibuni ya Benki ya Dunia nayo imethibitisha hivyo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni kutokana na hatua ambazo Serikali ilichukuwa, zikiwemo kutungwa kwa Kanuni za Maadili kwa Utumishi wa Umma na kuanzishwa kwa utoaji wa mafunzo ya wakufunzi wa maadili. Utaratibu huu umejenga uwezo wa watumishi 421 ambao wanaendesha mafunzo ya maadili mahali pa kazi. Aidha, hatua hii inawapa watumishi fursa ya kuyaelewa matatizo ya kimaadili yanayozikabili ofisi zao hivyo kuchukua hatua, jambo ambalo limesaidia kuboresha utoaji wa huduma. Vilevile kuwashirikisha Wananchi katika usimamizi wa maadili ya utumishi wa umma kwa kuwaelimisha kuhusu maadili, sheria mbalimbali za kiutumishi na maboresho.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa utaratibu wa kufuatilia malalamiko ya Wananchi yanayotolewa kwenye vyombo vya habari hasa magazeti na kutoa majibu ya malalamiko hayo kupitia vyombo hivyo, umezifanya ofisi za Serikali kushughulikia kwa karibu malalamiko yanayotolewa kwenye vyombo vya habari ambapo kati ya malalamiko 1,273 yaliyofuatiliwa, uchunguzi wa malalamiko 418 umekamilika na hatua zimechukuliwa. Hali iliyokuwepo ya kupuuzia malalamiko hayo kuwa ni majungu au hayana msingi imeanza kuondoka.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uwezo wa hali ya juu kama ilivyofafanuliwa katika Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1998, Serikali imekuwa ikiandaa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Viongozi na Watumishi mbalimbali. Aidha, maelekezo yametolewa kwa Wizara na Idara zote kuwa na programu za mafunzo kwa watumishi na kutenga bajeti ya kutosha kutekeleza programu hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho jumla ya viongozi na watumishi 14,140 wa ngazi mbalimbali walipewa mafunzo kuhusu mbinu mpya za uongozi, usimamizi, Utawala Bora, teknolojia ya habari, maendeleo ya kilimo na ufugaji, afya ya jamii, utayarishaji wa sera na utekelezaji wake, uendeshaji wa Serikali za Mitaa, mbinu za utafiti wa mahitaji ya mafunzo, usimamizi wa fedha na mbinu za kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujenga uwezo wa watumishi kufanya kazi kwa ufanisi, baadhi ya programu zinalenga pia, kuwa na utaratibu endelevu wenye makusudi ya kuwatambua, kuwavutia na kuwapa stadi zinazohitajika watendaji walioonyesha ujuzi na vipaji katika utumishi wa umma ili kukidhi mpango wa kuwa na watumishi mbadala *(Succession Plan)*. Pia, utaratibu huu ni kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kujaza nafasi za kazi mara moja pale zinapotokea kutokana na matukio ya kustaafu, kuhama na vifo. Hali ya sasa ambapo utumishi wa umma umekuwa ukipoteza watumishi wengi kutokana na janga la UKIMWI umefufua umuhimu mkubwa wa kuwa na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi husika ni pamoja na kukibadili Chuo cha Utumishi wa Umma *(Tanzania Public Service College - TPSC)* kuwa Wakala wa Serikali *(Executive Agency)* na kukiimarisha ili kitoe mafunzo ya uendeshaji, usimamizi, uhazili na utafiti kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji ya watumishi wote wa umma na wadau wengine. Katika kipindi cha miaka mitano, yaani 2001 hadi 2005, Chuo kimefanikiwa kuongeza programu za mafunzo kutoka 27 hadi 123, idadi ya wanachuo kutoka 1,500 hadi 5,195 kwa mwaka na mapato kutoka Shilingi 350,000,000.0 hadi Shilingi 1.5 bilioni kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeweza kuanzisha na kukiimarisha Kituo cha Tanzania cha Mafunzo kwa njia ya Mtandao *(Tanzania Global Development Learning Centre - TGDLC),* kwa watumishi wa umma na wadau wengine. Kituo hiki kimechangia kupunguza gharama ya mafunzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali huendeshwa kwa utaratibu wa kumbukumbu, ofisi yetu imeanzisha mfumo mpya wa utunzaji wa kumbukumbu katika ofisi za Serikali ili kuwa na kumbukumbu sahihi na zinazoweza kupatikana kwa urahisi. Mfumo huu unasaidia kuongeza ufanisi katika kutoa huduma na kupunguza kero kwa Wananchi wakiwemo watumishi. Aidha, Serikali imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Utunzaji wa Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya 2002 *(The Records and Archives Management Act),* ambayo inazipa uwezo mkubwa ofisi katika kusimamia na utunzaji wa kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imefanikiwa kurejesha utaratibu wa kuwepo vitabu vya kuweka kumbukumbu za matukio mbalimbali ya kihistoria Wizarani, Mikoani na Wilayani. Lengo la vitabu hivi ni kuhakikisha kuwa Serikali inaweka urithi wa historia ya nchi yetu vizuri kwa kutunza kumbukumbu andishi kwa vizazi vijavyo. Pia, katika kutunza historia ya nchi, Serikali imechukua hatua ya kutunga Sheria ya Kuwaenzi Viongozi Waasisi wa Taifa letu, yaani Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume *(The Founders of the National Honouring Procedure Act No. 18 of 2004)*. Sheria hii imeweka misingi na mazingira ya kuwa na utamaduni wa kudumu wa kuthamini na kutunza kumbukumbu za Viongozi wa Taifa na udhibiti wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tumeweza kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali kutumia teknolojia ya kompyuta katika kuhudumia umma wa Tanzania. Kupitia mafunzo na matumizi ya vifaa na mifumo ya teknolojia ya habari na mwasiliano, matumizi ya teknolojia ya kompyuta Serikalini yameongezeka sana. Hii imesaidia kuongeza ufanisi wa kazi na kuharakisha utoaji wa huduma kwa umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi hii inasimamia ujenzi wa mtandao wa mawasiliano katika Serikali, yaani Serikali-Mtandao *(e-government).* Kuwepo kwa mtandao huo kutaboresha utoaji wa huduma kwa umma na mawasiliano kufanyika kwa haraka na kwa gharama nafuu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997, Serikali ilitunga Sheria ya Wakala *(Executive Agencies Act No. 30),* iliyokusudia kuzibadilisha idara mbalimbali katika Wizara ambazo majukumu yake ni ya kiuendeshaji zaidi kuwa Wakala za Serikali *(Executive Agencies).* Lengo la mpango huu ni kuvipa vyombo hivi mamlaka zaidi ya kujiendesha kibiashara hasa katika matumizi ya rasilimali na kuvifanya viongeze tija na kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuviondoa katika urasimu wa kiutendaji wa Wizara mama.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa zimeanzishwa Wakala za Serikali 20, hatua ambayo imepunguza kwa kiasi kikubwa, gharama za uendeshaji wa Serikali, imeongeza ubora na ufanisi katika utoaji wa huduma. Mifano ya huduma ambazo zimeboreshwa na Wakala ni pamoja na ukusanyaji wa kodi, usajili na utoaji wa leseni za biashara, uendeshaji wa viwanja vya ndege, usalama wa anga na ujenzi wa nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma mbali mbali ambazo siyo za msingi kuendelea kutolewa na Serikali yenyewe kama huduma za usafi, ulinzi na chakula katika hospitali. Kuanzishwa kwa utaratibu huu, kumewawezesha watumishi wa umma kutumia muda wao kutekeleza majukumu ya msingi. Serikali inaendelea na mpango huu kwa kupanua wigo wa huduma zinazoweza kutolewa na sekta binafsi ambapo unatarajiwa kutoa fursa ya ajira na biashara kwa sekta binafsi ya zaidi ya shilingi bilioni 20 kwa mwaka kuanzia Julai mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, miundo ya Wizara (Idara na Sehemu) imepungua kuliko ilivyokuwa kabla ya mwaka 1997. Idara zimepungua kwa asilimia 20 na Sehemu kwa asilimia ipatayo 90. Pia, baadhi ya huduma zitolewazo na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala, kwa mfano, utoaji wa pasipoti, utoaji wa hati za viwanja, leseni za viwanda, biashara na usafirishaji, zimeendelea kutolewa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanikiwa kuongeza usawa wa jinsia katika utumishi wa umma kwa kuelimisha watumishi wake kuhusu masuala ya jinsia na kwa kuongeza idadi ya wanawake viongozi. Kwa mfano, tangu mwaka 1995 hadi 2005, idadi ya Makatibu Wakuu wanawake imeongezeka kutoka mbili hadi saba, Wakuu wa Wilaya 16 hadi 20, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na Miji 10 hadi 23 na Wakurugenzi wa Wizara kutoka sita hadi 33. Ongezeko hili limekwenda sambamba na ongezeko la Wakurugenzi Wasaidizi wanawake kutoka 16 mwaka 2000 hadi 48 mwaka 2005. Aidha, wanawake 373 wamehudhuria mafunzo ya uongozi na menejimenti ili kuwaongezea sifa zitakazowawezesha kushika nafasi za uongozi. Pia, wanawake wa ngazi za kati na chini 323 walihudhuria mafunzo mbali mbali ili kuongeza ujuzi utakaowawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Wanawake 70 walipatiwa nafasi ya kuchukua mafunzo ya shahada ya pili ambapo 20 tayari wamehitimu mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti maambukizi ya UKIMWI, watumishi 151 walihudhuria mafunzo ya elimu ya UKIMWI ili waweze kuhamasisha watumishi wengine katika sehemu zao za kazi kujikinga na janga hili. Kutokana na hatua hizi uelewa wa watumishi wa umma kuhusu kukabiliana na janga hili umeongezeka. Pia, katika kipindi hiki utafiti kuhusu athari ya UKIMWI katika Utumishi wa Umma umefanywa. Matokeo ya utafiti huu utawezesha uandaaji wa Sera ya UKIMWI katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, uhusiano kati ya Serikali na Wahisani wa Kimataifa umejengeka na kuimarika zaidi. Hali hii imetokana na mafanikio ambayo Serikali imeyapata kutokana na hatua za mageuzi katika kuboresha Utumishi wa Umma. Dhamira ya Serikali, ujasiri na ubunifu katika kutekeleza mageuzi kwa makini imewavutia wahisani kuendelea kutoa misaada kwa Sekta ya Utumishi wa Umma ili kuwezesha uboreshaji wa utumishi wa umma. Tangu mwaka 1993 hadi sasa wahisani mbalimbali wameweza kutoa misaada na mikopo ya masharti nafuu ya jumla ya Dola za Kimarekani 330.0 milioni kwa ajili ya Programmu ya Kuboresha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilianzishwa mwaka 1996 na mpaka sasa imeweza kuimarisha maadili ya viongozi wa umma kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendesha uchunguzi wa malalamiko dhidi ya viongozi wa umma waliolalamikiwa kwa kukiuka maadili, malalamiko yaliongezeka kutoka wastani wa 42 mwaka 2000 hadi 80 mwaka 2004; kutoa mafunzo kwa njia ya redio, magazeti, warsha na machapisho mbalimbali. Jumla ya beramu 7,000, vipeperushi 13,600, nakala 6,700 za Sheria ya Maadili, na nakala 1,400 za Mkataba wa Huduma kwa Mteja zilichapishwa. Jumla ya vipindi 255 vya redio kuhusu maadili ya viongozi vilitangazwa. Aidha, semina 53 kuhusu maadili ziliendeshwa na kuhusisha viongozi mbali mbali.

Ofisi tatu za kanda zilifunguliwa katika Miji ya Arusha, Dodoma na Mbeya na pia ilipokea na kuhakiki tamko la mali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma. Mwaka 1996 viongozi 5,619 walitoa tamko na ahadi na mwaka 2004 waliotoa tamko na ahadi ni 5,368. Sekretarieti ya Maadili iliimarishwa kwa kuajiri watumishi wapya na kuwapa mafunzo; kuandaa marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuongeza idadi ya watumishi mara mbili kutoka watumishi 22 mwaka 1996/97 hadi 56 mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, iliielekeza Serikali kuhakikisha inasimamia utekelezaji wa maadili ya viongozi wa umma kwa mujibu wa Sheria na miiko iliyopo na itakayotungwa. Katika kutekeleza jukumu hili, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- Hivi sasa viongozi wa umma wanatambua umuhimu wa kutaja mali zao na kuonyesha jinsi walivyozipata na hivyo kuweka uwazi kuhusu mali za viongozi hao. Aidha, utaratibu wa kisheria umewekwa kwa Wananchi wanaotaka kuona daftari la mali za viongozi wa umma;

- Wananchi wamehamasishwa kuwafichua viongozi wanaokiuka maadili ya uongozi. Aidha, utaratibu wa kuwasilisha malalamiko dhidi ya viongozi umerahisishwa kwa kuruhusu malalamiko yasiyomtaka mlalamikaji ataje jina lake;

- Wigo wa viongozi wa umma wanaowajibika na Sheria ya Maadili umepanuliwa ili viongozi wengi zaidi wawajibike na Sheria hiyo; na

- Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi imeimarishwa kwa kuipatia watumishi zaidi na vitendea kazi ili, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya umma, iwe na uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Tume ya Utumishi wa Umma mwaka 2004 ni matokeo ya utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Ingawa Tume hii ni changa, kazi yake kubwa ni kuhakikisha kuwa masuala yote ya Utumishi yanaendeshwa kwa Mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu, pamoja na kuhakikisha kuwa ajira katika Utumishi wa Umma inazingatia sifa, uwezo na ushindani, kwa madhumuni ya kufanikisha utendaji wenye malengo na matokeo yanayopimika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja wa uhai wake, tayari Tume imekamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Ajira na Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa katika Utumishi wa Umma. Aidha, mafanikio mengine ya Tume ni kama ifuatavyo:-

- Kukamilisha kazi ambazo zilikuwa zitekelezwe na Tume zilizovunjwa;

- Kuajiri jumla ya watumishi 387 ambapo 213 ni wanaume na 174 ni wanawake;

- Kusajili walimu wapya 3,434 ambapo 1,889 ni wanawake na 1,545 ni wanaume;

- Kupandishwa vyeo watumishi 31,770 ambapo 12,708 ni wanawake na 19,062 ni wanaume. Idadi hiyo inajumuisha watumishi walioshughulikiwa na Idara za Tume;

- Kupandishwa/kuwabadilisha vyeo kwa Mujibu wa Miundo ya Utumishi watumishi 1,617 ambapo 565 ni wanawake na 1,052 ni wanaume. Kati ya idadi hiyo Walimu walikuwa 1,335 na watumishi wa Afya 282;

- Kujadili na kuyatolea maamuzi mashauri ya nidhamu 185 ambapo 28 ni wanawake na 157 ni wanaume. Aidha, kati ya hayo, 173 ni ya walimu na 12 ni ya watumishi wengine;

- Kushiriki katika vikao vya Bodi za Ajira za Halmashauri, Kamati Maalum za Wizara, Idara zinazojitegemea, Kamati za Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Walimu;

- Makamishna wa Tume wametembelea Unguja na Pemba, pamoja na Mikoa kumi na moja ya Tanzania Bara, kwa lengo la kukutana na watumishi wa Umma na kuwaeleza kuhusu Tume yao;

- Kujadili rufaa za watumishi 33 ambapo tano ni wanawake na 28 ni wanaume na kuzifanyia maamuzi na hatimaye kuwajulisha warufani husika;

- Kuandaa mafunzo kwa watumishi wa Tume na Wadau/Waajiri mbalimbali kwa madhumuni ya kuimarisha shughuli za Tume; na

- Kuitangaza Tume kwa njia ya kusambaza vipeperushi, vijarida, kalenda na fulana, kwa waajiri na wadau mbalimbali. Aidha, kipindi cha *Ijue Teachers Service Department (TSD),* kinachorushwa hewani na Redio Tanzania Dar es Salaam kila siku ya Ijumaa saa 12.45 - 1.00 usiku kimekuwa kinawaelimisha Walimu kuhusu Wajibu na haki zao pamoja na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Wananchi ni kupata huduma bora kutoka kwa Serikali yao. Kwa kutambua jambo hili, Ofisi ya Rais na Taasisi zake, kwa pamoja zina majukumu ya kutekeleza kwa ukamilifu maelekezo yaliyomo katika Sera za Chama cha

Mapinduzi kama zilivyofafanuliwa katika Ilani ya Uchaguzi ya 2000, zikisomwa kwa pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya juhudi kubwa katika kurejesha nidhamu, ufanisi, ustahifu, uwezo na utendaji bora wa kazi katika Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, tumeweza kutunga Sera, Sheria, Kanuni, pamoja na taratibu nzuri za usimamizi na utendaji kazi kama misingi ya kujenga Utawala Bora katika nchi yetu. Lengo ni kuwa na utumishi wa umma ambao utatoa huduma kwa Wananchi kwa ufanisi wa hali ya juu, hivyo kujenga imani ya Wananchi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tulivyoeleza hapa juu kuhusu mafanikio ya Ofisi ya Rais, ni wazi kuwa tumeweza pia kuimarisha taasisi zinazosimamia Utawala Bora kama vile TAKURU na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kuzipa nyenzo za kazi pamoja na kuziwezesha kuajiri watendaji wenye sifa. Taasisi zimechangia kwa ukamilifu katika kukuza na kuimarisha Utawala Bora kwa njia mbalimbali kama vile programu za kuelimisha Umma kuhusu madhara ya rushwa kupitia vyombo vya habari na kwa kufanya chunguzi za kubainisha maeneo yenye mianya ya rushwa na kuchukua hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi, nchi yetu imeweza kufutiwa baadhi ya madeni yake kufuatia wafadhili wetu kuridhika na hali ya Utawala Bora. Hiki ni kigezo dhahiri kuwa tumepiga hatua kubwa katika suala la kuimarisha Utawala Bora, jambo ambalo bila shaka litaendelea kuchangia amani na utulivu katika nchi yetu na hivyo, kutuwezesha kujenga uchumi wetu na kuleta maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, ofisi hii iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuongoza, kufuatilia na kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Rais mwenyewe na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, aidha, shughuli za ukarabati wa majengo makuu ya Ikulu unakaribia kukamilika. Hivi sasa majengo ya Ikulu yako katika hali na hadhi inayostahili kuwa mahala pa kuishi Rais na kufanya kazi nzito na nyeti ambazo Taifa letu limemkabidhi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mei 2005, *TASAF* imefanikiwa kutekeleza malengo mbali mbali yafuatayo:-

- Kutoa mafunzo kwa watu 23,419 ambao ni wasimamizi na watekelezaji wa mradi;
- Kutoa mafunzo kuhusu UKIMWI kwa zaidi ya watu 30,000;

- Kukamilisha jumla ya miradi 1,338 kupitia miradi ya jamii na baadhi yake imeshaanza kutoa huduma muhimu;

- Kukamilisha miradi 61 kupitia makundi maalum, kwa mfano, yatima, wazee, wajane, walemavu na waathirika wa UKIMWI, ambayo imesaidia jumla ya watu 2,862;

- Kujenga miradi 305 ya ujenzi;

- Kutoa ajira ya muda kwa walengwa 113,646 kupitia Miradi ya Jamii; na

- Kushirikisha Taasisi 47 zisizo za Kiserikali na kijamii katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, TAKURU iliweza kutekeleza majukumu yake ya kupambana na vita dhidi ya vitendo vya rushwa kama ifuatavyo:-

- Majalada 458 ya uchunguzi yalishughulikiwa na kukamilika na hatua mbalimbali zilichukuliwa kutokana na ushahidi uliopatikana. Aidha, mashauri mapya 60 yalifikishwa mahakamani. Katika uchunguzi huu, jumla ya watumishi wa Serikali 116 walichukuliwa hatua za kinidhamu kwa kusimamishwa kazi na kati yao 70 wamefikishwa mahakamani kujibu tuhuma dhidi yao;

- Jumla ya kesi 216 ziliendeshwa mahakamani, ambapo kesi 29 zilitolewa maamuzi, kati ya hizo kesi sita washtakiwa walifungwa, kesi nane washtakiwa waliachiwa huru, kesi nne ziliondolewa mahakamani kwa sababu mbalimbali na kesi 11 Serikali imekata rufaa. Hadi sasa kesi 188 zinaendelea mahakamani;

- Kuanza kufanya uchunguzi wa matumizi ya fedha zaidi ya Shilingi 241.9 bilioni za MMEM zilizotolewa na wafadhili kwa Serikali kuanzia mwaka 2001/2002 hadi 2003/2004 ili kubaini kama zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa;

- Kufuatilia ili kubaini vitendo vya rushwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uandikishaji wa wapiga kura kwenye Daftari la Kudumu na uteuzi wa wagombea nafasi ya Urais katika vyama vya siasa pamoja na kuwasilisha taarifa zake kwenye mamlaka husika;

- Kufuatilia na kushiriki kwa karibu katika Uchaguzi Mkuu wa Shirikisho la Mpira la Tanzania *(TFF),* ili kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi huo;

- Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu mfumo wa utoaji wa leseni za biashara kwa wawekezaji katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ya biashara za mighahawa, maua na nyinginezo zinazoendeshwa na wawekezaji wageni na Watanzania;

- Usajili wa wanafunzi katika baadhi ya vyuo vya ualimu Daraja IIIA hapa nchini;

- Uhusiano kati ya waajiri au wawekezaji na wafanyakazi katika taasisi na makampuni binafsi. Nia ni kubaini mianya iliyopo ambayo inachangia matatizo ya kutotendewa haki kwa wafanyakazi. Utafiti huu bado unaendelea;

- Warsha ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), ambapo washiriki kutoka Wizara ya Fedha, TAMISEMI na Elimu, walishiriki na kuwasilisha mada. Pia, alikuwepo mwakilishi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali ambaye pia alitoa mada;

- Warsha ya mfumo wa utoaji wa leseni za biashara kwa wafanyabiashara wa kigeni ambapo washiriki walitoka Halmashauri mbalimbali, Kituo cha Uwekezaji, Wizara ya Viwanda na Biashara na Idara ya Uhamiaji;

- Kusambaza nchi nzima majarida yafuatayo: Taarifa ya tafiti zilizofanyika katika kipindi cha Januari - Desemba, 2003; udhibiti wa rushwa katika viwango vya ubora wa dawa za mifugo; Maadili ya Huduma ya Afya Tanzania *(Ethics in Public Health Service in Tanzania);* K

- Kukamilisha maandalizi ya uchapishaji wa majarida yafuatayo: *The Incidences and Effects of Corruption in the Judiciary in Tanzania* na *Incidences of Corruption in the Land Sector;"*

- Maadili katika utoaji huduma katika sekta ya afya;
- Kuendesha mikutano ya hadhara, semina/warsha 675 juu ya mbinu za kupambana na vitendo vya rushwa katika maeneo yao, ambapo Wananchi na watumishi wa umma walishiriki;

- Kutoa mafunzo kwa njia ya redio ambapo jumla ya vipindi 315 kuhusu rushwa vilitangazwa kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam, Redio Maria Songea na Redio Kwizera Ngara, Radio Faraja Shinyanga, Raedio Chemichemi Sumbawanga, Redio Sauti ya Injili Moshi, *Radio Magic FM* na vipindi 27 vya televisheni kuhusu "Rushwa ni Adui wa Haki;"

- Walimu 226 katika Mkoa wa Rukwa, 237 Kigoma na 334 Iringa walipatiwa mafunzo ya ukufunzi ili waweze kufundisha elimu juu ya rushwa katika maeneo yao;

- Kushiriki katika Maonesho ya 28 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam ambapo Wananchi 24,522 walitembelea banda na kupata maelezo/ufafanuzi kuhusu shughuli za TAKURU;

- Kuchapisha na kusambaza nakala 61,000 za kalenda, *posters* 5,000, majarida 108,000 na matangazo 95 kwenye vyombo vya habari;

- Kukamilisha ufunguzi wa ofisi katika Wilaya sita ambazo hazikuwa na ofisi za TAKURU. Aidha, watumishi 209 wameajiriwa kwa madhumuni ya kuimarisha ofisi zote za Wilaya ikiwa ni pamoja na kuzipatia vifaa vya ofisi; na

- Kutoa mafunzo kwa watumishi mbalimbali ambapo watumishi 83 walipatiwa mafunzo ya Uchunguzi Hatua ya Kati *(Intermediate Investigation Course)* na baadhi kuhudhuria warsha, semina na makongamano ya uchunguzi na taaluma nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetekeleza shughuli ilizozipanga na kupata mafanikio kama ifuatavyo:-

- Kuratibu na kuhuisha Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utawala na Utumishi ili ziendane na Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma;

- Kurekebisha Sheria ya Majadiliano ya pamoja Serikalini (1962). Sheria hii sasa inaitwa Sheria ya Majadiliano katika Utumishi wa Umma Na.19 ya mwaka 2003.

- Kukamilisha Kanuni za Utumishi wa Umma (2003) pamoja na Taratibu za uendeshaji kulingana na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya 2002;

- Kuimarisha utaratibu mpya wa kupima utendaji kazi kwa uwazi ili kuondoa uonevu na upendeleo, na kuimarisha uwajibikaji;

- Kuratibu ajira na kupandishwa vyeo kulingana na matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002;

- Kuimarisha taarifa za kiutumishi *(Human Resource Data Base)* zilizo katika mfumo wa kompyuta;

- Kutoa mafunzo kwa watendaji mbalimbali Serikalini kwa madhumuni ya kuchochea mabadiliko ya fikra kuhusu dhana ya utendaji kazi unaozingatia matokeo *(Performance Management)* katika Utumishi wa Umma;

- Kutoa mafunzo ya utekelezaji wa upimaji utendaji kazi uliowazi (*OPRAS)* kwa Wizara na Idara zinazojitegemea 34;

- Kutoa mafunzo kwa viongozi waandamizi kuwawezesha kusimamia mabadiliko ya mifumo ya utendaji kazi Serikalini;

- Kufadhili watumishi 78 kutoka Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa mbalimbali katika kozi za *Microsoft Access* na *Microsoft Project* ili kujenga uwezo wao katika kutekeleza mfumo wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Programme ya kuboresha Utumishi wa Umma;

- Kurusha jumla ya vipindi 108 kupitia Redio na Televisheni kwa lengo la kuelimisha Umma kuhusu Maadili, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma;

- Kujenga uwezo wa Wizara na Idara za Serikali kusimamia na kukuza maadili, ambapo jumla ya watumishi 91 walipatiwa mafunzo ya ukufunzi, maofisa 35 walipatiwa mafunzo kuhusu maadili, utawala bora na rushwa;
- Kukamilisha uwekaji wa mifumo ya uboreshaji wa utunzaji kumbukumbu za utawala na watumishi katika Wizara zote 25 na Idara Zinazojitegemea kumi. Aidha, zoezi la uanzishaji wa mifumo hii katika mikoa limeanza na litaendelea katika mwaka wa 2005/2006;

- Kuwezesha Wizara na Idara Zinazojitegemea 34 na Sekretarieti za Mikoa 21 kutekeleza Mipango yao ya Kimkakati *(Strategic Plans)* kwa nia ya kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi;

- Kugharamia mafunzo ya uzamili kwa wanawake ili kuongeza idadi ya wanawake wenye shahada zaidi ya moja katika utumishi wa umma ambapo wanawake 50 walinufaika na mafunzo haya;

- Kusimamia na kugharamia utafiti kuhusu menejimenti ya UKIMWI na masuala mbalimbali *(Diversity Issues)* katika utumishi wa umma;

- Kuhuisha miundo na majukumu ya Wizara nne (TAMISEMI, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Ulinzi) na kutengeneza majukumu na muundo wa Tume ya Pamoja ya Fedha inayoshughulikia masuala ya fedha za Muungano; na

- Kuwezesha Wizara za Afya, Maliasili na Utalii, Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu pamoja na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hospitali za Mikoa ya Morogoro na Dodoma kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, ofisi hii iliendelea na mkakati wa kuelimisha umma kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika Sekta ya Utumishi wa Umma kupitia Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma. Baadhi ya njia zilizotumika ni kutumia makala kwenye magazeti, kupitia mikutano na watendaji mbalimbali, vipeperushi, majarida, radio televisheni (vipindi vya tujirekebishe) na maonesho kama siku ya Utumishi wa Umma ambayo inaadhimishwa kila tarehe 23 Juni ya kila mwaka, Sabasaba na Nanenane.

Kwa upande wa siku ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka huu tumejumuika na Wizara na Idara nyingine kumi na tano kuonyesha na kuelezea huduma mbalimbali zinazotolewa na vyombo husika. Pia, tulitumia jumuiko hilo kukusanya matatizo na maoni mbalimbali kuhusu huduma zitolewazo na vyombo husika. Maoni na matatizo yaliyojitokeza yatafanyiwa kazi kama sehemu ya kuondoa kero zinazowakabili wananchi kutoka sekta ya utumishi wa Umma. Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza asasi zilizoshirikiana nasi na kuzialika nyingine kwenye maonesho ya miaka ijayo ili kuweza kujenga uelewa kwa wananchi wa huduma tuzitoazo kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika miaka 10 ya Serikali ya Awamu ya Tatu, Serikali imeweza kuimarisha maadili ya viongozi wa Umma kwa kuendesha uchunguzi dhidi ya

Viongozi wa Umma wanaolalamikiwa, kutoa mafunzo kwa viongozi kwa njia ya redio, magazeti, warsha na semina kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili kwa ngazi mbalimbali za uongozi katika utumishi wa Umma. Ili kusogeza huduma karibu na wananchi Sekretarieti imefungua ofisi katika kanda tatu, Arusha, Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Tume ya Utumishi wa Umma mwaka jana (2004) ni matokeo ya utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Kazi kubwa ya Tume ni kuhakikisha kuwa masuala yote ya Utumishi yanaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu, pamoja na kuhakikisha kuwa ajira katika Utumishi wa Umma inazingatia sifa, uwezo na ushindani kwa madhumuni ya kufanikisha utendaji wenye malengo na matokeo yanayopimika. Katika kipindi cha mwaka mmoja wa uhai wake tayari Tume imekamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa katika Utumishi wa Umma. Aidha, mafanikio mengine ya Tume ndani ya kipindi hiki kifupi ni kama yafuatayo:-

- Kukamilisha kazi ambazo zilikuwa zitekelezwe na Tume zilizovunjwa;

- Kuajiri jumla ya watumishi 387 ambapo 213 ni wanaume na 174 ni wanawake. Aidha, Tume imesajili Walimu wapya 3,434 ambapo 1,889 ni wanawake na 1,545 ni wanaume;

- Kupandishwa vyeo watumishi 31,770 ambapo 12,708 ni wanawake na 19,062 ni wanaume. Idadi hiyo inajumuisha watumishi walioshughulikiwa na Idara za Tume;

- Kupandishwa/kuwabadilisha vyeo kwa Mujibu wa Miundo ya Utumishi watumishi 1,617 ambapo 565 ni wanawake na 1052 ni wanaume. Kati ya idadi hiyo Walimu walikuwa 1,335 na watumishi wa Afya 282.
- Tume ilijadili na kuyatolea maamuzi mashauri ya Nidhamu 185 ambapo 28 ni wanawake na 157 ni wanaume. Kati ya hayo, 173 ni ya Walimu na 12 ni ya watumishi wengine;

- Tume ilishiriki katika vikao vya Bodi za ajira za Halmashauri, Kamati Maalum za Wizara, Idara zinazojitegemea, Kamati za Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Walimu;

- Makamishna wa Tume wametembelea Unguja na pemba pamoja na Mikoa kumi na moja ya Tanzania Bara kwa lengo la kukutana na watumishi wa Umma na kuwaeleza kuhusu Tume yao;

- Kujadili rufaa za watumishi 33 ambapo tano ni wanawake na 28 ni wanaume na kuzifanyia maamuzi na hatimaye kuwajulisha warufani husika;

- Kuandaa mafunzo kwa watumishi wa Tume Wadau/Waajiri mbalimbali kwa madhumuni ya kuimarisha shughuli za Tume; na

- Kuitangaza Tume kwa njia ya kusambaza vipeperushi, vijarida, kalenda na fulana kwa waajiri na wadau mbalimbali. Aidha, kipindi cha *Ijue Teachers Service Department*

*(TSD),* kinachorushwa hewani na *RTD* kila siku ya Ijumaa saa 12.45 - 1.00 usiku kimekuwa kinawaelimisha Walimu kuhusu Wajibu na haki zao pamoja na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Ofisi ya Rais Ikulu itaendelea kuongoza, kufuatilia, kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali na kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya kisera na miswada ya sheria kwa lengo la kumshauri Rais na Baraza la Mawaziri. Kazi nyingine zitakazofanywa ni pamoja na kukamilisha sera ya mawasiliano kwa umma, kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kiserikali kwa wananchi na kuratibu utendaji wa kazi wa vyombo vya dola kuhusu usalama wa Taifa. Vilevile, mafunzo mbalimbali yatatolewa kwa watumishi kwa ajili ya kuboresha utendaji wao wa kazi na kusimamia shughuli za uendeshaji wa ofisi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ofisi itaanza rasmi utekelezaji wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA), ambao umebuniwa na Serikali kama sehemu ya MKUKUTA. Madhumuni ya MKURABITA ni kuandaa mfumo wa kitaifa wa umiliki mali na uendeshaji biashara utakaoainisha na kuboresha kanuni na taratibu zinazotumiwa na makundi mbalimbali nchini na kuwa na mfumo mmoja wa kisheria. Jitihada hizi zitawawezesha walengwa kuutumia mfumo huo kupata mitaji ya kugharamia shughuli za kiuchumi. Aidha, mpango huu una lengo la kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa soko rasmi la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, MKURABITA itafanya yafuatayo:-

- Kupendekeza marekebisho ya sheria au utayarishaji wa sheria mpya za umiliki mali na uendeshaji wa biashara;

- Kupendekeza mfumo wa utekelezaji, kubaini taasisi husika na kugawa majukumu;

- Kuandaa mfumo wa ushirikishwaji wadau; na

- Kutathmini gharama za utekelezaji wa mpango mzima wa urasimishaji na kuweka vigezo au viashiria vya kutathmini matokeo.

Mheshimiwa Spika, TAKURU imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika kipindi cha mwaka 2005/2006:-

- Kuendelea na uchunguzi wa majalada 3,643 na mengine yatakayofunguliwa kutokana na malalamiko yatakayopokelewa;

- Kukamilisha majalada yanayohusu uchunguzi maalum wa mapunjo ya mishahara ya walimu dhidi ya baadhi ya watumishi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu. Pia kuendelea na uchunguzi wa MMEM;

- Kuendesha kesi 188 zilizopo mahakamani pamoja na zitakazofunguliwa kwa kipindi hicho;

- Kuendelea kufuatilia kampeni za uchaguzi mkuu 2005 ili kubaini vitendo vya rushwa katika shughuli za kampeni;

- Kufanya tafiti tano kuhusiana na shughuli mbalimbali zenye lengo la kuziba mianya ya rushwa na kuondoa kero mbalimbali kwa Wananchi.
- Kutoa mafunzo ya awali *(Basic Investigation Course)* kwa wachunguzi wapya 130 na mafunzo ya kati *(Intermediate Investigation Course)* kwa wachunguzi 150;

- Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya haki zao, madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana na kujiepusha na vitendo vya rushwa;

- Kuchapisha kalenda 135,000, vipeperushi 1,200,000, *stickers* 5,000, *posters* 25,000 na vijarida 1,460,000. Aidha, Taasisi itaandaa matangazo 96 ya kukemea rushwa kwenye magazeti, matangazo 208 kwenye televisheni na 208 kwenye redio;

- Kutangaza vipindi 416 Raeio Tanzania Dar es Salaam, Redio Maria Songea, *Radio Country FM* na Redio Kwizera Ngara, pamoja na redio nyingine nchini. Aidha, TAKURU itarusha vipindi vya moja kwa moja *(live),* wakati wa Maonesho ya Kitaifa ya Sabasaba kupitia televisheni.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa *TASAF* katika wilaya 40 za Tanzania Bara na visiwa vya Pemba na Unguja kwa upande wa Zanzibar, Serikali iliamua kuwa na awamu ya pili ya *TASAF* ambayo itatekelezwa katika halmashauri zote za wilaya, miji na manispaa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2005 hadi 2009. Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Dunia iliridhia na kupitisha mradi wa awamu ya pili ya *TASAF* tarehe 30 Novemba, 2004. Mkataba kati ya Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulisainiwa tarehe 19 Januari 2005. Madhumuni ya awamu ya pili ya *TASAF* ni kujenga uwezo wa jamii ili iweze kutumia fursa zilizopo kubuni, kutekeleza na kufuatilia miradi inayoweza kuchangia kuinua hali ya maisha kwa kuzingatia malengo ya Maendeleo ya Milenia kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania. Hivyo, awamu hii ni mojawapo ya hatua za serikali za kutekeleza MKUKUTA na itakuwa na sehemu kuu mbili:-

Mfuko wa Taifa wa Kijiji utatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi itakayolenga makundi yafuatayo:-

- Jamii maskini zisizokuwa na huduma za jamii kama vile huduma za afya, elimu, maji na usafi wa mazingira, barabara na huduma za kibenki. Jamii zitakazotekeleza miradi katika kundi hili zitachangia kiasi kisichopungua asilimia ishirini ya gharama za mradi, ikiwa ni fedha na/au vifaa na nguvu kazi, isipokuwa miradi ya maji ambapo mchango wa jamii ni kiasi kisichopungua asilimia tano;

- Kaya maskini lakini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi zinazokabiliwa na uhaba wa chakula. Walengwa katika kundi hili watapatiwa ajira ya muda katika miradi ambayo watashiriki kuitekeleza katika ngazi ya jamii ambayo itawaongezea kipato, ili kuwawezesha kupata chakula na mahitaji mengine ya msingi. Pia watapata fursa za kupata stahili ambazo zitawasaidia wasitumbukie katika hali mbaya zaidi ya umaskini; na

- Makundi maalum katika jamii kama yatima, walemavu, wazee, wajane, wagonjwa wa muda mrefu na waathirika wa UKIMWI. Walengwa katika kundi hili wanaweza kushirikiana na asasi zisizokuwa za kiserikali katika kutekeleza na kusimamia miradi yao. Mchango wa jamii kwa miradi ya makundi maalum utakuwa kiasi kisichopungua asilimia tano.

Katika sehemu hii kundi la walengwa katika ngazi ya jamii litakalosaidiwa ni wale ambao watapenda kujiunga katika vikundi vya kuweka akiba vyenye idadi ya wanachama wasiopungua kumi kwa kila kikundi na wadau mbalimbali watakaosaidia jamii kutumia vizuri michango inayotoka Mfuko wa Kijiji.

Mheshimiwa Spika, sekta zimeandaa miongozo ya ushiriki wa jamii katika huduma za sekta husika. Miongozo hiyo ya sekta itaonyesha aina ya miradi inayoweza kutekelezwa na jamii na ndiyo miradi pekee ambayo itachangiwa na *TASAF*. Sekta zitakazotoa miongozo ni afya, elimu, maji, ustawi wa jamii, uvuvi, chakula na ushirika, barabara, misitu, madini, benki na masoko. Miradi yote itakayochangiwa na *TASAF* itahakikiwa ili kubaini kama utekelezaji wake hautasababisha athari za mazingira. Aidha, hatua za kuhifadhi mazingira kwa miradi ambayo utekelezaji wake utasababisha athari lazima zichukuliwe mapema.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa umma kwa mwaka 2005/2006, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha uwekaji wa mifumo ya utendaji kazi *(Performance Management Systems)* katika mikoa na asasi nyingine za Serikali;

- Kushirikiana na Wizara ambazo tayari zimeanzisha Mifumo ya Utendaji Kazi kwa lengo la kufuatilia utekelezaji na uimarishaji wa Mifumo hiyo;

- Kuendelea kubadilisha Idara nne za Serikali kuwa Wakala pamoja na kuendelea kuimarisha wakala ambazo tayari zimezinduliwa;

- Kuendelea na mipango ya kushirikisha sekta binafsi katika utoaji huduma katika Wizara Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Hospitali za Rufaa na Mikoa;

- Kupitia mifumo na taratibu za kazi zilizopo na zinazotawala utumishi wa umma, pamoja na kuoanisha taratibu hizo na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002;

- Kutekeleza sera ya Muda wa kati ya mishahara kwa madhumuni ya kuboresha maslahi ya watumishi kama motisha wa kuongeza ufanisi na tija ambapo Serikali imetenga jumla ya Shilingi 681.897 bilioni kwa mwaka wa fedha 2005/2006, kwa ajili ya kugharamia mishahara ya watumishi. Aidha, hii ni ongezeko la asilimia 23.7 ikilinganishwa na jumla ya Shilingi 551.15 bilioni zilizotengwa kwa mwaka 2003/2004;

- Kutumia teknolojia mpya katika kutunza kumbukumbu za watumishi ili kuboresha usimamizi hususan katika eneo la matayarisho ya ikama na bajeti ya mishahara na pia kurahisisha utoaji wa maamuzi ya kiutumishi na utawala;

- Kuratibu utoaji wa vibali vya ajira na usahihi wa malipo ya mishahara kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuondokana na tatizo la ubadhirifu wa fedha za Serikali;

- Kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa umma zinazingatiwa na watumishi wote wa umma katika utekelezaji wa majukumu yao na utoaji huduma;

- Kuandaa na kusambaza miongozo ya *ICT* na viwango vinavyotakiwa kulingana na mpango wa Sera ya Serikali mtandao *(e-Government Strategy);*

- Kuanzisha Mifumo ya kutunza kumbukumbu hai na tuli *(Current and Semi-current)* katika Wizara na Idara Zinazojitegemea;
- Kujenga kituo cha Taifa cha Kumbukumbu *(National Records Centre)* na kuanzisha kituo cha Waasisi wa Taifa la Tanzania *(Establishment of the Founders of the Nation Centre);*

- Kujenga kituo cha *Network Management Centre* kwa ajili ya kusimika vifaa mbalimbali vya Serikali mtandao *(e-Government);*

- Kuendelea kuwezesha Wizara na Idara zinazojitegemea katika suala la kuendeleza Rasilimali-watu;

- Kuanzisha utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kuchochea mwamko kuhusu maadili ya kiutumishi katika Utumishi wa Umma;

- Kuendelea kugharamia mafunzo ya shahada ya pili kwa wanawake 40;

- Kutoa mafunzo ya ujuzi mbali mbali kwa wanawake 150, mafunzo ya jinsia kwa watumishi wapya 25 pamoja na kuwapatia mafunzo maalum watumishi 75 wanaoshughulikia masuala ya jinsia katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala;

- Kuandaa sera ya UKIMWI katika utumishi wa umma;

- Kukamilisha utafiti wa masuala mbali mbali *(Diversity Issues)* katika utumishi wa umma ambapo matokeo yake yatahuishwa katika sera, kanuni na taratibu za utendaji kazi; na

- Kuimarisha Chuo cha Utumishi wa Umma kwa kukijengea uwezo wa rasilimali-watu na miundombinu ili kiweze kutoa mafunzo ya uongozi, utawala na menejimenti kwa watumishi wa umma wa ngazi zote na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

- Kuchunguza malalamiko toka kwa wananchi dhidi ya viongozi mbalimbali wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya viongozi;
- Kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Sheria;

- Kutoa elimu ya maadili ya Uongozi wa Umma na viongozi kwa njia ya Redio, semina na machapisho mbalimbali;

- Kuajiri watumishi wapya, kununua vitendea kazi na samani kwa ajili ya ofisi za Kanda za Tabora, Mtwara na Mwanza; na

- Kuwapatia watumishi wa Sekretarieti mafunzo ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi 2005/2006, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kushughulikia rufaa za watumishi, waajiri na mamlaka za nidhamu;

- Kuwaelimisha watumishi na Wadau kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma;

- Kutoa miongozo mipya kuhusu masuala mbalimbali ya Utumishi wa Umma;

- Kufanya ufuatiliaji, ukaguzi na tathmini ya uzingatiaji wa Miongozo ya Ajira na nidhamu;

- Kuandaa mafunzo kwa watumishi wa Tume ili kuwajengea uwezo; na kutoa elimu kwa Umma kuhusu shughuli za Tume kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya kwa sehemu kubwa yametokana na msukumo mkubwa ambao Serikali imeutoa katika utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma *(Public Service Reform*

*Programme).* Hata hivyo, bado kunatakiwa juhudi zaidi ili kufikia lengo kubwa la kuwa na Utumishi wa Umma unaoheshimika na unaotegemewa kikamilifu. Hatua za kubadilisha fikra, utamaduni na maadili kwa watumishi wa umma, zinahitaji muda mrefu wa kutekeleza maboresho haya mfululizo. Hivyo, ni vyema Serikali iendelee na msukumo wa kuleta mabadiliko muhimu katika utendaji kazi na kutoa huduma kama ilivyofanya katika kipindi hiki cha miaka 10.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na misaada toka nchi rafiki na mashirika mbalimbali. Natumia nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo: Uingereza, Uholanzi, Malaysia, India, Ujerumani, Australia, New Zealand, Singapore, Pakistan, Misri, Thailand, Uswisi, Benki ya Dunia, *NORAD, JICA, UNDP, UNIDO, DANIDA, CIDA, DFID, SIDA, USAID, ACBF,* Jumuiya ya Madola na Jumuiya ya Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hotuba yetu, tunapenda kuwashukuru Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Matern Y.C. Lumbanga, Katibu Mkuu (UTUMISHI), Ndugu Joseph A. Rugumyamheto, Katibu Mkuu (Ikulu) Ndugu Abel W. Mwaisumo, Wenyeviti, Makatibu wa Tume na Taasisi mbalimbali na Watumishi wote walioko katika Wizara, Mikoa, Wilaya na Idara zinazojitegemea, siyo tu, kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaotoa katika kufanikisha malengo ya Serikali katika sehemu zao za kazi, bali pia kwa mchango wao uliowezesha matayarisho ya hotuba hii ya bajeti. Aidha, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wenu mzuri katika kipindi chote hiki cha miaka mitano cha uhai wa Bunge letu hili na tunawatakia kheri na kumwomba Mwenyezi Mungu ili tuweze kuchaguliwa tena kuendelea kusimamia na kuchangia maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Aidha, tunapenda kuwashukuru watumishi wote kwa ujumla, kwa kuitikia wito wa kujituma, kutoa huduma bora na kwa ufanisi kwa kujirekebisha.

Mheshimiwa Spika, tungependa vilevile kuwashukuru sana familia zetu mimi Mheshimiwa Mary Nagu na Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa kutupa msaada wa hali na mali kuweza kufanikisha malengo ya kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi tulioutoa hapa juu, ambao umeonesha hali ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma, kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, pamoja na mpango wa kazi kwa mwaka 2005/2006, tunaomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee maombi yetu ya fedha, ambayo yanafikia jumla ya Sh.204,858,023,800.00/=, kwa ajili ya kugharamia mpango wa kazi kwa mwaka 2005/2006 kwa mgawanyo ufuatao:-

(a) Fungu 20 - Ikulu:
- Matumizi ya kawaida Sh. 4,909,472,000.00/=

(b) Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri:
- Matumizi ya Kawaida Sh. 78,933,436,600.00/=

- Mpango wa Maendeleo Sh. 58,097,143,000.00/=

**Jumla Sh.137,030,579,600.00/=**

(c) Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma:

- Matumizi ya Kawaida Sh. 6,225,036,800.00/=
- Mpango wa Maendeleo Sh. 48,940,000,000.00/=

**Jumla Sh. 55,165,036,800.00/=**

(d) Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma:

- Matumizi ya Kawaida Sh. 1,161,680,400.00/=

(e) Fungu 94 -Tume ya Utumishi wa Umma:

- Matumizi ya Kawaida Sh. 6,476,255,000.00/=
- Mpango wa Maendeleo Sh. 115,000,000.00/=

**Jumla Sh. 6,591,255,000.00/=**

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunapenda kukushukuru tena wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kutusikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nitoe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa Kazi katika Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2004/2005 na Maoni ya Kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kwa niaba ya Kamati, ninaomba nitoe pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, kwa msiba mkubwa walioupata wa kuondokewa na ndugu yao huyo mpendwa pia mwenzetu katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani pia kwako wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kusoma taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004. Sasa naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Kazi katika Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishatamka nilipowasilisha Taarifa ya Kamati yangu kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, mojawapo kati ya majukumu ya Kamati hii pia ni kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi hii, Kamati ilipata fursa ya kuchambua Bajeti ya Ofisi hizi tarehe 1 Juni 2005 katika kikao kilichofanyika Dar es Salaam. Katika Kikao hicho Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa kazi uliofanywa na ofisi hizo kwa mwaka wa fedha 2004/2005 na kupokea maelezo kuhusu Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) kwa mafungu yafuatayo: Fungu 20 - Ikulu, Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Fungu 32 - Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) yamo katika kitabu cha maelezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2005/2006, kilichowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 1 Juni 2005.

Mheshimiwa Spika, katika ujumla wake lengo la mafungu niliyoyataja ni kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo na kwamba, utumishi wa umma utakuwa chombo chenye kutukuka, kinachowezesha watumishi wa umma kutoa huduma bora kwa Wananchi na kwa sekta zote za uzalishaji ili kujenga uchumi wa nchi yetu unaokua na unaowezesha kutokomeza umaskini na kuleta maisha bora kwa Watanzania. Katika kufikia lengo hili, ofisi hizi mbili zina jukumu la kusimamia na kuratibu kazi na kujenga uwezo wa watumishi ili wafanye kazi zao kwa misingi ya uadilifu, uwajibikaji na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilitekeleza shughuli ilizopanga kwa ufanisi mkubwa. Shughuli hizo ni pamoja na kuratibu na kuhuisha Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utawala na Utumishi ili ziendane na Mpango wa Kuboresha Utumishi wa Umma; Kuimarisha utaratibu mpya wa kupima utendaji kazi kwa uwazi ili kuondoa uonevu na upendeleo na kuimarisha uwajibikaji; Kuratibu ajira na kupandishwa vyeo kulingana na matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 na kukamilisha uwekaji wa mifumo ya uboreshaji kazi katika Wizara zote 25 na Idara Zinazojitegemea kumi.

Aidha, Sektretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma zimeweza kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mafanikio makubwa. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma 5,368 kwa mujibu wa sheria; kuchunguza malalamiko 51 ya Wananchi dhidi ya viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya viongozi; kutoa elimu kwa viongozi juu ya umuhimu wa kuzingatia maadili ya viongozi na kwa Wananchi juu ya wajibu wao katika kujenga safu ya viongozi

wanaozingatia maadili kwa njia mbalimbali ikiwemo redio, semina na machapisho mbalimbali kama vipeperushi, beramu na kadhalika.
Kwa upande wa Tume ya Utumishi wa Umma mafanikio yaliyopatikana ni kukamilisha kazi ambazo zilikuwa zitekelezwe na Tume zilizovunjwa; kuajiri jumla ya watumishi 387 katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni na kusajili walimu wapya 3,434 pamoja na kuthibisha kazini watumishi 287, kupandisha vyeo watumishi 31,770 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilifahamishwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Ikulu iliendelea kuratibu, kusimamia na kupima utekelezaji wa programu ya kujenga Utawala Bora nchini na hasa kuhakikisha kwamba, Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa unatekelezwa ipasavyo. Aidha, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) iliweza kutekeleza majukumu yake ya kupambana na vita dhidi ya vitendo vya rushwa kwa kufanya kazi zifuatazo: Kushughulikia na kukamilisha majalada 458 ya uchunguzi na kuchukua hatua mbalimbali kutokana na ushahidi uliopatikana; kuendesha jumla ya kesi 216 mahakamani; kuanza kufanya uchunguzi wa matumizi ya fedha zaidi ya sh. bilioni 241.9 za Mfuko wa Elimu (MMEM) zilizotolewa na Serikali pamoja na wafadhili kuanzia mwaka 2001/2002 hadi 2003/2004 ili kubaini kama zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na Serikali; kufuatilia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na uandikishaji wa wapiga kura kwenye daftari la kudumu na vitendo vya rushwa katika uteuzi wa wagombea nafasi ya Urais katika vyama vya siasa pamoja na taarifa zake kuwasilishwa mamlaka husika, na shughuli nyinginezo.

Kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* pamoja na mambo mengineyo ulifanikiwa kutekeleza yafuatayo: Kutoa mafunzo kwa watu 23,419 ambao ni wasimamizi na watekelezaji wa mradi; kutoa mafunzo kuhusu UKIMWI kwa zaidi ya watu 30,000; kukamilisha jumla ya miradi 1,338 kupitia Miradi ya Jamii na baadhi yake imeshaanza kutoa huduma muhimu; kukamilisha miradi 61 kupitia miradi ya Makundi Maalum, kwa mfano, yatima, wazee, wajane, walemavu na waathirika wa UKIMWI ambayo imesaidia jumla ya watu 2,862; kutekeleza miradi 305 ya Ujenzi; kutoa ajira ya muda kwa walengwa 113,646 kupitia miradi ya Jamii na Kushirikisha Taasisi 47 zisizo za Kiserikali na kijamii katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya Makundi Maalum.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha uliopita Kamati ilitoa maagizo mawili. Maagizo haya yalihusu Wizara (Ofisi ya Rais) kutekeleza malengo yake kulingana na Bajeti iliyotengwa. Agizo hili limezingatiwa ipasavyo na Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na ziara za Kamati katika Sekta/Taasisi zinazohusiana na Wizara zilizoko chini ya Kamati zipewe umuhimu unaostahili kwani huziwezesha Kamati kufahamu kwa vitendo hali iliyoko katika Sekta au Taasisi hizo. Agizo hili nalo limezingatiwa kikamilifu. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Idara/Taasisi za Ofisi ya Rais na Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu, Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa kwa mwaka wa Fedha wa 2005/2006, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: Kukamilisha usimikaji wa mifumo ya utendaji kazi katika mikoa;

kushirikiana na Wizara ambazo tayari zimeanzisha Mfumo wa Utendaji Kazi *(PMS)* kwa lengo la kufuatilia utekelezaji na uimarishaji wa mfumo huo; kuendelea kubadilisha Idara nne za Serikali kuwa Wakala pamoja na kuendelea kuimarisha wakala ambazo tayari zimezinduliwa; kazi nyingine ni kuendelea na mipango ya kushirikisha sekta binafsi katika utoaji huduma katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Hospitali za Rufaa na mikoa; kuanzisha Mfumo wa Kutunza Kumbukumbu Tuli *(Records Management Systems)* katika Wizara na Idara zinazojitegemea na kujenga Kituo cha Menejimenti ya Mtandao *(Network Management Centre)* kwa ajili ya kusimika vifaa mbalimbali vya Serikali na kadhalika..

Kazi zilizopangwa kufanywa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni pamoja na kuchunguza malalamiko kutoka kwa Wananchi dhidi ya viongozi mbalimbali wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya uongozi; kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma kwa mujibu wa sheria; kutoa elimu ya maadili ya uongozi wa umma na viongozi kwa njia ya redio, semina na machapisho mbalimbali; kuajiri watumishi wapya, kununua vitendea kazi na samani kwa ajili ya ofisi za Kanda za Tabora, Mtwara na Mwanza na kuwapatia watumishi wa Sekretarieti mafunzo ili kuboresha utendaji wao wa kazi. Aidha, katika kipindi hiki cha mwaka 2005/2006, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: Kushughulikia rufaa za watumishi, waajiri na mamlaka za nidhamu; kuwaelimisha watumishi na wadau kuhusu majukumu ya Tume ya Watumishi wa Umma; kutoa miongozo mipya kuhusu masuala mbalimbali ya Utumishi wa Umma na kuandaa mafunzo kwa watumishi wa Tume ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2005/2006, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeiomba Kamati yangu iidhinishie jumla ya Sh. 55,165,036,800/=, kati ya hizo Sh. 6,225,036,800/= zikiwa ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo na Sh. 48,940,000,000/= za Miradi ya Maendeleo. Aidha, jumla ya Sh. 1,161,680,400/= zinaombwa kwa ajili ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kati ya hizo Sh. 141,680.400/= kwa ajili ya mishahara na Sh.1.020,000,000/= kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Pia Sh. 4,883,000,000/= zinaombwa kwa ajili ya Tume ya Utumishi wa Umma, kati ya hizo Sh. 1,593,255,000/= kwa ajili ya mishahara na Sh. 115,000,000/= kwa ajili ya matumizi mengine. Kamati inapendekeza kuwa maombi haya yakubaliwe na kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Kamati ilipokea taarifa kuwa Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu uendeshaji wa shughuli za Serikali; kusimamia utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na Rais pamoja na Baraza la Mawaziri; kuendesha mafunzo ya watumishi na shughuli za uendeshaji wa ofisi na kuendelea na ukarabati wa Ikulu, kusimamia Mradi wa *TASAF* na Programu ya Kurasimisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge Tanzania, ambao umebuniwa na Serikali kama sehemu ya MKUKUTA.

Aidha, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea na uchunguzi wa majalada 3,643 na mengine yatakayofunguliwa kutokana na malalamiko yatakayopokelewa na kukamilisha majalada yanayohusu

uchunguzi maalumu wa mapunjo ya mishahara hasa ya walimu yanayoshukiwa kufanywa na baadhi ya watumishi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wa Wizara ya Elimu. Pia kuendelea na uchunguzi wa matumizi mabaya ya fedha za MMEM; kuendesha kesi 188 zilizopo mahakamani pamoja na zitakazofunguliwa kwa mwaka wa fedha 2005/2006 na kuendelea kufuatilia kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2005 ili kubaini vitendo vya rushwa katika shughuli za kampeni na kadhalika.

Kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* kazi zilizopangwa ni kuendelea na Awamu ya Pili ya *TASAF* kwa kuziwezesha jamii kupata na kuzitumia rasilimali za kijamii na kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yao; kujenga uwezo wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Kijamii, taasisi za kuweka fedha za kijamii, wasimamizi wa miradi na Wananchi kwa ujumla, kusimamia maendeleo na kuboresha mahusiano yao na wadau wengine katika maendeleo; kutoa ajira za muda kwa kaya maskini na wakati huo huo kuboresha huduma za jamii; kuboresha maisha ya makundi maalum na wasiojiweza na kuwezesha jamii kupata mikopo, kuboresha uwekaji wa akiba na mitaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa Fedha, Ofisi ya Rais, Ikulu imeiomba Kamati yangu iidhinishie jumla ya Sh. 4,909,472,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 78,933,436,600/= kwa ajili ya Ofisi ya Rais, pamoja na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa Matumizi ya Kawaida na Sh. 58,097,143,000/= kwa Miradi ya Maendeleo, fedha ambazo Kamati inapendekeza Bunge liidhinishe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Kamati yangu haikuwa na maagizo yoyote kwa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora). Hata hivyo, Kamati ilikuwa na maoni na ushauri katika maeneo kadhaa yanayohusu Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wetu kwa sehemu kubwa yalipata ufafanuzi wa kina kutoka Serikalini. Hata hivyo, kwa faida ya Bunge lako, niruhusu nitaje maeneo machache. Kwanza, ni kuhusu suala zima la mfumo mpya wa mageuzi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali, Kamati yangu imebaini kuwa utaratibu mpya wa kuhuisha vyeo na mishahara ya watumishi unalalamikiwa sana na baadhi ya watumishi waandamizi kwamba, hauwatendei haki hasa katika kupandishwa vyeo. Hivi sasa baadhi yao wamejikuta ama wanalingana na watumishi walioajiriwa karibuni au wamepitana kwa ngazi moja ya mshahara. Kwa maneno mengine utaratibu huu unaonekana kuwanufaisha sana watumishi wenye stashahada za juu au shahada walioajiriwa hivi karibuni na kutowanufaisha watumishi wa miaka mingi wenye sifa hizo. Pamoja na jitihada zinazofanyika, Kamati bado inasisitiza kuwa ni vema kero hii itatuliwe mapema, vinginevyo zoezi zima la kuleta mageuzi katika utumishi litaingia dosari.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine na ambao ulipatiwa ufafanuzi ni kuitaka Serikali isimamie na ifuatilie haraka suala zima la ajira hasa kwa walimu wanaofariki,

ambao mara nyingi nafasi zao huchelewa kuzibwa na kusababisha uhaba mkubwa wa watumishi hao katika maeneo mengi hapa nchini. Sambamba na hili ni kuishauri Serikali iweke mkakati madhubuti kuhakikisha kuwa watumishi wanakwenda kufanya kazi katika mikoa yenye mazingira magumu kiutumishi kama vile Mtwara, Lindi, Rukwa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, haya ndiyo mambo ya msingi ambayo yalijitokeza kwa muhtasari wakati Kamati yangu ilipopata fursa ya kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora). Endapo yapo maeneo ambayo sikuyazungumzia, bila shaka Wajumbe wa Kamati yangu watayazungumzia watakapopata nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii adhimu. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi na wataalamu wake wote, kwa maelezo yake ya kina mbele ya Kamati. Vilevile, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa ushirikiano mkubwa alioutoa katika Kamati yetu kwa kipindi chote Kamati hii ilipokuwa ikifanya kazi katika Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja nao ninaomba kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara na Wabunge wote kwa ushirikiano walioipa Kamati hii kila mara Kamati ilipoleta hoja kuhusu Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda nichukue fursa hii niwashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa kufanya uchambuzi wao wa kina ulioiwezesha hoja hii kufikia hatua iliyopo sasa. Wajumbe wa Kamati walioifanya kazi hii ni Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Zahoro Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Juma S. N'hunga, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah S. Fundikira, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, napenda niwashukuru, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Athumani Hussein, Makatibu wa Kamati hii, chini ya uongozi wa Bwana Damian Foka, Katibu wa Bunge, kwa kuihudumia vema Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, naomba pia nichukue nafasi hii niwashukuru sana kwa ushirikiano wao walionipa kwa kipindi hiki cha miaka mitano na ninaomba kushirikiana nao katika Uchaguzi ujao Mwenyezi Mungu akipenda.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwatakie pia Wabunge wengine wote Uchaguzi mwema na wenye kuwarudisha tena hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, niwataje wale waliokwishajiandikisha kuchangia hoja hii ili wawepo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Frank Maghoba. Naomba wawepo kwenye ukumbi ili wasikose nafasi zao. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye sekta hii ya Utawala, Mheshimiwa Grace Kiwelu, atoe maoni ya Kambi ya Upinzani.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ningependa kutoa shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii, nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5), (b) na (c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nitoe pole na salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, aliyetutoka kabla ya Mkutano huu kuanza na familia ya Marehemu Mheshimiwa Margareth James Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM. Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu. Vyama mbalimbali vya siasa vimeshawapitisha wagombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia vyama vyao. Kwa ajili hii ningependa niwapongeze wote walioteuliwa na watakaoendelea kuteuliwa na vyama vyao kugombea nafasi hizo za juu za uongozi.

Ningeomba kumpongezaWaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Katibu Mkuu, pamoja na Wakuu wa Vitengo na asasi zilizowekwa chini yake kwa kazi nzuri ya kuratibu na kusimamia mchakato mzima wa Bajeti hii ambayo imesomwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia neema zake hadi leo hii tunapokutana katika Mkutano wetu wa mwisho. Mwenyezi Mungu, awajalie wale wote waliofanya kazi zao kwa ufanisi kwenye Majimbo yao ili tuweze kukutana tena katika kipindi kipya cha 2005 - 2010 tukiwa na Serikali itakayoongozwa na upinzani.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kukushukuru wewe binafsi na watendaji wote wa ofisi yako, kwa ushirikiano uliotupatia kwa kipindi chote tangu mwaka 2000 hadi Bunge hili la mwisho kabla ya uchaguzi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano waliotupa sisi Kambi ya Upinzani kwa kipindi chote cha miaka takribani mitano tukiwa hapa Bungeni, niwatakie safari njema pindi watakaporudi majimboni kwao na kama watafanikiwa kupewa ridhaa na Wananchi basi tukutane tena Bungeni tukiwa watiifu chini ya Serikali mpya inayoongozwa na sisi Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa Uchaguzi na kutokana na uwajibikaji wa baadhi ya Viongozi na Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali kuwa mbovu, wamejikuta wanajisahau na kusahau hata nyadhifa zao walizokabidhiwa na umma kwa kufanya kazi zao kwa maslahi ya Chama Tawala badala ya kutanguliza maslahi ya umma. Mifano ni mingi sana ila ningependa kukumbusha japo mfano uliotokea hivi karibuni kwa baadhi ya taasisi za umma kutumia fedha za umma kulipa mamilioni ya shilingi kwa ajili ya matangazo ya mteuliwa wa Chama cha Mapinduzi. Huu sio utendaji mzuri hata kidogo na inaonesha jinsi watumishi wa umma wanavyoendesha mashirika ya umma kwa maslahi ya Chama Tawala. Mbaya zaidi ni pale viongozi wa juu wa Serikali wanapojitokeza na kutetea hali hiyo. Tunaipongeza Tume ya Uchaguzi ya Taifa kwa kulitolea msimamo suala hilo na bila shaka wamejifunza na kuona aibu na ndio maana matangazo hayo hayaonekani tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa kada ya chini na kati wamekuwa wakati mwingine wakikopwa na Serikali mishahara yao au mafao yao mengine, kwa mfano, walimu, wauguzi, wapiganaji, askari na kadhalika, wengi hawalipwi haki zao za kwenda uhamishoni ama likizo. Haijawahi kutokea hata siku moja mtumishi au kiongozi wa ngazi ya juu kucheleweshewa kupata mshahara wake au kupelekwa kwenye matibabu, marupurupu au posho yake wakati wote wa utumishi wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ikipewa ridhaa na Wananchi katika kuongoza itakuwa ni kosa kubwa lisilovumilika kwa Serikali kuwakosesha watumishi haki zao zote na hasa wa ngazi za chini na kati ambao wanaonewa kwa sasa na Serikali. Mfumo wetu utakuwa ni wa chini kwanza na wa juu baadaye. Kima cha chini cha sasa ni dharau kubwa kwa wafanyakazi, hii pia inamfanya mfanyakazi wakati wa kustaafu kwake pensheni yake inakuwa ndogo mno wakati muda huo atakuwa anahitaji sana pesa kwa ajili ya kujikimu kulingana na umri wake. Kambi ya Upinzani tuchukuapo Serikali Oktoba 30, 2005, maslahi yote anayopaswa kulipwa mtumishi yatawekwa kwenye mshahara wake na kada zote zitashughulikiwa ipasavyo. Hii itamuwezesha mtumishi kupata pensheni nzuri wakati wa kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa watumishi wa Serikali wanaongoza kwa kulipa kodi kubwa sana Serikalini wakati kipato chao ni kidogo sana ukilinganisha na wafanyabiashara wakubwa na hata wa kati ambao kipato chao ni kikubwa. Kambi ya Upinzani tunasema tukipewa ridhaa na Wananchi tutawapunguzia kodi watumishi wote

wa Serikali na mashirika binafsi ili walipe kutokana na vipato vyao halisi na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunasema Wananchi wakitupa ridhaa ya kuwaongoza tutawapunguzia mzigo mzito wa kodi ambao kwa sasa wametwishwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa mfano, Mtumishi wa Serikali ambaye mshahara wake ni mdogo anakatwa kodi kwenye huo mshahara mdogo na wakati huo huo kodi nyingine anaendelea kuzilipa wakati wa kununua bidhaa mbalimbali kama vyakula, nguo na mahitaji mengineyo. Kwa wingi wa kodi hizi mwananchi wa kipato cha chini hataweza kujikwamua kwenye wimbi la umaskini kwani atajikuta kwa kile kidogo anachopata anakitumia kulipa kodi badala ya kujiendeleza yeye na familia yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na jinsi ambavyo Serikali inachelewesha kuwapandisha watumishi wake madaraja, kwani uzoefu unaonesha kuwa, watumishi wengi wa Serikali na hasa kwenye Idara ya Elimu, wanachukua muda mrefu sana bila ya kupandishwa vyeo. Inasikitisha zaidi pale ambapo Serikali inawanyima walimu na watumishi wengine, nafasi za kujiendeleza kimasomo na mfano mzuri ni mwaka huu ambapo kati ya walimu wote walioomba nafasi za masomo ya juu, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Kitivo cha Elimu ni mwalimu mmoja tu ndiye aliyepata nafasi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inajiuliza Serikali inampango gani na walimu hawa kwani kila siku shule zetu zinalalamika kuwa na ukosefu wa walimu au pia wale wachache waliopo hawapewi nafasi za kujiendeleza ili waweze kupanda madaraja.

Lipo tatizo la kuwatenga, kuwabagua na hata kuweka tofauti kubwa ya kimapato na kimaslahi miongoni mwa watumishi wa Serikali japo wote ni watoto wa baba mmoja na mama mmoja na wanahemea kwenye soko moja. Hii ni hatari kubwa huko mbele tunakokwenda, tunatengeneza matabaka ya kiutumishi ndani ya Serikali moja. Kwa mfano, inasikitisha kuona kuwa watumishi wa Redio Tanzania, pamoja na kuwa chini ya chombo kimoja na wenzao wa Televisheni ya Taifa, yaani Taasisi ya Utangazaji Tanzania, bado mwelekeo wao wa kiutumishi haufanani, haueleweki na unaelea hewani. Maslahi yao kiutumishi yanapishana mno baina yao. Hali hii ambayo inajitokeza katika taasisi nyingi za Serikali inachangia kuzorota kwa ufanisi wa kazi na kuwanyima ari na moyo wa kutenda kazi kwa nguvu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Idara ya Jeshi la Polisi, mambo ni hayo hayo, hawapandishwi vyeo kwa muda muafaka. Sisi Kambi ya Upinzani tunasema pindi tutakapoingia madarakani, watumishi wote wa Serikali wanaostahili kupandishwa vyeo, Serikali yetu itafanya hivyo ili tuweze kuwapa moyo na ari ya kulitumikia Taifa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara na marupurupu ya madaktari si jambo la kungojea kushauriwa na wataalam mbali mbali, bali ni suala la kuona umuhimu wa kazi waitendayo kwa jamii. Madaktari wetu wamekuwa wakihamia nchi za wenzetu kwa kufuata maslahi yalinganayo na kazi waifanyayo kwa jamii na jinsi wanavyothaminiwa na nchi zao. Mfano mdogo, Mzee wetu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa,

amepelekwa Afrika Kusini kwa matibabu, lakini kuna uwezekano mkubwa daktari anayemtibu huko ni Mtanzania mwenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama inavyoeleweka, Wizara ya Afya ndio mlezi wa madaktari, hivyo basi, malalamiko yao kuhusiana na mishahara sio jambo lililojitokeza jana au juzi bali ni suala la siku nyingi. Tunaamini kabisa kuwa, madaktari hao kupitia Wizara yao, walikwishapeleka maombi yao Utumishi. Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri awaeleze Watanzania kama maombi yao yalikwisha wasilishwa kwake au bado na kama ndivyo ni kwa nini maombi yao yamechelewa kushughulikiwa mpaka Serikali ikaingia aibu na watu kufa na wengine kupata mateso kutokana na kukosa huduma wakati wa mgomo.

Mheshimiwa Spika, hebu tuwe wakweli kuhusu mambo muhimu, posho anayopewa Mheshimiwa Mbunge kwa siku tatu ni sawa na mshahara wa daktari kwa mwezi mzima, licha ya kushinda na kuhitajika usiku kucha kuwatibu wagonjwa. Hii inasababisha wasomi na mabingwa katika fani mbalimbali, kuziacha fani zao na kukimbilia nchi za nje au kufanya shughuli tofauti na fani zao. Kambi ya Upinzani inawaahidi wataalamu mbalimbali kuwa, itakapopata ridhaa ya Watanzania, itarejesha heshima ya taaluma mbalimbali katika nchi hii. Hivyo, kura zenu tupeni kwenye uchaguzi wa Oktoba 30, 2005, vinginevyo mtaendelea kujinyonga kwa kura zenu hizo hizo na mtaendelea na malalamiko chungu nzima mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa zisizo rasmi ambazo Kambi ya Upinzani inazo kuhusu zoezi la kumtafuta na kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Muhimbili kuwa, limeigharimu Serikali shilingi milioni 100. Kitu ambacho tunaona si haki kwa Watanzania, kwani ni Watanzania wangapi wamehitimu hapa kwenye vyuo vyetu na wengine nje ya nchi katika fani hiyo ya utawala na wana uwezo mkubwa wa utendaji na ubunifu?

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, tunaiomba Serikali itoe taarifa rasmi kuhusu suala hilo kwa manufaa ya Watanzania wote na iwaeleze Watanzania kama hiyo ndiyo njia sahihi ya matumizi ya fedha ya walipa kodi. Hivi sasa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, inajitahidi kuhuisha mfumo na muundo wa utumishi katika Sekta nzima ya Serikali. Hii ni pamoja na kuweka utaratibu na mvuto kwa kuwa na watumishi wa Serikali waliosoma. Tunalipongeza jambo hili kwani ndio njia pekee ya kuwa na Serikali inayokwenda na wakati. Hata hivyo, tunashauri jambo hili lifanyike kwa umakini mkubwa ili lisilete vurugu na kero kwa watumishi ambao wamelitumikia Taifa hili kwa muda mrefu, kwa uaminifu na kwa utii wa hali ya juu, pamoja na elimu yao ya darasa la saba. *(Makofi)*

Zoezi hili lizingatie hali halisi na lisiwatelekeze au kuwalazimisha watumishi hao kufanya lile ambalo kutokana na hali zinazowazunguka sasa wasiweze kukidhi matakwa yaliyotarajiwa au yanayotakiwa. Kwa mfano, haitarajiwi dreva wa Bunge ambaye hakufika Kidato cha Nne, mwenye umri wa miaka hamsini au zaidi, mwenye wajukuu nyumbani na familia kubwa, umtake leo akasome na kufaulu ili apate cheti cha Kidato cha Nne kwa miaka miwili ili aweze kuendelea na kazi ya udreva hapa Bungeni.

Kumwachisha kazi wakati umebakia muda mfupi astaafu, Serikali itakuwa inafanya kufuru. Ni bora watumishi kama hawa ambao kimsingi inatulazimu kuwaenzi, waondolewe kazini taratibu, kwa umri wao wa kustaafu na hao wanaoingia katika ajira mpya na wenye umri unaoweza kumudu mchakato huo, wafuate utaratibu huo mpya. Serikali ya CCM kama haiko tayari kulifanya hilo, watumishi wa Serikali chagueni na kuufagilia upinzani Oktoba 30, 2005 ili tuwanusuru na *tsunami* hilo mnaloletewa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki Kambi ya Upinzani imeshuhudia pamoja na Wananchi kwa ujumla, ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaofanywa na vyombo vya dola. Tumeshuhudia jinsi ambavyo raia wa nchi hii wamekuwa wakiuwawa bila hatia yoyote na wala sheria kuchukuliwa dhidi ya wale wote ambao wamehusika katika kutenda makosa hayo na mfano mzuri ni wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa pale mwanafunzi alipouwawa na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa hadi leo. Aidha, tumeshuhudia wakati wa uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura huko Zanzibar, Wananchi walivyoumizwa hasa Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunasisitiza tena na tena juu ya suala la haki ya raia ya kuchagua na kuchaguliwa. Inapokuwa hii ni haki ya msingi kabisa kwa raia wetu lakini bado Katiba yetu inamapungufu makubwa kwani inamnyima raia haki yake ya kuchaguliwa hasa pale ambapo raia huyo hana chama cha siasa, lakini wakati huo huo raia huyo analazimishwa kuchagua miongoni mwa vyama vya siasa hata kama hakubaliani na sera, pamoja na falsafa za vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni haki ya msingi kabisa kwa raia kuchaguliwa na kuchagua kiongozi ambaye anaamini anafaa kuongoza. Hivyo basi, kipengele cha kumnyima haki ya kuchaguliwa ni kukiuka misingi ya haki za binadamu, ndio maana Wapinzani tunasema tukichukua nchi Oktoba 30, 2005, Katiba lazima iandikwe upya.

Mheshimiwa Spika, kuchaguliwa ni haki ya msingi kabisa kwa raia wa Tanzania. Kambi ya Upinzani tunasikitishwa sana na Sheria za Nchi hii zinazopitishwa ndani ya Bunge hili za kuwanyima watu haki ya kuchaguliwa kuwa viongozi na kubwa ambalo linaathiri sana ni Sheria ya Takrima. Kambi ya Upinzani tunasema takrima ni rushwa na pindi tutakapoingia madarakani tutaifuta sheria hii mara moja. Katika hili tunawapongeza baadhi ya watendaji katika vyombo vya Polisi, *PCB,* Mahakama, taasisi za dini na kadhalika, ambao bila woga, wamekuwa wakieleza bayana kuwa takrima ni rushwa. *(Makofi)*

Mheshiwa Spika, ningependa kurudia tena ya kuwa, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ifute takrima kabla ya uchaguzi wa mwaka huu ili raia wote bila kujali uwezo wao wa kifedha, wapate uwanja sawa wa kisiasa ili waweze kushindana kwa haki na usawa kupata fursa ya kukamata nafasi za uongozi. Ni aibu ugonjwa wa takrima, ambao CCM wenyewe wanauogopa na wameupiga vita katika kanuni na taratibu zao za uchaguzi ndani ya chama, ugonjwa huo huo unasambazwa wakati wa uchaguzi wa jumla kwa kutungia sheria na kuipitisha kwa kishindo humu Bungeni! Huu ni ugonjwa wa kiroho kama walivyosema viongozi wetu wa kidini, ambao wote tunawaheshimu.

Mbona tunapenda kuifanya mioyo yetu kuwa migumu? Kambi ya Upinzani tunazidi kusisitiza kuwa takrima ni rushwa na rushwa ni dhambi na dhambi ni mauti, mauti ni jehanamu na jehenamu ni moto, je hamwogopi moto wa milele? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Serikali, pamoja na asasi binafsi, kwa hivi sasa ndio waathirika wakuu wa gonjwa hili hatari la UKIMWI. Takwimu zinaonesha ya kuwa, walimu ndio kundi kubwa katika watumishi wa Serikali walioathirika zaidi. Kambi ya Upinzani inapenda kuishauri Serikali kupitia kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi ya kuwa, sasa ni muda muafaka wakuandaa mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kuepuka kuambukizwa Virusi vya UKIMWI na hii itafanya watumishi wengi wa Serikali kuweza kijifunza mbinu hizo badala ya Serikali kuachia jukumu hili kufanywa na mashirika binafsi ama dini peke yake.

Mheshiwa Spika, mara nyingine watumishi wa Serikali wanaopata fursa za kuhudhuria semina juu ya UKIMWI ni wale ambao wengi wao wako mjini wakati wahanga wakuu ni wale walioko vijijini, ambao hawapatiwi fursa hiyo wala kupewa mbinu au zana mbalimbali za kuepuka kupata virusi vya UKIMWI. Kambi ya Upinzani tunasema sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuhamishia nguvu zake vijijini zaidi badala ya kuishia mjini ambapo mwamko ni mkubwa kwa sasa kwani tayari wanapata mafunzo na taarifa kupitia njia mabalimbali za habari.

Dhana ya Utawala Bora ni pana sana na haiwezekani Serikali kuzungumzia dhana ya Utawala Bora kwa nadharia tu. Pia haiwezekani dhana ya Utawala Bora kueleweka kwa Wananchi, pamoja na watumishi wa Serikali, kama Serikali hiyo haifanyi jitihada zozote kuhakikisha kuwa watumishi wake, pamoja na Wananchi kwa ujumla, wanapata fursa ya kufundishwa elimu ya uraia, ambayo ndio kiini kizima cha dhana ya Utawala Bora. Kambi ya Upinzani tunasema pindi tutakapoingia madarakani na kuongoza dola, tutatenga fungu la kutosha katika Bajeti yetu ili kuwafundisha watumishi pamoja na Wananchi dhana ya Utawala Bora.

Aidha, kwa kutambua wazi kuwa Utawala Bora ni ule unaoendeshwa na kusimamiwa na Katiba, Sheria na Kanuni, Serikali mpya ya Upinzani, itahakikisha inachukua hatua za makusudi za kutafsiri sheria zote katika Lugha ya Kishwahili, kuweka taratibu za elimu ya uraia au upashanaji mzuri wa habari na taarifa kupitia kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji, ili umma usiongozwe kimbumbumbu. Wajue wanapaswa kuwajibika katika maeneo gani na mambo gani na Serikali nayo inapaswa kufanya nini au kuwajibika katika mambo yapi. Hii itawaongezea raia uelewa wa wajibu wao na haki zao na hivyo kuzidai kwa lazima na wao pia kuwajibika.

Mheshimiwa Spika, ni vyema nchi yetu imeweka utaratibu wa kuwahudumia Viongozi Wakuu wa nchi wanaofikia kipindi cha kuacha madaraka. Kutokana na taratibu zetu zilivyo ni wazi katika kipindi kifupi tunaweza kujikuta tuna orodha ndefu ambayo inatulazimu kuihudumia. Pamoja na nia njema iliyopo ya kuwapenda viongozi wetu lakini ni vyema Serikali ingeanza kuangalia utaratibu mpya ambao ni rahisi kuusimamia na kuutekeleza kabla mambo hayajatuelemea huko mbele. Ingekuwa bora kumfungashia Kiongozi *package* yake kama inavyofanyika huko Marekani na tukamaliza

biashara ili awe huru kupanga na kufanya mambo yake. Serikali ibakie na majukumu mengine machache kama ya kiusalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi ambayo yameendelea kufanyika katika Taifa letu ambapo Sekta binafsi inaendelea kushika kazi na kuwa mhimili mkubwa wa kutoa ajira, ni vyema Serikali ikaweka utaratibu makini na wenye nguvu za kimaamuzi za kusimamia ajira katika sekta binafsi zitakazohakikisha waajiriwa wote wanatendewa haki. Tukiacha mambo yajiendeshe hivyo hivyo au kutegemea waajiriwa wajitetee kupitia vyama vyao vya kazi, tuna uhakika wengi watapoteza vibarua vyao na wengine wataendelea kumtumikia kafiri ili mradi wapate hicho wanachokipata. Katika hali hiyo, tutakuwa tunawauza Watanzania katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, sio siri hivi sasa kutokana na tatizo la ajira, Watanzania wanafanyiwa vituko katika vyanzo mbalimbali vya binafsi wanavyobahatika kupata ajira.Wengi wanafanyishwa kazi za ajabu, mishahara mibovu, saa za kufanya kazi hazieleweki. Ni lazima tuyalinde maslahi ya Watanzania katika hali yoyote ile. Tusiachie utandawazi uwameze jumla Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimewasilisha mambo yote hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda nitumie fursa hii, nimshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare,kwa kuniamini kipindi chote cha miaka mitatu na nusu na kunikabidhi jukumu la kuisimamia Wizara hii nyeti. Aidha, tuwaeleweshe baadhi ya Wabunge wenzetu wa CCM, ambao huenda hawana taarifa kuwa mara zote hotuba za Mawaziri tumekuwa tukikutana nazo humu humu ndani ya Bunge, lakini pamoja na hali hiyo, tumekuwa tukiwasilisha maoni na matakwa ya umma mkubwa ulioko nje ya Bunge hili.

Nikiwa Bungeni nimejifunza mambo mengi mno hususan namna umma wa milioni 37 unavyomalizwa au kunusuriwa na maamuzi mazuri au mabaya ya watu 295 na hayo yote yasingeliwezekana endapo Chama changu cha CHADEMA, kisingeniteua kukiwakilisha katika nafasi ya Ubunge wa Viti Maalum. Ninawashukuru sana Wanachama, Viongozi wangu wa Chama na Wananchi kwa ujumla, ambao mmeendelea kuunga mkono Upinzani kwa kutupigia kura. *(Makofi)*

Nawashukuru Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani kwa msaada ambao mmekuwa mkinipa na nawaomba tuzidishe kusimamia vyema mikakati ya kiushindi itakayotuwezesha kuikamata dola na kurejea hapa Dodoma Novemba, 2005, tukisubiri kuteuliwa kama Mawaziri kamili. Wito wangu mkubwa ni kwa watumishi wote nchini, tuungeni mkono japo kimya kimya sisi Wapinzani tukamate madaraka ya dola, ili tuwarejeshee ari na moyo wa kulitumikia Taifa. *(Makofi)*

Kwa kuwa msingi mkuu wa Utawala Bora na utumishi uliotukuka na wenye tija ni ule unaopatikana baada ya kuwapata viongozi shupavu na mahiri waliochaguliwa na Wananchi kwa ridhaa yao ndani ya uchaguzi ulio huru na haki, ni vyema Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu Mtarajiwa, akatamka bayana na kwa uwazi

kwamba, pamoja na vyombo vya dola kuhakikisha vinasimamia amani, utulivu na vitendo vya fujo wakati wa uchaguzi, lakini pia Serikali iliyoko madarakani na vyombo vyake vyote vya dola, vitakuwa tayari katika njia za kistaarabu, kukubali matokeo na kukabidhi madaraka endapo Upinzani utashinda uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, sasa tunaingia kwenye mjadala wa jumla namwita Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia huu mjadala wa Utawala Bora na Utumishi. Kwanza, ningeomba nitoe rambirambi zangu kwa kifo kilichompata Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, ambaye tulishirikiana sana katika kazi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, *speech* ya Waziri ni nzuri sana, nianze kuisifia sio mbaya na sina sababu ya kuikosoa na sikupata hata huo muda wa kuisoma vizuri ili niweze kutoa makosa kama yapo. Lakini nitazungumzia kwa ujumla maana ya Utawala wa Bora na matatizo tuliyonayo katika nchi yetu kwa ujumla, ambayo ningeomba Waziri ayachukue na ayafanyie kazi. Kwanza, nitaanza na Wakurugenzi. Natoa mfano halisi ambao umetokea kule Moshi kwenye jimbo langu la uchaguzi. Kuna Kata moja inaitwa Kiboriloni, ambayo kwa bahati nzuri Ikulu iko katika Mtaa wa *KDC,* Kata ya Kiboriloni, imemtia Mkurugenzi matatizo makubwa kwa sababu Kata ile nimeichukua kwa sababu na mimi nakaa katika Kata ile na Mtaa ule.

Amekwenda Mahakamani na amekiuka Sheria, kati ya walioandikishwa kupiga kura katika Kata ile amewafuta wapiga kura 153 na kusema hawa hawapo mjini wako Moshi Vijijini na akatoa ramani yake aliyoipeleka ambayo mimi niliiona ni feki, hii iko hapa. Lakini chini ya *Government Notice No. 294, published on 1954,* inatoa mipaka na kuonesha *beacons* zinazohusu ile Kata mipaka yake ikoje. Baada ya kwenda kumwonesha na kumwelimisha kuwa haya anayofanya sio Utawala Bora, akasema sasa wote wale nawarudisha na kisa kilikuwa wamekwenda mahakamani ili wawafute na ile Kata irudi CCM. Katika Utawala Bora kijiji kinacho tawaliwa na wapinzani, Ikulu ile iko chini ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Diwani wa CHADEMA, Mbunge wa CHADEMA, lakini Rais akija hatualikwi, wakati sisi ndiyo tunatakiwa tumpokee, hii inaonyesha jinsi utawala mbovu unavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, a-*make note of that,* sisi ndiyo watawala katika eneo lile ni lazima Rais anapokuja au yeyote, tunatakiwa tumpokee, sio Viongozi wa CCM, kwa sababu ile ni Serikali yetu. Katika Kata hiyo hiyo, kwa kuwa Mama Anna Mkapa, anatoka kijiji cha jirani, wapigakura wote wa Kata ya Kiboriloni walilazimishwa kwenda kupiga kura kwenye Kijiji cha Mama Mkapa ili ashinde. Uchaguzi uliahirishwa mara nne ili waweze tu kuchukua kwa nguvu. Hivi leo ninaposema hapa, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kikarara ni mkazi wa Kiboriloni na hii ni *agaist the law.* Mheshimwa Waziri, naomba ulichukue hilo na uka-*check* ujue kwa uwazi

ya kuwa yule anakaa Kiboriloni na hana haki ya kuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Kikarara. Huo si Utawala Bora. Sisi Tanzania tunasifiwa sana na tunapata misaada mingi nje kwa sababu tunatumia utaratibu mzuri wa Utawala Bora na tumekuwa ni watu tunaaminika. Serikali ya Tanzania ina heshima kubwa katika dunia hii, lakini mimi nina wasi wasi huenda tunataka kugeuka na tutapata matatizo. Tunakwenda katika ushirika wa *East Africa,* nchi moja ya Uganda, haitaki demokrasia wala uchaguzi wa Rais, Rais anataka kuwa wa maisha. Tunaungana vipi na nchi yenye viongozi wa namna hii? *(Makofi)*

Matatizo yaliyoko Zimbabwe yanahamia Uganda na yatatuathiri sisi na *credibility* yetu Watanzania itakuwa *tarnished.* Kwa hiyo, wakati tukifikiria Muungano wetu wa *East Africa,* tuwe makini na tujue tunafanya nini. Ni heri tukaendelea wenyewe kwa sababu tuna *credibility* na tunapata misaada. Si uongo hata *Europe* sasa inaanza kubadilika na kurudi badala ya kuwa pamoja wanakwenda moja moja.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu chenye heshima katika Utawala Bora kama kuheshimiana, ni jambo la msingi. Wakati unapofika, ninawazungumzia *the learned friends* anapoanza kumsaliti mwenzake hadharani, tulimsikia *Attorney General* alivyomdhalilisha Jaji Kissanga. Hii ni aibu, siyo Utawala Bora. Tulimsikia Waziri alivyokuwa anamzungumzia *Registrar,* Bwana Tendwa, anaambiwa ni Karani. Huyu ni Jaji mwenye heshima dunia nzima. *They are learned friends* na ndivyo wanavyojiita. Huwezi kumtukana mwenzako. *(Makofi)*

Kama tukianza kufanya hivyo, kesho kutwa hata Spika wetu tunayemheshimu tutamwita ni *MC.* Ni lazima tulinde heshima ya viongozi, tusitanie haya ni mambo ya Utawala Bora tunazungumzia hapa. Tukifika kiwango cha kuanza kumwita Spika wetu ni *MC* tutakuwa tumekosa adabu wote sisi Wabunge wa Bunge hili. Sasa tumemfanya Tendwa ni Karani, Jaji Kissanga tumemwita hana maana pamoja na *experience* yake ya miaka mingi, kwani ni ajabu gani kumwita Spika, *MC!* Tutafika hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge tulitakiwa tuwe wa kwanza wa kutoa mfano wa Utawala Bora kwa kufuata maadili na Kanuni za Nyumba yetu. Kanuni za hapa kwenye Bunge hili Tukufu, tunasema mtu akishazungumza jambo fulani si vizuri wengine wakalirudia. Tunaweka matatizo hapa ya kurudia kila kiongozi anayesimama, Kikwete, Kikwete Kikwete. Sasa akishasema mmoja si imetosha! Sasa siyo tunavunja Kanuni zetu ambapo tunatakiwa tuwe ndiyo tunaoongoza kuonesha wengine Utawala Bora maana yake nini. Kama sisi tunaanza kuvunja kwa kusema Kikwete, Kikwete, kila dakika, nadhani huo siyo Utwala Bora. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza sana juu ya uuzaji wa nyumba za Serikali ambazo hazikufuata utaratibu. Naomba vilevile niligusie kidogo. Kuna watu wanalalamika wamefukuzwa kwenye nyumba, wanapewa Mabalozi wako nje. Lakini Sheria inasema anayekaa kule ndani ndiye auziwe ile nyumba. Mtu anakuja kufukuzwa na Askari anatolewa kwenye nyumba eti ni ya fulani kwa kuwa ni Balozi yuko Marekani, yuko China, yuko wapi! Anaambiwa nyumba iko Dar es Salaam ni yako. Jamani huo ndiyo Utawala Bora? Sisi CHADEMA tunasema na tunaliambia Bunge lako na naomba

iingie kwenye *record.* Siku ikitokea hata kama ni miaka mia moja kuanzia sasa zile nyumba tutazitaifisha na tutazirudisha kwa Serikali. Tutazitaifisha na tutazirudisha kwa Serikali. Hilo nasema na nina imani hiyo, maana mabadiliko ni lazima na ni lazima patatokea Serikali ambayo itaona haya yalikuwa ni maamuzi mabaya, kwa hiyo, waliopewa nyumba wakae chonjo. Hata kama zitakuwa mtu kaziuza, kiwanja tunajua ni chetu, tutakwambia bomoa nyumba yako nenda nayo kiwanja ni chetu. Lakini tunasema ni tahadhari tunatoa. Tutarudisha zile nyumba hata kama ni miaka mia kuanzia sasa, ndiyo Utawala Bora. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Moshi Mjini, mwenye kiburi ya kuweza kuja kugombea aje, mwenye kiburi cha kuweza kupigania Moshi namkaribisha aje halafu nitamdhalilisha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ambayo nimeyasema, naiunga mkono hoja na ninaomba myafanyie kazi yale ambayo yatahimiza Utawala Bora. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kuweza kutujalia asubuhi hii kuamka na afya, tukaweza kushiriki katika shughuli za Bunge letu salama salmini. Baada ya shukrani hiyo kwa Muumba pia nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa pili katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze na Utawala Bora. Hatuwezi kusema kwamba, Serikali hii hawajafanya lolote katika suala la Utawala Bora. Lazima tukubali kwamba, kuna mambo ambayo yamefanywa, lakini pia niseme kwamba na mapungufu yapo. Mimi sitaki nitaje mengi, lakini nitataja mambo mawili. Naomba Serikali, haya mambo ambayo nitayataja ili kuiweka Serikali katika nafasi nzuri katika *record* ya Utawala Bora, basi wangeyachukulia hatua ya haraka.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, juzi tulisikia kwenye vyombo vya habari sakata la Wananchi, wapiga kura wetu wa Serengeti kwamba, Serikali kupitia Mkuu wa Wilaya, imevunja nyumba za Wananchi. Kwa kweli ni kitendo cha kusikitisha kwa sababu kwa namna yoyote itakavyokuwa kwamba sisi tunaokusudia, tunandaa mikakati mbali mbali ya MKUKUTA, MKURABITA na mingine katika kupunguza umaskini, leo tunathubutu kuwavunjia Wananchi kadhaa makazi. Kwa vyovyote itakavyo kuwa, basi Serikali ingetafuta njia mbadala ya kutafuta suluhisho la eneo hilo. Lakini kwa kweli haikuwa sahihi hata kidogo kuwavunjia Wananchi makazi, wanyonge ambao hawamudu kuweza kupata nyumba. Kwa hiyo, nadhani suala hili kwa kweli Serikali iko haja ya kulitazama, vinginevyo kwa kweli halitatoa au halitoi picha nzuri kwamba kuna Utawala Bora Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la pili, nilipoingia mwaka 2003 nakumbuka Mwezi wa 11 niliuliza swali hapa ambalo lilikuwa linahusu walioathirika katika maandamano ya tarehe 26 na 27 Januari 2001. Suala lile likapelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu na ninakumbuka kama sikosei Mheshimiwa William V. Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu

(Sera), alijibu kwa niaba ya Serikali na naomba ninukuu machache katika majibu yake. Mimi nilikuwa nimeuliza Serikali ina mpango gani kuwalipa fidia waathirika wa maanadamano ya tarehe 26 na 27? Serikali ikajibu kwamba, hatuna mpango wa kulipa fidia badala yake tutalipa kifuta machozi na mipango hii iko mbioni kutayarishwa na itakapokamilika wahusika watajulishwa. Hiyo ilikuwa ni 2003. Tukakaa mpaka 2004, suala hili ni kimya.

Swali hili liliulizwa tena na Mheshimiwa Masoud kwa namna nyingine. Badala yake suala lile lile, mantiki ile ile, likahamishiwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, likajibiwa kwa namna nyingine. Tukaacha 2004, hii 2005 suala lile mimi nikaliuliza kwa namna nyingine na nikajibiwa katika karatasi ambazo tunawekewa kule kwenye *pigeon-hole* kwamba, suala lako litajibiwa tarehe fulani katika Mkutano uliopita. Ilipofika tarehe ile lile suala sikuliona kwenye *Order Paper.* Nakumbuka kuna siku nilisimama hapa nikitaka mwongozo wa Spika, lakini akanisitisha kwamba, siyo utaratibu. Lakini ilikuwa dhamiri yangu, nilikuandikia Mheshimiwa Spika kwamba, kwa mujibu wa taarifa nilizopata, swali langu hili lingejibiwa leo lakini halimo kwenye *Order Paper.*

Nikamwandikia mama wa maswali akaniambia kwamba, swali lako halijapata jibu kwa hiyo Serikali imesema tuliondoe. Sasa kwa kweli likaondolewa. Nilidhani kwamba, Mkutano huu wa mwisho kwa sababu swali la toka tangu 2003, basi Mkutano huu lingepata jibu, lakini pia halimo katika taarifa ya maswali ambayo yangejibiwa. Hapa inaonesha kwamba, Serikali imekwepa hili suala. Sasa nataka nikumbushe kitu kimoja kwamba, suala hili lilitokana na kuundwa kwa Tume ambayo aliiunda Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, Tume ile aliiunda yeye kwa hiyo majukumu yanarudi kwake yeye na tukumbuke kwamba, Mheshimiwa Rais alichukua ahadi mbele ya Watanzania na Taifa kwa ujumla kwamba, yale yote yanayomuhusu yeye basi atayatekeleza kwa asilimia mia moja. Hili Mheshimiwa Rais linamhusu yeye lakini bado watendaji wake wanalikwepa.

Naomba sana kwamba, hicho mlichodai kwamba ni kifuta machozi, basi kingelipwa kwa hawa Watanzania wanaoishi Pemba. Walioko kule ni Watanzania na tunasema kwamba, Watanzania ni wamoja. Tusiwabague Watanzania kwa sababu tu wanatoka Pemba. Hili nilidhani kuwa ni moja kati ya jambo ambalo linaweza kuwa ni dosari kubwa katika Utawala wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Basi nakuambieni kwamba, hili la kutolipwa hicho kifuta machozi kwa walioathirika na maandamano, miongoni mwao mna yatima na mna vilema ambao wamevunjwa. Kuna wanawake wengine ambao walikuwa ni wakulima sasa hawawezi tena kulima wamevunjwa wakiwemo ndani ya Jimbo langu la Ziwani. Kwa kweli hili mimi nakuombeni sana Serikali, mfikirie hicho kifuta machozi japo kidogo, muweze kukitoa ili tuthibitishe, tuamini kwamba kweli Serikali hii inajali haki za binadamu, inajali Wananchi wake, inatekeleza Utawala Bora. Nadhani ombi hili, Serikali yote iko hapa, mtalichukulia hatua muafaka.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nataka niseme ni suala la rushwa na takrima. Suala hili mara nyingi nilikuwa nikisema mimi humu kwamba, kwa kweli tatizo la

rushwa, bado ni *crucial* katika nchi yetu na dunia kwa ujumla na hatua kadhaa kila siku zinachukuliwa lakini kila kukicha bado tatizo la rushwa linaongezeka. Sasa nataka nitoe changamoto kwa Serikali, mara nyingi mmependekeza mambo mengi hapa ili yafanywe lakini sioni kamaSerikali inaona ni ya maana. Sasa nadhani kwa suala la rushwa kama Serikali mtakubaliana na mimi, nina ushauri mzuri lakini kwa kuwa mara zote ninapotoa ushauri huu hamtekelezi, basi leo sitautoa hapa. Lakini nasema kama mnataka kweli tuondoe rushwa, nitafuteni niwape dawa ya rushwa leo hapa. Sisemi naacha *question mark. Inshallah* tutakapoingia madarakani Novemba 2005, basi nitatoa kwa sababu najua ushauri wangu utasikilizwa. *(Kicheko/Makofi)*

Pamoja na kima cha chini kufikia Sh. 60,000/=, bado ni kidogo mno kulingana na hali ya maisha ya nchi yetu. Hali ya maisha ni ngumu, tukiichukua Sh. 60,000/= tukaitia katika matumizi ya chakula, huduma za afya, matibabu, masomo, kulipia maji na umeme, kwa kweli hata asilimia tano bado hujafanya kitu. Kwa hiyo, bado Serikali, pamoja na kufikia hapo mlipofikia, iko haja ya kukaa tena upya mkaangalia angalau kwa asilimia 100 ya hiyo ambayo mmekusudia kwamba, ndiyo kima cha chini, yaani badala ya kuwa Sh. 60,000/= angalau ikawa Sh. 120,000/=.

Mheshimiwa Spika, la nne ni suala la UKIMWI. Hili nalo ni tatizo kwa kweli. Mimi mara nyingi nilikuwa nalisemea suala hili. Serikali inatumia mamilioni ya pesa kuwafundisha Watanzania lakini ndiyo Watanzania hao hao wanaondoka mmoja baada ya mwingine. Sasa nadhani inabidi tubadili mtazamo wetu katika suala la UKIMWI. Ninapendekeza kwamba, hebu sisi kwanza viongozi tuwe mfano katika suala hili. Namna gani, hebu tujaribu kufanya marekebisho katika sheria zetu kwamba, wale wote iwe ni mfano kwa Watanzania ambao wanataka kugombea nafasi za uongozi ndani ya Serikali kuanzia Diwani, Mbunge, Mwakilishi, Rais na wote kwa ujumla, basi iwe *certificate* ya kwanza kabisa ya kuwa nayo mtu ni *HIV Negative.* Najua kwamba, hili kwa kweli linauma, lakini ndiyo ukweli wenyewe ulivyo. Wengi watasema huyu kijana mkorofi, lakini kwa kweli kwa nini tusipime na ikawa sasa wewe kama unataka kwenda kugombea baada ya kuwa wewe una sifa ya miaka 21, ni Mtanzania, basi sifa ya tatu iwe una *HIV Negative.* Bila kuoneana haya, kila mtu atajichunga na kweli Watanzania watajua kwamba kweli sasa viongozi wetu hili wamekusudia kulipiga vita. Hebu tujaribuni hili Waheshimiwa Wabunge, wala tusione uzito sana katika hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tano ni utumishi na ajira katika nchi yetu. Nchi yetu tulikubali kwa makusudi kabisa kuingia katika mfumo wa vyama vingi, kwa hiyo, baada ya kuingia katika mfumo wa vyama vingi ni dhahiri kwamba, mambo mengi yatabadilika, miongoni mwa mambo hayo tulidhani kwamba ni suala zima la utumishi na ajira kwamba, sasa utumishi na ajira usingezingatia itikadi ya kisiasa ambayo mtu anayo. Tulidhani kwamba, sasa kwa sababu tumeingia katika vyama vingi na kila Mtanzania ana haki ya kuingia katika chama chochote, basi itikadi yake isingekuwa ni kigezo cha kutumika katika kupata ajira Serikalini.

Mheshimiwa Spika, sasa bado hasa ngazi za huku chini za utumishi unazingatia itikadi ya kisiasa. Mheshimiwa Waziri, kama bado wewe hujui hilo, huku juu kidogo

kuna afadhali afadhali lakini ngazi za huku chini vijijini hao watendaji ambao mnawaweka kwa kweli wanawanyanyasa watu sana kwa sababu za itikadi zao tu za kisiasa. Ukionekana wewe ni mpinzani basi tayari umekwisha onekana adui. Sidhani kama Upinzani ni uadui na kama ni uadui, kwa nini mlikubali hapo mwanzo? Upinzani nadhani umesaidia sana kutufikisha hapa ambapo leo tumefika. Kama si Upinzani nakuhakikishieni kwamba hapa ambapo tumefika sisi na matunda haya ambayo tunayo tusingekuwa nayo. Kwa hiyo, lazima tuuchunge, tuuenzi na tusionekane kwamba sisi wapinzani ni watu wakorofi, hapana si kwa sababu sisi ni wapinzani kwa hiyo tunapinga kila kitu. Sisi tunapinga pale ambapo panastahili kupingwa na pale ambapo panastahili kupongezwa sisi tutapongeza kabisa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri katika hili, unapokutana na watendaji wako wa chini hawa, waambie tumo katika vyama vingi na wapinzani msione kwamba ni maadui lakini tunawategemea wasaidie katika kuendesha nchi yetu kwa maslahi yetu sote. *(Makofi)*

La mwisho, niseme kwamba namshukuru Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (UTUMISHI), kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii. Mimi niseme kwamba, toka tuanze katika mambo ya kuwasilisha, basi usomaji wake umenivutia sana. Kwa hiyo, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kabla ya kuchangia, napenda nichukue nafasi hii, niwape pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana na Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, ambao wametutoka. Tunaomba Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana alikuwa dada yangu na kifo chake kwa kweli nilipata habari nikiwa Japan nilisikitika sana. Kwa hiyo, tumeguswa sana.

Napenda nichukue nafasi hii kwa moyo wa dhati kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, kwa hotuba yake nzuri sana, aliyoitoa hapa ndani. Vilevile nichukue nafasi hii nimpongeze yeye na wafanyakazi wa Wizara yake, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika miaka mitano ambayo Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, amekuwa Waziri katika Wizara hii. Mambo mengi mazuri yamefanyika, hakuna mtu yeyote anayeweza kusimama hapa akasema hajayaona mazuri yaliyoyafanywa, yanaonekana na nitayataja baadaye. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, mtani wangu wa jadi kabisa, kwa kazi nzuri aliyofanya katika wakati wake, *PCB* imeenea katika kila Wilaya. Sasa hivi nikiwa na shida au kero yoyote mtu akiniletea, namwambia bwana chukua barua nenda *PCB.* Majibu ambayo nimekuwa nikipata kutoka kule *PCB* ni kwamba yanashugulikiwa vizuri. Kwa hiyo, hongera sana Mheshimiwa Wilson Masilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii vilevile kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu. Katika miaka kumi hii iliyokuwa madarakani, imeboresha kabisa

maisha ya wafanyakazi. La kwanza kabisa ilikuwa kupandisha mishahara kutoka shilingi 17,000/= mwaka 1995 na leo ni 60,000/= na leo kima hicho nafikiri kimepanda kwa asilimia 27. Hayo ni maendeleo mazuri na Serikali inaonesha kwamba, inajali wafanyakazi na hivyo napenda kuipongeza, hongera sana. *(Makofi)*

Naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Ukiangalia majengo hata la kwetu kule Dar es Salaam, safi kabisa, hili la hapa linakamilika, Wabunge watakaokuja wataishi mahali pazuri kabisa. Angalia Wizara zilivyo nzuri, angalia Wizara ya Mambo ya Ndani safi kabisa, ya Utumishi kule safi. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri hiyo. Vilevile napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa sababu imeanzisha Bima ya Afya ya wafanyakazi. Haya ni maendeleo mazuri kwa sababu zamani ilikuwa kero lakini sasa ukiumwa unachofanya ni kwenda hospitali, una Bima yako pale unatibiwa.

Lakini kikubwa ambacho nataka kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu, angalau watu wamepiga kelele na kazi kubwa iliyofanywa ilikuwa kuwauzia wafanyakazi nyumba za Serikali. Mwanadamu hujakamilika kama huna nyumba, familia yako inaishi kwa wasiwasi. Sasa kitendo cha Serikali kuuza nyumba zilizokuwepo halafu haikukomea hapo, imejenga nyumba angalia Dodoma hapa, kama unakuja na ndege, unafikiri ile bahari gani. Nyumba safi kabisa zimejengwa na nina hakika kila mfanya kazi hapa Dodoma zile nyumba zinatosha atapata nyumba. Sasa mnataka Serikali ya aina gani tena. Safi kabisa, Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya kazi nzuri kabisa.

Kuhusu Utawala Bora, Watanzania lazima tuangalie. Tunaweza kusema mambo ambayo mengine hata mtu mwingine akisikia anashangaa hivi hawa wakoje. Hakuna nchi ambayo ina Utawala Bora katika nchi ambazo nimetembelea, nimetembea Mabara yote Duniani, ndiyo nimewasili toka Japan jana. Lakini ukiangalia Tanzania, Utawala wake Bora, yaani ni wa hali ya juu. Sikiliza Waamerika wenyewe, nimemsikia Bush mwenyewe juzi anasema nchi kama Tanzania tutaipa misaada kwa sababu ina Utawala Bora, Rais wa Amerika, halafu leo tunasimama tunasema nchi haina Utawala Bora; hivi tunataka kuipeleka wapi hii nchi!

Tangu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, amekuwa kwenye Utawala wake, sijawahi kusikia sijui anamuweka mtu ndani. Mrema ametamba miaka kumi, sijawahi kusikia Mheshimiwa Rais akisema weka ndani huyu mtu. Profesa Ibrahim Lipumba, ametamba amepewa uhuru anatamba mpaka leo, yuko safi, sijawahi kusikia akitishwa. Rais Benjamin William Mkapa amekuwa ni mtawala safi kabisa, hana wasi wasi na lolote. Nchi nyingine, angalia *Ivory Coast, Congo* hapo, kila siku wanakuja kupatanishwa hapa nyumbani, Burundi watu kule wanauana, leo Mtanzania gani umesikia ameuwawa.

Kama ni mambo ya uhalifu basi hayo ni mambo mengine, tunamkamata tunamuweka ndani, hiyo ni sheria, lakini kusema kwamba Serikali ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa imemwadhibu mtu kwa sababu ya kisiasa hamna. Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii nimpongeze mia kwa mia. Ni Rais mzuri huyu katujengea

uchumi, kaleta Utawala Bora, lakini bado tunasema hakuna Utawala Bora, Utawala Bora gani mnaoutaka?

Mtu ni kuwa huru na Jimboni nimeangalia kulipokuwa na matatizo niliwapeleka *PCB* wakashughulikiwa. Sasa hivi tunaenda kugombea Ubunge, hakuna mtu atakayekamatwa kwa sababu ni wa Chama cha Upinzani. Nenda ukipita utakuja Bungeni, Wananchi wakikuzuia hata sisi wa CCM ndiyo itakavyokuwa hatuna hakika. Hii ni Serikali ambayo sijawahi kuiona, nimetembea nchi na nchi zenye Utawala Bora kama hii hata Bush mwenyewe anaisifu. Hii ni Sera ya CCM wanasema kwamba, Utawala Bora lazima uwepo nchini. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ametekeleza hivyo. Sasa kosa tena liko wapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kuna machache ambayo nitatoa ushauri kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa ni kwamba, nimekuwa katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara, nimetembelea viwanda vingi, nimetembelea sehemu nyingi na kitu ambacho nimekuta ni kwamba kuna kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania, lakini zinafanywa na wageni. Mfano, hizi shule uzosikia za Kiingereza zimejaa wageni, nashangaa! Hata mwalimu wa *primary school* ni mgeni. Ina maana sisi kweli hatuna watu wa kuweza kufundisha katika hizo shule? Hao watu wanakujaje mpaka wanapata hizo kazi?

Mheshimiwa Spika, ninachoshauri ni kwamba, naomba Wizara ya Utumishi iweke kwamba wale watu ambao wanatoa kibali cha watu wanaokuja kufanya kazi nchini wawe ni watu *senior, very senior* kama Katibu Mkuu awe mle, hata ikiwezekana na Waziri Mkuu awe mle ili mtu kabla hajapewa kazi kwanza itangazwe nchini.

Mheshimiwa Spika, mimi nilienda kufanya kazi Zimbabwe, kazi yangu ilitangazwa na hakuna Mzimbabwe aliyetokea mwenye sifa kama zangu, nikapewa ile kazi, lakini walikaa Makatibu Wakuu, sikwenda tu kienyeji na walipopata mtu mimi niliondoka. Kwa hiyo, tunaomba kuwe na wakala wa kuchunguza mambo hayo kabisa.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama Kamati ikiwepo itaruhusu walimu wa *primary school* kuja kufundisha katika shule hizo zinazoitwa sijui *international. International* gani, ukienda shule hiyo wala siyo *international,* lakini wamejaa watu toka nje tu na vijana wetu waliomaliza ualimu wanahangaika! Vile vile, ukienda kwenye viwanda unakuta mtu tu amekuja pale ni *supervisor* sijui nini, yaani tumeshindwa kupata mtu wa ku-su*pervise* watu kwenye *textile mills!* Nenda pale Vingunguti kwenye kile kiwanda, ukiingia unakuta ni watu wamevaa nguo zile za *Panjab* ndiyo ma-*supervisor* pale na vijana wetu wanafanya kazi katika mazingira mabaya sana. Kwa hiyo, tunaomba sana tuangalie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu mishahara kwa sekta binafsi. Serikali leo tumepandisha mishahara, wenyewe hawapandishi. Mtu anatoka Uingereza anakuja kumlipa Mtanzania shilingi 20,000/= !

**MBUNGE FULANI:** Shilingi 15,000/=.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Shilingi 15,000/=. Jamani Serikali angalieni suala hili. Mtanzania hapa ndiyo kwao, hana mahali pengine! Mtoto hujivunia baba yake na mama yake, sasa Mtanzania anajivunia Serikali ya Tanzania, hao watu wasitoke nje kuja kunyanyasa watu wa kwetu hapa. Ndiyo tumewakaribisha, lakini binafsi sidhani kama kweli unahitaji mwalimu wa *primary school* kutoka Kenya! Elimu yetu ni safi na tuna watu na pale ndiyo watu wanalipwa mishahara mizuri, sasa unakuta watu wa nje wamekuja pale. Pia sidhani kama unahitaji Mhindi toka *Panjab* kuja ku-*supervise* Mtanzania, halafu Mtanzania huyo anakuwa na hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, angalieni viwanda kama hivi vya sabuni. Mfano nilikwenda Tanga, unakuta watu wetu wanaofanya kazi wana hali mbaya sana. Kwanza unakuta katika *management* yote hakuna Mtanzania, ni watu kutoka sehemu nyingine. Halafu Watanzania asili sasa *digenous,* unajua kuna *indigenous,* sasa unakuta *indigenous* yaani ukiangalia hali aliyonayo inatia aibu! Jamani, hii ni nchi yetu na ni lazima Mtanzania apate anachostahili kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa kazi, ili Taifa liendelee ni lazima lifanye kazi kwa bidii na kwa muda unaotakiwa. Mimi nimechunguza, ukiangalia Dar es Salaam mtu anafika kazini saa mbili na saa tisa anaondoka. Muda aliofanya kazi ni saa saba, lakini vile vile ametumia huo muda kwa *lunch,* ametumia kupumzika na kunywa chai. Ukitoa pale tunafanya kazi saa sita tu, hatutafika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana tubadilishe utaratibu wetu. Kama mtu anakuja saa mbili kama kawaida, atoke dakika 15 za kunywa chai, tena iwe *official* asiulizwe, wewe mbona umetega kazi? *Official* kabisa, iandikwe pale. Ikifika saa saba aende kula kwa ile saa moja, hata kama anaenda benki asiulizwe kwa sababu ni muda wake, ikifika saa nane ndiyo atamaliza kazi saa 11. Kufanya kazi saa sita ni hatari sana kwa Taifa. Halafu ukienda hapo Kenya utakuta ni hivyo hata ukienda Zimbabwe, ni lazima wanapumzika. Lakini kuchukua saa mbili mpaka saa tisa na mtu anakula hapo kwa saa moja, jamani hatutafika mbali, *productivity* ni lazima iende na muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo sikuwa na mengi ya kuchangia, ila napenda nichukue nafasi hii kwa sababu hizi ni dakika za mwisho niwashukuru sana wananchi wa Serengeti kwa kunichagua kwa miaka mitano. Tumefanya kazi kubwa na ndugu zangu wa Serengeti, tumechimba malambo, sasa hivi umeme unakuja, barabara zetu zinapitika, MMEM imetusaidia kujenga shule za kutosha, kwa hiyo, kwa sasa wanaokuja ni wakati muafaka kuendeleza hayo yote. Vijana wanaokuja wasiwasumbue wapite tu ili tarehe 4 tupambane. Wakinishinda sawa, nikishinda sawa, kwa hiyo, sasa ni muafaka, wafike vijana bila matatizo nawakaribisha. *(Makofi)*

Mwisho kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru mke wangu mama Neema na wanangu. Muda mwingi nilikuwa sipo nyumbani, lakini wamenivumilia mpaka sasa na vile vile nawashukuru sana marafiki zangu na ndugu zangu ambao

waliniunga mkono pamoja na Wabunge wenzangu kwa namna tulivyoshirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoletwa leo hii na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kufanya hivyo naomba kwa masikitiko makubwa kabisa niweze kutoa pole kwa familia za watumishi wafuatao wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa waliopata ajali sehemu ya Chalinze.

Ni watumishi saba walipata ajali wakafariki pale pale, tena ajali ambayo ilikuwa ni mbaya sana. Watumishi hawa walikuwa ni Kamanda wa *PCB* wa Mkoa wa Singida, mke wake na watoto wake wawili, Mhasibu wao wa Mkoa, dereva pamoja na mlinzi wao. Jumla walikuwa watu saba na wote walifariki hapo hapo. Mwenyezi Mungu azilaze pema peponi roho za marehemu hao waliokwenda kwa pamoja kwa masikitiko sana. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Kamanda huyu wa *PCB* kwa kweli alikuwa ni kijana mmoja mchapakazi sana na kwa muda mfupi ambao aliweza kukaa Singida aliweza kutuelimishia tangu viongozi wa Vijiji, Kata mpaka Wilaya kwa kuwapa semina, kuwaelimisha kuhusu masuala ya rushwa, kuwaelimisha masuala ya utawala bora na kuweka mambo safi kabisa katika Mkoa wetu wa Singida. Lakini basi kwa bahati mbaya Mungu naye labda anapenda kuwachukua hao wazuri mapema, kazi yake haina makosa, tumekubaliana na hilo, lakini tunasikitika sana kwa kuwapoteza kwa mara moja watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba sasa nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza Mawaziri wetu hawa wawili ambao wameleta bajeti yao, hapa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika muda wao wote huo. Ukweli ni kwamba mambo mengi katika uboreshaji wa utumishi wa umma yamebadilika tangu tulipoanza na hata ukiangalia hapa tunapiga maneno, lakini ukweli ni kwamba utawala bora hapa hapa unaonekana. Tulipoanza hapa mwaka 2000 hali haikuwa hivyo, lakini leo unakuta wenzetu kwa mfano upande wa upinzani mambo wanayoongea, wanaongea vizuri sana. Hiyo ni sehemu ya utawala bora, imewanoa mpaka wamebadilika, sasa wanaongea mambo mazuri kabisa.

Sasa tukianza kusema kwamba utawala bora haujafanya kazi, nashindwa kuelewa na hata sasa hivi wanaanza kutamka kwa matumaini, wanaanza kuishi kwa matumaini maana matumaini yao wanayotaka ya miaka 100, tunataka muelewe hivyo kwamba baada ya miaka 100 ndiyo mtaanza kunukia nukia labda pengine kukabidhiwa nchi, lakini kwanza muelewe utawala bora jinsi unavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba katika bajeti hii nizungumze yangu machache tu ambayo nimeyaona na ambayo nafikiri niishauri Wizara ili iweze kuendelea kuboresha utumishi bora na kuboresha utawala bora.

Mheshimiwa Spika, tangu tuanze utawala bora umeshaonyesha tofauti ya tulikokuwa na hapa tulipo sasa. Mambo mengi yamebadilika kwa watumishi ikiwa ni pamoja na mishahara, vitendea kazi, pamoja na sehemu za kufanyia kazi. Lakini hata hivyo bado tuna safari ndefu sana ya kufanya shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji ambao tunausema bado katika sehemu nyingi za Wizara nyingi unakosekana, moja katika hivi vinavyokosekana ambao bado unajieleza ni katika sehemu chache au Wizara chache kupandisha vyeo watumishi wake, bado kuna matatizo.

Mimi nina matatizo katika Wizara ya Afya, hasa kwenye hospitali zetu. Nina malalamiko mengi sana ya manesi na watumishi wengine katika hospitali kwamba hawajapandishwa vyeo kwa muda mrefu na wale waliobahatika kuletewa taarifa ya kupandishwa vyeo hawajapewa mishahara yao. Sasa unashindwa kuelewa kwa nini umpandishe mtu cheo kama hauko tayari kumpa mshahara unaolingana na ngazi hiyo! Tafadhali tuliangalie suala hilo kwa sababu bado lipo sana kwa watumishi wa ngazi hizo na sielewi ni kwa nini wakati sasa tunasema tunadumisha na tunaboresha kumbukumbu zetu.

Mheshimiwa Spika, walimu nao ni yale yale, wengine wanapandishwa vyeo na hasa walimu wa sekondari, wanapandishwa vyeo lakini hawapati mishahara inayolingana au wakati mwingine anakutwa hata na yule anayeajiriwa leo. Sijui huyu anayeajiriwa leo kumbukumbu zake zinaonekana vizuri, maana mshahara wake unalingana na yule aliyeajiriwa zamani. Sasa hiyo ni kasoro ambayo inamfanya huyu avunjike moyo wa kufanya kazi. Tafadhali naomba tofauti ndogo ndogo kama hizo zirekebishwe ili tuweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira bora ya utumishi ambayo yamezungumzwa, tukiangalia ukurasa wa 23 katika ile sehemu ya 33 ambayo Mheshimiwa Waziri anasema: "Mazingira mazuri yamekwenda sambamba na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi, maeneo yaliyotiliwa maanani katika maboresho haya ni pamoja na mazingira ya ofisini ambapo ofisi za Serikali zinaendelea kuboreshwa ili zikidhi afya za kikazi."

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hayo na wala sina ugomvi, lakini mazingira mazuri haya mbona tunaendelea kujiwekea ofisini Dar es Salaam na maofisi mengine mikoani? Mazingira gani haya sasa ambayo tunawawekea wafanyakazi walioko katika sehemu nyingine hasa vijijini kwenye kata na tarafa zetu mbona mazingira bado ni yale yale?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mazingira bado yanakatisha tamaa na ndiyo maana tunakuta watumishi wanakimbilia mijini, walimu wanakimbilia mijini na waganga wanakimbilia mijini kwa sababu bado hatujawawekea mazingira mazuri kama ambavyo

tunajiwekea mazingira mazuri mijini. Sasa hiyo ni kasoro moja kubwa sana kwa sababu tutaendelea kuwa na watumishi wanaong'ang'ania kubanana mijini. Walimu wengi sasa hivi tunajua kwamba wako mijini na hasa akinamama kwa sababu wanashindwa mazingira ya kule vijijini. Yuko tayari kufunga ndoa hata na ndugu yake au kaka yake ili mradi aonekane amefunga ndoa na mtu ambaye anafanya kazi mjini ili arudi mjini. Hii yote ni kwa sababu ya mazingira ambayo hayaridhishi kule.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwamba moja ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi ni kujenga nyumba za watumishi. Mtumishi akipata nyumba nzuri ataishi, lakini anakwenda kule hakuna hata nyumba ya kupanga, sasa huyu mtumishi unategemea hata kama angekuwa mtiifu vizuri namna gani aishije kule? Hasa akinamama, unakuta wanakuwa na matatizo sana, angalau hata vijana wa kiume wale ni rahisi kwa sababu anaweza akafanya urafiki hata na kijana mwenzake mmoja akaenda kuishi mahali pengine, lakini kwa mwanamke inakuwa ni tatizo. Tunataka tuwalazimishe wengine waanze kuolewa mahali ambapo haiwezekani!

Naomba watumishi wajengewe nyumba hasa watumishi wa vijijini. Tuwajali hawa wa vijijini na kama hatuwezi kuwajali labda pengine bado uwezo wa Serikali wa kujenga nyumba vijijini kwa haraka sasa hivi haupo, hebu tutofautishe basi mazingira haya kwa kuwawekea angalau mishahara yao kidogo tuwape nauli na angalau posho kidogo ya kuweza kuwafanya ziwafanye waishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, huyu mtumishi analipwa shilingi 60,000/= au shilingi 80,000/= na wa mjini analipwa hivyo hivyo, sasa hebu niambie huyu anatumia muda wake kutoka kijijini nauli labda shilingi 5,000/= anakuja kufuata mshahara na anapofika pale ni lazima ale, alale, inakuwa amepoateza zaidi ya shilingi 30,000/= katika mshahara wake wa shilingi 80,000/=, anaondoka pale na shilingi 40,000/=, lakini wa mjini anapata pesa yake hiyo hiyo shilingi 80,000/= akichukua anakwenda zake nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa nini huyu naye asione ni heri aje mjini ili kama ni mshahara wa shilingi 80,000/= aendelee kupata huo huo? Kama nyumba na vitu vingine bado tunaona tofauti kuwapatia, hebu tuwapatie mishahara au hata motisha kwa kuwalipa nauli zao pamoja na posho ndogo ndogo ili tuweze kuwaboresha hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira mazuri ambayo yamewekwa au hasa kumbukumbu ambazo Mheshimiwa Waziri amesema, kwamba kumbukumbu za watumishi zenye uhakika Serikalini zimefanikiwa kuanzisha mfumo wa kumbukumbu za watumishi kulingana na orodha ya malipo ya mishahara yao. Nashukuru kwamba wamefanya hivyo, lakini bado kuna matatizo pia. Hivi inakuwaje mtumishi tena pengine ambaye ni *very senior* yuko hapo hapo Wizarani anahamishwa labda kutoka kitengo kimoja anapelekwa kitengo kingine. Kwa kuhamishwa kupelekwa kwenye kitengo kingine anashindwa kupata mshahara, kwa sababu ametoka kwenye kitengo kile amewekwa kwenye kitengo kingine, lakini yuko kwenye Wizara hiyo hiyo lakini anashindwa kupata mshahara wake kwa muda labda a miezi mitano au kumi inakuwaje? Kumbukumu hizi zinakuwaje kwamba mtu amehamishwa tu hapa ni kwa nini asipate mshahara wake? Anaambiwa labda bado Utumishi, bado sijui wapi, bado kumbukumbu zako

zinarekebishwa. Hivi kumbukumbu zinarekebishwa kwa muda gani hadi mtu kupata mshahara? Unategemea huyu mtumishi aendelee kukufanyia kazi nzuri wakati miezi mitano/sita, hajapata mshahara wake na ni *senior officer!*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kumbukumbu bado zina matatizo, naomba kumbukumbu hizi ziendelee kufanyiwa utafiti. Wapo watu wa namna hiyo ambao wanatulalamikia, tena mtu yuko pale pale Wizarani. Hivi inatokea nini au ni chuki binafsi kati ya watumishi na watumishi? Maana mimi sioni kama kuna tatizo, takwimu za mtu yuko pale pale halafu anashindwa kupata mshahara kwa muda wa miezi hiyo, nafikiri labda ni tatizo lingine na wala siyo tatizo la kumbukumbu zake. Sasa chuki binafsi tukizileta makazini, utawala bora sasa unakuwa kwenye matatizo. Ni kwa nini ulete chuki binafsi kwenye kazi ya Serikali? Kama mmekosana huko basi mrekebishe mambo yenu huko, lakini kazi za Serikali ziende vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru utawala bora kwani sasa hivi umetuwekea mazingira mazuri na hasa nishukuru kwa ofisi ambazo zimefunguliwa Wilayani na Mikoani za Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Sasa hivi vijana waliko kule naona wanaendelea kupambana na masuala ya sasa hivi yanayokuja ya uchaguzi na ninafikiri hali wanaiweka vizuri. Hebu waendelee na kasi hiyo na hasa kasi ya kuelimisha Wananchi. Ninamwomba Waziri asichoke maana bado ofisi hizi sehemu nyingine hazijaeleweka kwa wananchi na wengine bado wanaziogopa, mtu anafikiria labda akipeleka mambo kule pengine ataeleweka vibaya. Elimu ifanyike ili wananchi waelewe hizi ofisi na kwa hiyo iwe rahisi kwao kupeleka matatizo wanayoyapata. Wananchi katika sehemu nyingi wanapata matatizo, wanaonewa, lakini mtu kwa kutokujua haki yake anashindwa aende wapi, lakini kama anajua hiyo ofisi akifika mahali ameombwa rushwa nina uhakika mambo yatakuwa yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya machache, naomba niunge mkono hoja hii na nawatakia kila la kheri ili mambo yaweze kuwa vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha Mheshimiwa Margareth Bwana, naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi na awape roho ya ustahimilivu ndugu zake, lakini pia naomba Mwenyezi Mungu atupe sisi Wabunge Wanawake roho ya ustahimilivu kwani hatujazoea mwanamke kufariki, mara nyingi wanafariki wanaume tu. Katika kipindi cha miaka kumi alifariki Mbunge mmoja mwanamke wa CHADEMA Viti Maalum na sasa Mheshimiwa Margareth Bwana. Kwa hiyo, wanawake kwa kweli, kwa kutokuzoea tu hii imetuumiza sana, lakini maamuzi ya Mwenyezi Mungu hayawezi kupingika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwako wewe na kwa Bunge kwa kuruhusu Wabunge kuwa na *caucus.* Katika kuwa na *caucus,* sisi Wabunge tunaopenda kupambana na rushwa ulituruhusu tukawa na *caucus* inaitwa *African Parliamentary Network Against Corruption, Tanzania Branch.*

Naomba nikushukuru sana na kwa msaada wako kwani tuliweza kufanya kazi na kushirikiana vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na hasa Utawala Bora kwa kushirikiana na *caucus* hii ya Wabunge ya *African Parliamentary Network Against Corruption, Tanzania Branch.* Tumeshirikiana sana na wameweza kusaidia Wabunge kuelewa masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na semina mbalimbali waliweza kutuunganisha na *organization* za Kimataifa kwa mfano *UNDP,* waliweza kutupatia semina mbalimbali. *APNAC* kwa kushirikiana na *Tanzania branch* tukaweza kushawishi hata *caucus* kama hii ya Wabunge ianzishwe kwenye dunia ambayo inaitwa *GOPAC.* Pia, kwa kushirikiana na Wizara hii, *SIDA* imeweza kutusaidia kwa semina mbalimbali na hata kututoa nje ya nchi kwenda kujifunza. *SUNNY Tanzania* pia imetusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba, aliyeshirikiana na sisi katika kutushauri ili tuweze kufanya kazi vizuri hasa katika suala zima la kupambana na rushwa. Natoa shukrani zangu kwa *NGO's* mbalimbali zilizokuwa na msukumo huu wa kupambana na rushwa, tulifanya nao kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nitoe pongezi kwa Serikali. Kwa kweli waliweza kuimarisha utekelezaji wa ule Mpango wa Kitaifa wa Utawala Bora na Vita Dhidi ya Rushwa katika Sekta zote za Serikali. Katika kufanya hivyo, sehemu kubwa kabisa za idara ziliweza kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji. Ziliweza kutoa ufanisi mkubwa kabisa na naomba niseme bila ya kusita kwenye suala la elimu, kwenye masuala ya ujenzi wa barabara na hata kwenye masuala ya wenzetu wa Polisi na idara mbalimbali ziliweza kufanya kazi kwa uhakika na mafanikio yake tunayaona. Tanzania sasa imefutiwa madeni, hii kwa kweli ni kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika suala zima la utawala bora. Sasa hivi unakuta watanzania wengi wamepewa elimu ya suala zima la kupambana na rushwa kwenye Mikoa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ofisi za *PCB* zinaitwa TAKURU zipo mpaka Wilayani, wananchi sasa wanaweza kufika na kutoa malalamiko na wanakubaliwa na wanapokelewa kwa heshima nzuri na wenyewe wanajisikia vizuri. Kwa hiyo, naomba nionyeshe kwamba haya ni mafaniko ya kitengo hiki. Tukumbuke rushwa ikishamiri hakuna maendeleo katika nchi na uchumi wa nchi unashuka, lakini ninyi wote mtakubaliana kwamba rushwa Tanzania imepigwa vita kwa uhakika na sasa hivi uchumi wa nchi umepanda kwa asilimia 6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba watu hawayaoni haya, lakini wenzetu waliopo nje wakirudi nyumbani wanaona. Sasa hivi ukienda kijijini unakuta barabara safi, unakuta shule safi, haya yote ni masuala ya utawala bora. Naomba niwapongeze sana na ninapongeza kitengo cha *PCB* Serikali imeongeza wafanyakazi *(staff)* na inawapa

*training.* Hii inaonyesha kabisa Serikali ya Awamu ya Tatu ilikuwa *serious* katika suala zima la kupambana na rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepitisha sheria mbalimbali ndani ya Bunge hili. Sheria hizi zilikuwa na nia ya kudhibiti mianya ya rushwa. Naomba niwapongeze na matokeo yake sasa hivi ni kwamba Serikalini kuna kitu kinaitwa *quarterly review,* inatolewa mpaka kwenye magazeti, zamani haikuwa hivyo, huo ni utawala bora.

Mheshimiwa Spika, bado taarifa mbalimbali za Serikali zinatolewa ndani ya magazeti kwa mfano Hazina walikuwa wamelalamikiwa na walimu kwamba hawajalipwa marupurupu yao, lakini wakatoa katika magazeti *cheque numbers* na hata Serikali ikaamua kuunda Tume ya kutafuta na kutazama malalamiko ya walimu. Hii inaonyesha kwa kweli Tanzania imefanya kazi katika suala zima la utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, kila mwisho wa mwezi analihutubia Taifa na kuelezea mambo mbalimbali, huu ni uwazi. Sasa hivi tumeanzisha Sekretarieti ya Maadili na watu wengi huwa wanakwenda kutoa malalamiko mbalimbali japokuwa kwa bahati mbaya inapotokea suala la watu wa Mahakama wamepoteza maadili hii Sekretarieti inakuwa haina meno, naomba itafutiwe utaratibu na yenyewe iwe na meno kwenye suala zima la Mahakama kwa sababu watu wanalalamika, rushwa pia iko mahakamani.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niipongeze Serikali kuonyesha dhahiri katika suala zima la utawala bora na kupambana na rushwa wameweza kutushawishi Wabunge tukaridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kwa mfano, Mkataba ya *United Nation Convention Against Corruption 2003, African Union Convention Preventing Combating Corruption* na la mwisho lililonifurahisha ni sisi kuridhia suala zima la *African Peer Review Mechanism (APRM).*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi bado, sasa sisi kuonyesha kweli suala la kupambana na rushwa tunalikubali na tunalitetea, tumekubali na kuridhia. Nilizungumza na Walibya wakasema wao hawakubaliani na hawatakubali kamwe kwa sababu hii inapendekezwa na wenzetu wa Ulaya, lakini sisi Watanzania tunasema hapana kwa sababu tunashughulika na suala zima la kupambana na rushwa na tuna mikakati na mipango, tumekubali. Kwa hiyo, naomba niwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, naipongeza Serikali kwa kukubali kabisa utawala bora na kwa vitendo. Bunge hapa kupitia Kamati ya *PAC* ili-*table report* ambayo ilikuwa inahisia kwamba kuna rushwa katika *TACAIDS* na suala zima la ule mradi wa...

Mheshimiwa Spika, samahani nimesahau, lakini kuna mradi mwingine wa ...

**MBUNGE FULANI:** *TVT.*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Eeh, *TVT.*

Sasa hivi *PCB* inachunguza, huu ndiyo uwazi wa Serikali. Naomba niwapongeze kabisa. Ombi langu ni kwamba, naomba *PCB* iwe huru. *PCB* kwamba mambo yake ni lazima iripoti sehemu fulani si vizuri. Mfano, ikiambiwa, fanyeni hivi, ndiyo wafanye, nendeni mkashtaki, ndiyo washtaki, msishtaki, wanyamaze!

Hii haina uhuru, sasa hivi kama Nigeria mifano ipo, ukienda *South Africa* mnamwona Makamu wa Rais. Sasa naomba wapewe uhuru.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba vile vile Mheshimiwa Waziri Wilson Masilingi ukiwa una-*windup* waeleze Watanzania wajue maana ya takrima na maana ya rushwa. Hivi vitu ni maneno mawili tofauti. Takrima lina maana gani na rushwa ina maana gani. Kwa hiyo, msinyanyase neno takrima kuliweka neno rushwa tutakuwa tunakosea, Kiswahili kitatupotosha. Takrima ni ukarimu isipokuwa mtu anapofanya ukarimu kwa nia inayoonyesha ni ya rushwa, basi ichukuliwe kuwa ni rushwa na adhibitiwe. Kwa hiyo, tusiyachanganye haya maneno mawili. Mimi naomba niisisitize hiyo sana. Naomba uwatangazie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *PCB* imejitahidi, rushwa nyingi zimepungua, hasa rushwa moja, samahani natamka hili inawezekana siyo neno zuri kwenye Bunge. Rushwa ya ngono katika ajira mmejitahidi. Mimi nawapongeza sana. Lakini kuna rushwa ya ngono inajitokeza katika uchaguzi na baadhi ya wanawake wananyanyasika. Unakuta mwanamke ana uwezo wa kufanya kampeni na watu wanasema wanawake hodari, unakuta mtu anataka kugombea anakwenda kuomba, anaambiwa: "*You must be my friend"* kusudi akishamkubali kwa lolote atamdhibiti. Hii ipo sasa hivi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe. Kuna baadhi yetu Wagombea tunatumia nafasi ya kuwanyanyasa kijinsia wanawake na kuwatisha wakati mwingine ili wakukubalie kufanya kampeni. Hili naomba lichukuliwe kwa uzito wake. Linaonekana geni lakini lipo. Rushwa ya ngono ya ajira ilikuwa ngeni, lakini sasa nimethibitisha na sasa hivi watu hutumia ngono ya uchaguzi kama rushwa ili kumnyanyasa mwanamke, naomba hili nalo litazamwe na *PCB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ninaomba *TRA* isaidie wafanyabiashara wadogo wadogo. Walikubali kutangaza, wana biashara wasaidiwe ili wajue jinsi ya kuweka mahesabu yao ili wailipe *TRA* malipo halali kuliko kuwakadiria, unakuta mtu hana hata biashara, ilikufa anaambiwa unadaiwa Shilingi milioni nane. Naomba wafanyabiashara wadogo wadogo muwasaidie nao watasaidia nchi hii katika kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo na mimi naungana na wenzangu kuiunga mkono Wizara hii, hotuba hii, Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Nawashukuru sana hasa Mheshimiwa Wilson Masilingi, kufanya kazi na mimi kwa muda wote kunishauri na nisifike mahali nikapayuka kwa ajili ya rushwa nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Bajeti hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi. Kwanza nimpongeze Waziri wa Utumishi Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Waziri Wilson Masilingi na bila kuwasahau Makatibu Wakuu wa Wizara hiyo na hasa wataalam wa Wizara hiyo kwa kazi kubwa ya kuandaa Bajeti hii ambayo leo hii imesomwa na leo tunataka kuiangalia na kuipitisha. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia, naomba kupitia Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niwape pole Wabunge wenzetu wa Malawi kwa kufiwa na Spika wao ambaye alikuwa anatetea Katiba ya nchi hiyo ili Wabunge wasimsulubu Rais wao katika nchi yao ya Malawi. Nawapa pole sana na ndiyo kazi. Pia, nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Spika, huyo aliyefariki Afrika Kusini hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia juu ya *TASAF*. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin Mkapa pale alipoamua kwamba mradi wa *TASAF* upelekwe Wilaya ya Temeke ambako aligundua kwamba wananchi wengi walikuwa katika hali mbaya hasa katika huduma za jamii ikiwemo Shule, maji na barabara na vitu kadhaa. Huu mradi ulioletwa Temeke wananchi wa Temeke waliupokea kwa mikono miwili na kwa kiwango kikubwa mradi huu umefanikisha vitu vingi.

Leo hii wananchi wa Temeke hususan Jimbo la Kigamboni wamekuwa wakifarijika kwa kupata maji kupitia visima, Shule ambazo zimeboreshwa kupitia mradi wa *TASAF*, *Dispensary* ambazo zimejengwa kupitia *TASAF* na hususan katika Kata za Kibada, Kisarawe *Two*, Kigamboni yenyewe, Mjimwema, Charambe, Tuwangoma, Chamazi na Mbande ambako visima vimechimbwa. Leo hii wananchi hawana wasiwasi na suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kidogo ambalo limejitokeza katika mradi huu ni pale tu wananchi ambao nadhani kutokana na Elimu yao ndogo, kutokana na vikundi vyao wamekuwa wananunua mashine ambazo mara nyingi zinakuwa zinakufa baada ya muda si mrefu sana. Hilo ni tatizo ambalo nadhani linaweza kutatuliwa na wananchi wenyewe. Lakini nasema kwamba kwa wataalam ambao wanasimamia mradi huu watoe elimu zaidi kwa wananchi wa Jimbo la Kigamboni na hasa hususan Wilaya ya Temeke, kwamba wakati wananunua mashine ya kuvuta maji katika visima hivyo, basi waangalie pampu hizo ziwe pampu za kudumu ambazo zitaweza kuwasaidia zaidi.

Serikali haiwezi kurudia kuchangia tena katika maeneo ambayo imechimba visima kununua pampu ambazo tayari zilishanunuliwa na hela ilishatumika tayari. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi hiyo ambayo sasa wananchi nadhani wanafarijika sana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la Walimu, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesimama kuhusu Walimu jinsi wanavyofanya kazi ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu ili baadaye Watanzania hao waweze kuwa Viongozi wetu.

Nadhani Walimu ndiyo kiungo muhimu katika maisha ya binadamu na vinginevyo hasa kwa Viongozi kwa sababu bila kupata elimu na bila Walimu hao sisi hapa tusingekuwepo Bungeni leo tukizungumzia habari za nchi yetu. Sasa nilikuwa nasema kwamba Walimu wanapotakiwa kupewa mshahara wapewe kwa muda unaotakiwa. Mara nyingi kumekuwa na malalamiko kwamba mishahara yao inachelewa sana. Katika kuchelewa huko kunasababisha kuwe na madeni mengi kwa walimu ambao wanakopa madukani na sehemu mbalimbali wakisubiri mishahara yao. Sasa inapofika siku ya kupata mshahara hela yote anakwenda kulipa deni ambalo alikuwa amekopa kwenye maduka. Sasa Walimu wanapata taabu sana katika hilo.

Kwa hiyo, naomba sana Walimu wapewe mishahara kwa wakati unaotakiwa ili kuepuka adha ambazo wanazipata. Pia, kuhusu posho zao hata za uhamisho wapewe mapema ili wanapohama kwenda maeneo mengine, basi waende mapema na wakiwa na posho zao tayari kuliko kufika maeneo ambayo wanakwenda wanaanza tena kukaa muda mrefu bila kupata posho na pia bila kupata mshahara kwa sababu wanapohama kuhamishia mishahara yao inachukua muda mrefu sana mpaka kupata mishahara yao. Kwa hiyo, naomba pia hilo liangaliwe sana ili watumishi hawa ambao ndiyo nguzo yetu na nyenzo yetu na ndiyo msingi wa maisha yetu sisi wote Viongozi hapa wapewe heshima ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nije kwa ndugu zangu madereva wa Serikali na wa umma kwa ujumla. Kuna wakati niliwahi kuzungumzia kuwaombea madereva kwamba wanapaswa sasa kupata elimu ili angalau wanapopata elimu mishahara yao ipande. Tukumbuke madereva wanachangia asilimia 10 katika pato la nchi yetu na katika uchumi wa nchi yetu kwa sababu dereva ndiye anayehimili na anayetunza maisha ya kiongozi yeyote katika nchi hii na Maofisa wetu.

Dereva anatoka nyumbani kwake saa kumi na mbili kasoro robo au saa kumi na moja alfajiri kukufuata wewe, anakuta wewe unakunywa chai unajiandaa, anakuchukua muda unaotakiwa anakupeleka Ofisini. Anapokuacha Ofisini wewe unapofanya kazi za Serikali yeye anakaa kwenye gari na kuangalia gari lake akiwa amechapa usingizi pale ili kukusubiri wewe utakapokuja. Lakini utakuta posho zao na mishahara yao madereva hailingani na kazi wanazozifanya na michango yao wanayotoa katika nchi yetu. Bila madereva sisi Viongozi hatuwezi kufanya kazi. Lazima tuwe wazi! Kama kuna mtu anapinga hili, atakuwa mtu wa ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitoka hapo unaingia kwenye gari lako unakwenda nyumbani kwako *comfortably* kwa sababu dereva wako amejiandaa kwa ajili ya kukupeleka nyumbani. Kwa hiyo, pia anachunga maisha yako na jinsi wewe unavyokwenda katika shughuli zako. Sasa madereva nao tuwathamini katika suala la posho pia na mishahara yao iangaliwe kwa sababu wao wanatunza roho za Viongozi na wao wanatunza magari ya Serikali, na wanatunza mambo mengi na siri za Viongozi na mambo kadhaa. Sasa lazima wathaminiwe kwa hilo. *(Makofi)*

Nina maana kwamba, madereva pia waendelee kupelekwa kwenye Shule ili wapate elimu zaidi. Kumekuwa na malalamiko hivi karibuni kwamba wale madereva wa

siku nyingi ambao elimu yao wameishia Darasa la Saba sasa wanataka kuenguliwa ili wasiendeshe viongozi. Lakini tunasema kwamba madereva hao ndiyo wametufikisha hapa tulipofika leo hii, tusiwakatae na kuwanyanyapaa. Madereva hao kama kuna kosoro walizonazo ndogo ndogo wapewe elimu zaidi basi ili waendelee kuhudumia Viongozi kwa sababu hawa watakaoajiriwa *Form Six, Form Four* sawa, lakini bado watakuwa hawana uzoefu wa muda mrefu.

Kwa hiyo, naomba sana madereva waangaliwe katika hili, wasiondolewe katika nafasi zao au kunyanyaswa kwa sababu ya elimu zao. Tukumbuke kwamba hawa wametumikia nchi hii kwa muda mrefu na wameendesha Viongozi kwa muda mrefu mpaka hapa tulipo sasa. Kwa hiyo, wathaminiwe kama vile ni Idara ya Viongozi ambao wanaongoza Viongozi wetu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la UKIMWI, mimi naomba Idara ya Utumishi iangalie hasa suala la elimu kwa Watumishi wetu hasa Vijijini tukiondoa Mjini. Kumekuwa kukifanyika Semina mbalimbali kama walivyosema Viongozi wengine hasa Mjini, lakini waathirika wakubwa ni wale ambao wako Vijijini. Haifiki elimu ya kutosha kule Vijijini kuhusu UKIMWI. UKIMWI ni janga. Sasa imefikia leo hii ukienda kule Vijijini kondom moja inatumika na zaidi ya watu wawili kwa sababu ya elimu ndogo kumbe hili ni tatizo kubwa sasa ndiyo maana wanasema elimu ipelekwe.

Pia, gharama ya kununua kondom ipunguzwe, iangalie kule Vijijini. Mtu akifikia kuchukua hatua hiyo ni tatizo. Sasa Ukimwi hauwezi kuishi katika nchi hii na watu tunawategemea ni hao wakulima na wakafanyakazi wetu. Ukifikia hatua mnaingia kwenye Kilabu cha pombe mmeshalewa, basi ile kondom mnatumia watu wawili. Ni tatizo! Bado unakuwa haujaokoa tatizo. Kwa hiyo, elimu ipelekwe Vijijini ili kuwaimarisha wananchi ambao wanatusaidia katika kulima na kuboresha uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kwa kutuongoza vizuri katika Bunge hili na kuwa karibu na Wabunge wote. Umekuwa mcheshi, mkarimu na mtoa mawazo n mwenye kuelimisha Wabunge. Kwa hiyo, lazima tutoe pongezi kwa sababu umefanya kazi nzuri tumeiona. Kama una kosoro zako, basi ni za kawaida ambazo ni za kibinadamu ambazo kila mtu anazo. Hizo hatuwezi kuziingilia, kwa sababu ni suala la binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kumalizia, jana kulikuwa na utaratibu Mheshimiwa Mark Mwandosya alizungumza kwamba tumekuwa tukiwasifia Viongozi, Watumishi na watu kadhaa, lakini tunahasau familia zetu hasa mke na familia yako. Mke wako ndani ya nyumba au mume ndani ya nyumba ndiye anayekuandaa kuja hapa ukiwa barabara. Lakini mara nyingi tumekuwa tunasahau kuwashukuru na kuwapongeza, aidha tunawapongeza kwa kurudi huku wanatupa pole sisi lakini tukumbuke kwamba bila wao sisi tusingeweza kufanya kazi vizuri kwa sababu tungekuwa na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia nafasi hii, naomba nimpongeze sana mke wangu Cecilia Maghoba kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuniandalia nguo na kunizuia

kama nimevaa vibaya kwamba hii nguo siipendi vaa nyingine. Sasa leo lazima nichukue nafasi hii kumpongeza kwa sababu inawezekana ikawa nafasi ya mwisho kuingia ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nisisamhau mama yangu Anne Matingo ambaye ni mzazi wangu pia kwa kunipa ushauri mzuri na kunishauri kwamba siasa uzifuate kwa utaratibu, lakini unapoona zinakushinda achana nazo fanya shughuli nyingine. Lakini namwambia mama kwamba kwa ushauri wake mzuri, leo nimefika hapa pazuri na kwamba nitaendelea kuwa kwenye siasa mpaka nitakapoamua vinginevyo nitawatangazia umma. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wale waliojiandikisha kuchangia hoja hii kwa mdomo wamemalizika, wote wamepata nafasi. Sasa ukiwajumlisha pamoja na wale waliochangia kwa maandishi ndiyo tumefikia mwisho wa Mjadala wa hoja hii. Kwa hiyo, tutakaporejea saa kumi na moja, Watoa Hoja wataanza kuhitimisha tukianza na Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora halafu ndiyo tutamwita Mtoa Hoja mwenyewe. Baada ya maelezo haya sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.43 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipatia nafasi na mimi nishiriki katika mjadala huu ambao unatokana na hoja iliyowasilishwa kwa niaba yetu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kazi nzuri ambayo imefanywa na Waziri mwenzangu Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Waziri mwenye dhamana ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, moja kwa moja napenda nimshukuru kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa niaba ya Ofisi yetu wote. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa mara nyingine, mara ya kwanza kwa niaba ya Ofisi yetu ya Rais katika hotuba yetu kwa pamoja, tumewasilisha salamu za rambirambi. Sasa kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini, naongezea salamu hizo hizo za rambirambi kufuatia misiba mikubwa iliyotufika baada ya kuondokewa na Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na hivi karibuni Mheshimiwa Margareth J. Bwana. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hawa mahala pema Peponi na awafariji Wapigakura wao, familia zao ndugu na jamaa.

Aidha, naungana na Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mbunge wa Singida Mjini kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya vijana wetu watumishi wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa Ofisi ya Singida, Mkoa wa Singida iliyokuwa inaongozwa na Marehemu Juddy Juma Muyovela, ambaye alipoteza maisha na watumishi wenzie Josephat Valley Hugo,

Chambo Said Mwaulambo, Joachim Hala pamoja na mke wa Marehemu Juddy Muyovela, ambaye ni Jenifa Nicholaus Wilkaye na watoto wake wawili Shadrack na Meshack. Naomba Mwenyezi Mungu afariji familia waliobaki, wazazi, ndugu na jamaa na watumishi wote wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye kujibu hoja zilizojitokeza katika maeneo ya Utawala Bora na *TASAF*. Kabla sijajibu hoja moja baada ya nyingine, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu mafanikio ambayo yamepatikana katika eneo la Utawala Bora katika nchi yetu yametokana kwa ushirikiano mkubwa ambao Serikali yetu ilikuwa inaupata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na hasa hasa Bunge zima la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama chombo cha kutunga Sheria na hivyo kuwezesha Serikali kutekeleza mikakati yake na sera ili kuletea heshima nchi yetu na kuhakikishia wananchi wa Tanzania usalama, amani na utulivu ili waweze kukabiliana na matatizo yao ya umaskini na mengineyo.

Sasa naomba niingie kwenye hoja. Nikianza na hoja ambazo zimejieleza kwa kifupi kutoka kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum ambaye ndiye amewasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo - Mbunge wa Kisarawe akisaidiwa na Mheshimiwa George M. Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa. *(Makofi)*

Kamati nzima ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kweli imetusaidia sana kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri mwenzangu katika kutupatia ushirikiano wa kila hali kuongoza shughuli zilizokuwa tumekabidhiwa katika dhamana zetu. Ushauri tuliokuwa tunapewa mara kwa mara siyo katika Bajeti hii, bali tangu mwaka 2000. Lakini pia katika maelekezo mazuri ambayo tumeweza kuyatekeleza kwa sababu tulikuwa tunapewa maelekezo yanayotekeleza ndiyo maana tumepewa pongezi ambazo zimepatikana katika taarifa iliyowasilishwa kwa ufasaha kabisa na kwa umaridadi ambao umemvutia kila mmoja wetu kutokana na kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Tumevutiwa na kupongezwa na Kamati na kusema kweli sina mengi ya kusema kwa sababu hiyo. Kamati ndiyo inayotusimamia kwa niaba ya Bunge Zima na Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia, wote nawapongeza kwa kazi nzuri ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ujumla na hivyo kubakiza kazi ndogo tu ya kujibu hoja ambazo zinajitokeza chache. Tumevutiwa zaidi na Kambi ya Upinzani pia katika taarifa yao kusema kweli na wao wametupongeza sana kwa kazi nzuri. Isipokuwa dada yetu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, amesita tu kusema anaunga mkono hoja.

Lakini sisi tumeridhika na pongezi ambazo ametupatia katika hotuba yake na pia tunapokea kwa heshima ushauri alioutoa juu ya kuboresha masuala ya utawala bora akisema tuboreshe elimu ya uraia ili wananchi waweze kuielewa fika dhana pana ya utawala bora.

Kuhusu takrima, yeye ameahidi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwamba wakishika madaraka watashughulika nayo kwa sababu ni Sheria ya Bunge na sisi tunaomba Mungu tuwemo kwenye Bunge kuona hoja zao katika kuomba Sheria hiyo irekebishwe. Tutashiriki kama mijadala mingine. *(Makofi)*

Lakini siamini kabisa, walianza kufurahi kwamba nimekiri kushindwa. Nataka kumalizia kwa kusema kwamba kwa vile Mheshimiwa Ndesamburo amesema itachukua miaka 100 ndiyo wanakuja hapa, mimi najua sitakuwepo. Sijui Mheshimiwa Ndesamburo kama atakuwepo, lakini na hiyo sina uhakika. Kwa hiyo, sitaijadili, miaka 100 ni mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na hoja za Waheshimiwa Wabunge moja baada ya nyingine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo ameeleza matatizo ambayo anayapata katika Jimbo lake la Moshi Mjini katika Kata ya Kiboriloni. Nilikuwa nimeandika bila kuipata sawasawa, naomba radhi kwa kutoitamka vizuri sana. Lakini maelezo ambayo tunaweza kutolea hoja alizozieleza kutopewa ushirikiano mara viongozi wa Kitaifa wanapotembelea Mkoa wa Kilimanjaro na hususan Moshi Mjini kutoshirikisha Viongozi wa Kata hiyo, sio utaratibu sahihi na kwa kuwa ziara za Viongozi wa Kitaifa huandaliwa na Mkoa na Wilaya, tunaagiza Viongozi wa maeneo hayo wawe wanashirikisha Viongozi wote bila kujali tofauti za Vyama. *(Makofi)*

Aidha, Mheshimiwa Ndesamburo amezungumzia juu ya mipaka ya Kata kutoeleweka sawasawa ya Kata yake, lakini ametusaidia sana kwamba alipowaonyesha mipaka walikubali. Hiyo inapelekea kwamba walikuwa wana mashaka na mipaka kwa sababu hawakuwa na uhakika. Tunamshukuru kwa ushirikiano wake wa kuwaonyesha hiyo mipaka. Kwa hiyo, tunaaamini hilo limekwisha.

Mheshimiwa Ali Said Salum amezungumzia matatizo yatokanayo na matukio ya kusikitisha ya Januari tarehe 26 na 27 huko Pemba yaliyopelekea ndugu zetu kufariki akiwemo Askari wa Jeshi la Polisi aliyetenganishwa kichwa na kiwiliwili. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba, ndani ya Serikali tulishatoa kauli kwamba watalipwa kifuta machozi. Sasa swali limeulizwa kweli mara kadhaa kwa namna tofauti tofauti, ndiyo ikawa inatukanganya tusije tukatoa majibu ya kujikanganya. *(Makofi)*

Lakini msimamo wa Serikali bado uko pale pale kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha linafuatiliwa, watu walipwe kifuta machozi chao haraka sana. *(Makofi)*

Masuala ya Serengeti, ningeshauri tuachie Vyombo vya Sheria kwa mujibu wa taratibu kwa vile viko mbele ya Mahakama, tuachie Sheria ichukue mkondo wake. Lakini nataka kuwahakikishieni haki inaendelea kuzingatiwa katika utaratibu mzima.

Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, kama Waheshimiwa Wabunge wengine ametoa pongezi kubwa sana ambazo nimezipokea kwa ujumla. Lakini naongezea kumshukuru mjukuu wangu huyu kwa jinsi ambavyo sio tu ameunga mkono, bali ametoa ushahidi wa *Hansard* ambayo nimeshatoa *order* niondoke nayo. Maana yake amejenga

hoja mzuri sana kwa ushahidi, ni kwa nini anaunga mkono Serikali ya Awamu ya Tatu inayoongozwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, katika mafanikio yake katika kutekeleza programu ya utawala bora na mikakati ya kupambana na rushwa. Ahsante mjukuu. Pongezi tunazipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, ametushauri kwamba ni vyema tukaboresha Taasisi ya Kuzuia Rushwa TAKRU ili kusudi iweze kuboresha elimu kwa wananchi na hiyo ni baada kuwapongeza vijana wetu waliopoteza maisha kwa kazi nzuri waliyokuwa wamefanya ya mfano, Mkoani Singida kuelimisha kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Mkoa.

Kwa hiyo, sisi ushauri wake Mheshimiwa Nguli tunauzingatia na Ofisi yetu tumeshaiagiza itafute vijana haraka sana wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi na Marehemu ili elimu iendelezwe kwa sababu elimu haina mwisho na pia kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa waweze kushiriki kikamilifu kudhibiti rushwa wakati wa uchaguzi. Kazi hizo watazifanya. Tunashukuru kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Beatus Magayane – Mbunge, ameshauri kwamba Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma isijikite zaidi kwenye kuangalia mali za viongozi tu, bali pia iangalie mwenendo na tabia za Viongozi wa Umma. Napenda kumshukuru kwa pongezi alizozitoa kwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa kwa kazi nzuri aliyoifanya na kushauri kwamba wasibweteke, bali waongeze bidii na wasipuuze taarifa zitakazokuwa zinaletwa na wananchi zinazohusiana na rushwa.

Ushauri huo unazingatiwa na nataka kumhakikishia kwamba Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inafanya kama anavyoshauri na inashirikiana kwa karibu na Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Vile vile, ameishauri Serikali iwe inatumia Sheria na Kanuni na taratibu kusimamia tabia na mwenendo wa Viongozi wa Umma. Lakini pia katika Idara Kuu ya Utumishi kuna Idara ya Maadili ya Watumishi ambayo ina-*deal* na watumishi. Sektretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina-*deal* na watu wazito kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama naye ametoa orodha ya mafanikio na ushirikiano mzuri ambao amekuwa anaupata kutoka Ofisi ya Rais na Utawala Bora na Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Tunamshukuru kwa ushirikiano huo na yeye tunamshukuru binafsi kama Mwenyekiti wa *APNA Tanzania Chapter* na Wabunge wote wanachama na Wabunge wa Majimbo yote.

Kwa Bunge limechangia kwa kiwango kikubwa katika kuboresha mikakati na utekelezaji wa shughuli nzima ya vita dhidi ya rushwa. Ndiyo maana Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama ana uwezo wa kuorodhesha mafanikio katika muda mfupi. Ametoa machache tu na amesema mengi.

Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, amenitaka vile vile nikisimama nielezee tofauti ya takrima na rushwa. Kila ninaposimama hapa naulizwa hilo na sasa karibu imeshakuwa kama mimi ndiyo niliyeleta hiyo sheria ya takrima hapa. *(Kicheko)*

Lakini nataka kuwahakikishieni kwamba huwa natetea Sheria ya Uchaguzi inayohalalisha takrima kama sehemu ya ukarimu. Kwa nafasi yangu ya wajibu kama Mbunge niliapa kulinda Katiba na Sheria na pia kama Waziri mwenye dhamana na Utawala Bora. Naamini kabisa kwamba mtu anayeonyesha ukarimu bila kuwa na nia mbaya, kweli hatoi rushwa. Mimi binafsi nitaendelea kuamini kwamba mtu mkarimu kama ni mkarimu kweli si mtoa rushwa, lakini tukisema tuharamishe ukarimu kwa sababu tumeshindwa kutofautisha takrima na rushwa, hiyo ni juu ya Bunge kuamua.

Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ameshapeleka suala la utata huu wa takrima kwa Tume ya Kurekebisha Sheria yenye viongozi wenye uwezo wa kutathimini mjadala kama ukifungwa utaletwa Bungeni. Mimi siwezi kusita. Lakini nitaendelea kuamini kwamba ukiingia kwenye uchaguzi na ukarimu, Wapigakura wanakujua kwamba wewe ulikuwa mkarimu kabla ya hapo. Lakini kama unaanza baada ya kuchukua fomu hata Wapigakura wenyewe wanaweza wakakataa takrima yako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, labda nichukue fursa hii kutoa wito kwa Wapigakura kwamba watakayemgundua analeta takrima kwa kificho cha rushwa, wasiikubali au watoe taarifa Taasisi ya Kuzuia Rushwa wamshughulikie huyo mgombea.

Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, anasema *CUF* walihonga Sh.1,000/= katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na hawajachukuliwa hatua. Sisi tutafuatilia eneo hilo kufanya uchunguzi na vile vile tutamfuata Mheshimiwa Ali Said Salum, ametuahidi kwamba ana dawa ya kupambana na rushwa. Nimeshaagiza Idara ya Itafiti, Taasisi ya Kuzuia Rushwa wamwone. Inawezekana akapata dawa ya moja kwa moja ikatuondolea kero hii mara moja. Hatuwezi kudharau ushauri wa Mbunge, tumeuchukulia *serious*. *(Makofi)*

Kuhusu rushwa ya ngono katika uchaguzi, tunashauri wahusika watoe taarifa katika Taasisi ya Kuzuia Rushwa katika maeneo yao ili iweze kuchunguzwa, kwa sababu rushwa ya ngono ni kama rushwa nyingine.

Mheshimiwa Herbert James Mntangi, amezungumzia matumizi ya fedha za MMEM uchunguzi umefikia wapi na kama tunaweza tukaboresha utekelezaji wa mpango mzima wa MMEM. Serikali inafanya uchunguzi wa fedha za MMEM zilizotolewa na Serikali wa kupitia wafadhili na kwa ajili hiyo, shughuli nzima ya ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu, vyoo na mafunzo ya Kamati, vitaangaliwa kwa kuchunguza kuona kama zilitumika vizuri na taarifa ikikamilika wananchi watajulishwa.

Aidha, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, ameshauri awepo Afisa wa kuratibu malalamiko ya Wabunge juu ya rushwa. Ni ushauri mzuri tu, tutaangalia uwezekano wa kutenga Afisa pamoja na kwamba kila Kikao cha Bunge huwa nakuja na timu nzima ya Taasisi ya Kuzuia Rushwa kuratibu mambo haya. Lakini kuwepo na Afisa wa kuratibu inaweza ikafaa vizuri zaidi akawa na Ofisi kwenye Ofisi ya Bunge. Ni ushauri mzuri.

Mheshimiwa John Singo – Mbunge wa Same Magharibi, Waraka wa Msajili wa Mahakama unajibu hoja yake kwamba kesi za ardhi hazipaswi kufanywa na Mahakama za kawaida. Hii ni kutokana na Waraka uliotoka kwa Msajili wa Mahakama ya Rufaa kwa barua yake ya tarehe 14 Machi, 2005 kwa Mahakimu wa Kazi Wafawidhi wote, Mahakimu wa Kazi Wafawidhi Tanzania Bara kwamba kwa mabadiliko ya Sheria Na. 4 na Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria Na. 2 ya mwaka 2002 ya Baraza la Ardhi na Nyumba inayoainisha miundo na mamlaka ya vyombo tajwa, yaani Mahakama ya Rufani, Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu, Baraza la Kata na Baraza la Ardhi ya Kijiji.

Tangu tarehe 1 mwezi wa Kumi, 2003 Hakimu yoyote haruhusiwi kushughulikia kesi za ardhi. Waking'ang'ania, Taasisi ya Kuzuia Rushwa itawashughulikia. Lakini tunaagiza Wakuu wa Mikoa wahakikishe Waraka huu unawafikia Mahakimu wote wa Mahakama za Mwanzo. Yawezekana wanafanya hivi kutokana na kutokuwa na Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya *TASAF*, Mheshimiwa Omar Mjaka - Mbunge wa Vitongoji, anaulizia kama maeneo ya Vitongoji na Bombani yatapatiwa msaada katika Awamu ya Pili ya *TASAF*. Ndiyo. Awamu ya Pili ya *TASAF* itaenea nchi nzima. Kwa hiyo, Vijiji vyote vitapata fursa sawa ya kuleta maombi ya miradi hii ili kupata msaada wa kuzingatia taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

Kulikuwa na suala kwamba Mgawanyo uwekwe wazi, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, mgawanyo wa fedha zote za *TASAF* Awamu ya Pili utakuwa wazi na kutangazwa kwenye Vyombo vya Habari na taarifa zitatolewa kila baada ya miezi mitatu kuhusu matumizi ya kila Halmashauri na Visiwa vya Pemba na Unguja vikiwemo. *(Makofi)*

**Mheshimiwa Herbert James Mntangi - Mbunge wa Muheza, anaulizia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* kutafuta fedha za kumalizia utekelezaji wa miradi ya Awamu ya Kwanza. Kwa mujibu wa Wataalam, kumbukumbu walizoniletea ni kwamba zinaonyesha kuwa kuna miradi 13 ambayo haijapatiwa fedha za kukamilika utekelezaji katika Halmashauri ya Muheza. Lakini fedha hizo zimewekwa kwenye Bajeti hii ya mwaka 2005/2006. Aidha, ni matarajio yetu Halmashauri ya Muheza na jamii watatoa mchango wao.**

**Maelezo ya ziada kuhusu Mfuko wa Taifa wa Kijiji utakavyofanya kazi, taratibu zitafanywa kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge ili ngazi zote za utekelezaji ziweze kuelewa taratibu.**

Kuhusu kupunguza mchango asilimia 20 kutoka kwa wananchi, uzoefu kutoka Awamu ya Kwanza kwa mujibu wa wataalam umeonyesha kwamba kiasi hicho kinawezekana kwa sababu kinajumuisha nguvu kazi, vifaa vinavyopatikana katika eneo husika na fedha taslimu. Siyo lazima iwe fedha taslimu, ni fedha taslimu na nguvu kazi na vifaa katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Aridi Uledi – Mbunge wa Nanyumbu aliuliza kuhusu Mfuko wa Maendeleo *(TASAF)*, Miradi ya barabara ambayo haikukamilika. Kulingana na mikataba

ya utekelezaji katika barabara hizo kati ya *TASAF* na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, *TASAF* ilishatoa fedha zote kwa Halmashauri hii na ni matarajio kwamba Halmashauri itakamilisha miradi hiyo.

Kutokamilika kwa Mradi wa Maji wa Ndwika/Mangaka kwa kuishiwa mabomba, maelezo ni kwamba makisio ya awali hayakukidhi mahitaji. Hivyo jamii imeshauriwa kutuma maombi katika Awamu ya Pili ya *TASAF*. Tunatoa ushauri kwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuisaidia jamii hiyo, kuandaa makisio sahihi.

Kuhusu mabwawa ambayo hayakupatiwa fedha, Halmashauri ilileta maombi kwa ajili ya mabwawa sita na yote yalifanyiwa *survey.* Kulingana na fedha zilizokuwa zimebaki kwenye mgao wa Halmashauri iliwezekana kutoa fedha kwa mabwawa mawili tu.

Mheshimiwa wa mwisho ni Mheshimiwa Frank Maghoba wa Kigamboni ambaye ametoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kupeleka mpango wa *TASAF* katika Wilaya ya Temeke. Tunazipokea pongezi hizo na tutafikishia Mheshimiwa Rais. Lakini Mheshimiwa Maghoba anashauri itolewe elimu kwa jamii kuwezesha kununua vifaa bora. Tunakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge na tunashuri Manispaa ya Temeke kuziwezesha jamii kuzielimisha kuhusu ununuzi wa vifaa vyenye ubora unaokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini nimeweza kujibu hoja zilizofika kwetu, kama zitakuwa zina mapungufu tutaongeza maelezo kwa ruksa yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwako na kupitia kwako kumfikia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano walionipatia mimi na Ofisi yetu muda wote nilipokuwa nawasiliana nanyi kama Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora. Maana yake yawezekana nisirudi hapa. Lakini huko kuna uhakika karibu asilimia 99. *(Makofi)*

Aidha, namshukuru Mwenyekiti mwenzako wa Bunge kwa kazi nzuri aliyofanya na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote pia wa Upinzani wakiwemo kwa ushirikiano mlionipatia kama Mbunge mwenzenu na Waziri na nikaweza kufanya kazi ambayo ninaweza kusema kwa kadri ya uwezo wangu nimeifanya. Nawaombea nyote afya nzuri na mafaniko makubwa katika mapambano yaliyoko mbele yetu kuanzia mwezi kesho Julai au mwezi wa nane. *(Makofi)*

Pia, naishukuru Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ushirikiano walionipatia nilipokuwa nafika mbele ya Kamati hiyo kwa dhamana ya kuwakilisha Ofisi ya Rais katika Kamati hiyo. Naishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, pia imenipa ushirikiano mkubwa sana nilipokuwa nafika pale kwa dhamana ya Uwaziri.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, huwa hapendi kupewa shukrani, lakini kwa sababu hayuko hapa atazisikia. Namshukuru kweli kweli kwa kunichagua kuwa Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Rais, mara mbili kukaa katika Ofisi yake Ikulu kumsaidia katika masuala ambayo aliamua ayasimamie mwenyewe masuala ya Utawala Bora.

Namshukuru Makamu wa Rais, naye amenipa ushirikiano nzuri ndani ya Ikulu. Namshukuru Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Ma-Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu Ikulu, Watumishi wote wa Ikulu, kwa kweli nilipoingia Ikulu mle nilikuwa naingia mara ya kwanza… *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Uliogopa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Niliingia kwa woga, lakini waliniondoa woga kwa sababu Rais ni mwema, familia ni wema na watumishi niliowakuta Ikulu wote ni wema. Tulikuwa tunaishi kama *family* na nilipoteuliwa mara ya pili kurudi mle nilifurahi sana kwa sababu nilijua sitahitajika kwenda Wizara nyingine kujifunza tabia za watu wengine. *(Makofi)*

Nimeendelea kushirikiana nao vizuri sana na nitaendelea kuwa nao Mungu akipenda miezi minne iliyobaki, mniombee nisifukuzwe mpaka mwezi wa Kumi. *(Makofi)*

Namshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Mzee Abson na timu nzima. Huwa mnasema hawaonekani hapa, lakini wanafanya kazi nzuri kwa kutoonekana huko. Mambo yanakwenda vizuri na nchi yetu ni salama na tulivu. *(Makofi)*

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa na watumishi wote wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa wamenipa ushirikiano nzuri sana. Kamishna wa Maadili ya Viongozi wa Umma, Mzee Jaji William Maina na watumishi wote Idara ya Viongozi, Idara ya Sekretarieti ya Viongozi wa Umma, kwa kweli hawa Wazee bahati nzuri mimi nafanya kazi na wazee pale, lakini ujana wangu haukuingiliana na mahusiano ya kazi. Nawapa shikamoo zangu, kazi tunakwenda barabara na hatujagongana miaka yote minane hii na ni marafiki zangu kweli na ni watumishi wazuri, hodari na nyinyi mmetoa sifa kwa sababu kuna timu kiboko huko kama Waziri alivyoeleza. Inachapa kazi kweli kweli, sisi tunakuja hapa Makamisaa wa Siasa kueleza maneno kwa furaha kwa sababu kazi nzuri inafanywa na wenyewe katika *field.*

Shukrani kwa Vyombo vya Habari. Vyombo vya Habari havikuandika sana safari hii, jamani mmenisikiliza. Mambo yangu hayatoki! Angalau yatoke haya! Maana yake mimi nikitoka kwenye gazeti ni kashfa tu. Nikitoka kwenye gazeti ni kashfa tu. Angalau zitoke hizi shukrani kwamba nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Vyombo vya Habari kwa sababu bila Utawala Bora, uhuru wa Vyombo vya Habari usingekuwepo na wale wanaokiuka uhuru wa Vyombo vya Habari, tunajua namna ya kuwashughulikia. *(Makofi)*

Hawa ni wazuri walioko huku na wengi kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Ni wachache tu wanaochafua heshima ya Vyombo vya Habari. Shukrani kwa Wapigakura

Jimbo la Muleba Kusini, kwa kuniwezesha kuwa Mbunge mara kadhaa. Lakini kwa kuridhisha Wapinzani wangu wa kisiasa kukimbilia Dar es Salaam kwenye magazeti ya Rai na Tazama.

Napenda kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, kama nilivyowahutubia tarehe 19 mwezi huu wa Juni kwamba hao wakimbizi wa kisiasa waliokimbilia Dar es Salaam nimeshawazingira na nitawashughulikia. Hawatapata fursa ya kurudi huko Muleba kwa kutumia Sheria. Zitawazingira na Polisi na Vyombo vya Dola. Watazingirwa na Watalaam wangu wa Sheria. Nimeshawapa maagizo, wawashughulikie kupitia Mahakama. Hiyo sio siri. Nimewaambia waombe radhi, hawakuomba, kwa hiyo sio waungwana. Sasa watakayowapata hawatanilaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa mke wangu, Marystela na watoto wangu Nelson Mutalemwa na Yustina Kemilembe kwa kunivumilia muda wote ambapo nimekuwa nakaa na Mheshimiwa Sarungi , Mbunge wa Rorya, hapa ananisumbua.

Huyu ni mjukuu wetu, lakini Mzee Sarungi naye namshukuru sana. Ni mshauri wangu wa karibu. Nipigie makofi basi!! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Naunga mkono hoja yetu, ni yetu kwa pamoja. Tunaomba fedha ili kusudi Awamu ya Nne iweze kuchapa kazi kwa misingi iliyowekwa vizuri na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na sisi tukimsaidia kwa pamoja ndani ya Ukumbi huu. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa tena nafasi hii jioni ili niweze kuhitimisha hoja yetu ambayo niliwasilisha leo asubuhi kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, napenda tena kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu, inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kutekeleza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka wa 2000. *(Makofi)*

Mafanikio haya ni matokeo ya kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau na wananchi wake. Namshukuru sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kama alivyosema Mheshimiwa Wilson Masilingi, kuniteuwa na mimi kuwa kwenye Ofisi yake kuwa mmoja wa Mawaziri ambao walikuwa wanamsaidia. Pia, namshukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika mafanikio haya ya Serikali ambayo mmeyakiri nyie leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yanatokana na Utawala wa Serikali inayoendeshwa kwa misingi ya Katiba, Sheria na utaratibu mzuri hazina ya busara,

uzoefu na uwajibikaji wa pamoja wa Serikali. Matokeo dhahiri ya utawala huo ni kuendelea kuwepo na amani na utulivu katika nchi ambayo ni mazingira muafaka kama nilivyosema asubuhi ya kutoa huduma bora za jamii na kuendesha uchumi kwa njia ya kisasa ili kuongeza kasi ya wananchi kutokomeza umaskini na majanga kama UKIMWI, njaa na mengineyo pamoja na matatizo ya rushwa, ubadhirifu na uzembe.

Hayo yote yamewezekana kwa kuwa Serikali hiyo inatokana na Chama chenye Taasisi imara, muundo mzuri na sera zinazotekelezeka na kusheheni Viongozi wenye uzoefu na utaalam na si Chama kingine isipokuwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Waziri Wilson Masilingi kwa ushirikiano mzuri ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Aidha, napenda nimpongeze kwa kutoa ufafanuzi mzuri jioni hii ya leo kwa hoja ya Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yake na mengine ya kwangu vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe na hasa nafurahi leo wewe ni Mwenyekiti hapa kwa sababu tumeongozana wanawake. Wewe, mimi, Jenista Mhagama na Grace Kiwelu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha jinsi jamii ya Watanzania sasa inavyowaamini na kukubali kwamba wanawake wanaweza kuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti Eliachim Simpasa kwa kutuongoza vyema katika Kikao chote cha Bajeti na kwa muda wote wa uhai wa Bunge hili. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao endelevu ambayo imesaidia sana kuboresha utendaji wetu na hasa utendaji wangu. Ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge hauishii katika hii kazi ya Uwaziri tu, bali hata katika matatizo na furaha zetu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti Athumani Janguo na Makamu Mwenyekiti George Lubeleje na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na maelekezo yao ambayo yametuwezesha kufika hapa tulipo leo. Ningependa kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama sana kwa kuwasilisha maoni yake ya Kamati kwa ufasaha mkubwa. Nimefurahi sana kwa sababu Jenista Mhagama amekuwa akinichukua kama dada yake na mimi siku zote tumekuwa tukishirikiana naye kwa mambo mengi ya kuimarisha Bunge la Jamhuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kumshuru sana mdogo wangu Grace Kiwelu ambaye amenipongeza na amepongeza Ofisi ya Rais kwa ujumla. Hakuunga mkono hoja, lakini pongezi maana yake ni kuunga mkono. Vilevile, alipotembelea Wilaya ya Hanang na Mkoa wa Manyara aliwaeleza wananchi wetu kwamba yeye ni Dr. Mary Nagu wa CHADEMA. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi namshukuru sana kunichagua kuwa *long modal* wake, naomba uendelee hivyo na mimi nitakuwa nachukua yako mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru kwa dhati Wabunge wote ambao wamechangia katika hoja hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora. Napenda kuwahakikishia kwamba mapendekezo na ushauri na maelekezo tutayazingatia kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kusema na wengine ambao wamechangia kwa maandishi. Aidha, kuna wengine ambao walichangia wakati wa kujadili hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwataje wote waliochangia. Hawa ni wale waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista Mhagama - kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Grace Kiwelu - kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Aggrey Mwanri - Mbunge wa Siha, Mheshimiwa Herbert James Mntangi - Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Omar Chubi - Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali - Mbunge wa Vitongoji, Mheshimiwa Esha Stima - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa William Shellukindo - Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Beatus Magayane - Mbunge wa Buyungu na Mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri - Mbunge wa Kuteuliwa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa John E. Singo - Mbunge wa Same Magharibi, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri - Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga – Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Aridi Uledi - Mbunge wa Nanyumbu, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa George M. Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa na Mheshimiwa Mark Mwandosya - Mbunge wa Rungwe Mashariki. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kusema ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo - Mbunge wa Moshi Mjini, Mheshimiwa Ali Said Juma - Mbunge wa Kojani, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha - Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Hamisi Nguli - Mbunge wa Singida Mjini, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama - Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Frank Maghoba - Mbunge wa Kigamboni. *(Makofi)*

Waliochangia katika Wizara zilizotangulia ni Mheshimiwa George Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Willfred Lwakatare - Mbunge wa Bukoba Mjini, Mheshimiwa Maria Watondoha - Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo – Mbunge wa Tabora Mjini na Mheshimiwa Emmanuel Kipole - Mbunge wa Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi zimetolewa na ninapenda kuwahakikishia tena Wabunge kwamba, kwa kushirikiana na Waziri mwenzangu, mwisho tutakuwa tumetoa maelezo kwa kadri inavyowezekana na kwa hiyo, wakati wa mafungu hatutakuwa na wengi watakaosimama. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja za Wabunge. Hoja ya kwanza ilikuwa inahusu mishahara ya Watumishi na kwa kweli mishahara ni haki ya Watumishi. Kwa hiyo, kuona Wabunge wengi wamesimama kuwatetea ni kwamba wanaona umuhimu wa Watumishi wa Umma na kwa hiyo, umuhimu wa kuwapa ujira unastahili.

Waliochangia katika hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Salum**,** Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha na Mheshimiwa Mzee Philemon Ndesamburo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya Watumishi wa Umma hutegemea hali ya uchumi wa nchi. Nyongeza yoyote katika mishahara haina budi kuwiana na kukua kwa uchumi na mapato ya Serikali. Aidha, Serikali imetunga Sheria ya majadiliano ya pamoja katika utumishi wa Umma Na.19 ya mwaka 2003, ambayo inatoa fursa ya kufanyika kwa majadiliano kuhusu utaratibu wa malipo ya mishahara kati ya mwajiri na mfanyakazi kupitia Vyama vyao vya Wafanyakazi. Linalofanyika katika majadiliano ni kuangalia na kukubaliana kuhusu mgawanyo wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya mishahara baina ya makundi mbalimbali ya Utumishi wa Umma.

Hivyo viwango vinavyolipwa kwa makundi yote wakiwemo Madaktari, Walimu, Wahandisi, Wanasheria na wengine, vimetokana na makubaliano katika majadiliano hayo. Inapotokea kundi lolote kutoridhika na utaratibu huu wa majadiliano kwa pande zote mbili, yaani Serikali kama mwajiri na watumishi, basi tunaendelea na majadiliano mpaka pale tunapoelewana. Nataka kurudia kusema kwamba mapato ya Serikali ndio yanayopelekea mishahara kuwa mizuri au kuwa duni. Mapato ya Serikali yakiwa mazuri na mishahara nayo inakuwa mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwa ufupi kusema, toka mwaka wa 2003 kwa kiasi gani mishahara ya Walimu imepanda. Mwaka 2002/2003 mshahara wa Mwalimu aliyetoka Chuo Kikuu ulikuwa 81,950 na mwaka uliofuata 2003/2004 ulikuwa ni 99,090. Mwaka 2004/2005 ukafika 140,000 utaona kwamba nia ya Serikali ya kutambua umuhimu wa kazi ya Walimu inaonesha kwa kadri ambavyo imekuwa ikiongeza mishahara ya Walimu.

Ninajua bado mishahara ni midogo, lakini sio tu kwa Walimu, bali kwa watumishi wote wa Watanzania na njia pekee ya kuongeza mishahara ni kwa sisi watumishi wa umma kuongeza tija na ufanisi ili kuongeza mapato ya Serikali ili Serikali ipate fursa ya kuongeza mishahara ya watumishi wake wakiwemo Walimu. Ninapenda kusema kwamba wakati Walimu ni asilimia 49 ya Watumishi wote wa Serikali au wa Umma mshahara uliotengwa kwa Walimu ni asilimia 54 na kwa hiyo, utaona jinsi Serikali inavyotoa umuhimu mkubwa kwa hii kazi ambayo ni uhai wa nchi yetu kwa sababu elimu ndiyo uhai wa nchi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Madaktari mwaka wa 2002/2003, Daktari aliyehitimu Chuo Kikuu alipata Sh.118,720/=, mwaka uliofuata wa 2003/2004, Daktari aliyetoka Chuoni Kikuu alilipwa Sh.139,380/=. Ni kama nyongeza ya asilimia 20. Mwaka uliofuata wa 2004/2005 Madaktari waliongezewa mshahara kufikia Sh. 201,650/= nyongeza ya takribani asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona kwamba na kazi ya Udaktari inathaminiwa sana hata tukizingatia kwamba ukitaka wananchi wenye afya lazima uangalie afya na si wengine wanaoangalia afya zao isipokuwa Madaktari. Kwa nia hiyo hiyo, Serikali mwaka huu 2005 itaangalia kwa namna ya pekee namna ya kuongeza mishahara ya wataalam wakiwemo Madaktari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaomba watumishi wa Serikali kwamba Serikali inajitahidi sana kuangalia maslahi ya watumishi wake. Lakini namna pekee ya Serikali kuongeza mishahara ni pale ambapo mapato yanaongezeka na si kwa ajili ya kuomba kutoka nje, bali kuongeza tija na ufanisi wa kufanya kazi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye hoja ya pili ambayo ni tathmini ya kazi. Dhana ya tathmini ya kazi ni kuweka vigezo vya kisayansi katika kuweka ngazi za mishahara kwa taaluma mbalimbali katika utumishi wa Umma. Zoezi hili ambalo lilikamilika mwaka 2003 limesaidia sana kuboresha mfumo wa mishahara katika Utumishi wa Umma. Hata hivyo katika utekelezaji wake yametokea matatizo hususan kwa waatumishi waliocheleweshwa kupandishwa vyeo.

Serikali imelitambua tatizo hili na waajiri wote wameagizwa kwa Waraka wa Katibu Mkuu wa Utumishi wa tarehe 10/03/2005 kufanya uchambuzi kuhusu idadi ya watumishi waliocheleweshwa kupandishwa vyeo na kuainisha gharama za kurekebisha dosari hiyo ili tatizo hilo lipatiwe ufumbuzi. Mpaka sasa kuna waajiri wachache walioleta, ninaomba wale waliobaki wafanye hima walete uchambuzi ili hatua stahili zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kwa Serikali na kwa Chama Tawala kama nitaachia maneno yaliyosemwa na Upinzani, kwa mfano mishahara na ajira Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana sana na Wasemaji wa Upinzani kwamba tumekubali wote Upinzani uwepo na sisi wa Chama Tawala tunatazama Wapinzani kama kioo. Asubuhi ukitoka nyumbani ni lazima ujitazame kwenye kioo ili uone uso wako hauna masizi au uchafu mwingine. Kwa hiyo, Upinzani wanatusaidia kuibuka lakini ninakubaliana na ninawapongeza pale wanapotupongeza tunapostahili kupongezwa. Lakini pale ambapo wanatulaumu bila sababu ili wajenge hoja ya wao kuonekana wa maana, Serikali nayo itachachamaa kujenga hoja. Kwa hiyo, siamini kwamba Upinzani watachukua hoja ya mishahara ya Madaktari kuifanya ya kwao wakati nimeonyesha juhudi ya Serikali ya Miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini na ninakubaliana na wananchi wote kwamba Madaktari wa Watanzania wamejitolea na kwamba wataendelea kujitolea, kwa sababu ni wananchi wenzetu, wanajua umaskini wa Watanzania, wakati huo huo, Serikali ikiwapa tuzo kwa ajili ya mshahara kila inapowezekana kuwaongezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi wanaojiendeleza na kupandishwa vyeo bila kupewa nyongeza ya mishahara, Waajiri wote wameagizwa kwa Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 2004, kuhakikisha kwamba watumishi wote wanaomaliza mafunzo ya kujiendeleza wanapewa vyeo wanavyostahili kulingana na miundo ya Utumishi na mishahara yao kurekebishwa pindi wanapopata sifa zinazostahili. Kwa sasa watumishi wanaruhusiwa kulalamika pale ambapo hawakutendewa haki. Kwa hiyo, wasisite pale Waajiri wanapoacha kuwafanyia wanavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha utekelezaji wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002 imetoa madaraka ya kuajiri kwa Waajiri, kupandishwa vyeo, kuwapeleka mafunzoni watumishi na pia kuweka kumbukumbu zao katika *computer* mahali walipo na inategemea kumaliza tatizo hili. Kwa hiyo, uimarishaji na usahihi wa kumbukumbu utasaidia kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tofauti kubwa ya mishahara katika Halmashauri, Serikali imebaini tofauti kubwa ya mishahara kati ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara na imechukua hatua ya kutenga fedha ili kushughulikia tatizo hili katika mwaka huu wa fedha 2005/2006. Aidha, Ofisi yangu itafanya zoezi la tathmini ya kazi kwa ngazi ya Serikali za Mitaa ili viwango vya mishahara viwe na uwiano mzuri kati ya watumishi wa Serikali Kuu na wale wa Serikali za Mitaa na ndani ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara ya Watendaji wa Vijijini na Kata, Waziri wa Fedha na Waziri wa TAMISEMI walitoa majibu na mimi napenda kuungana nao kuendelea kueleza kuwa hao wamelipwa na wanaendelea kulipwa kupitia TAMISEMI na Halmashauri za Serikali za Mitaa zinazohusika na kama bado kuna matatizo tunaendelea kuyatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malimbikizo ya mishahara ya Watumishi wengine, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kuunda Tume iliyobaini madai ya Walimu na ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Omar Kwaangw’ na wale Wabunge waliobaini madai ya Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo hayo yanafanyika kwa watumishi wote, hadi tarehe 30/06/2005 takriban Shilingi bilioni 18 zilikuwa zimetumika kulipia malimbikizo ya watumishi wengine. Aidha, uhakiki wa malimbikizo yaliyobaki unaendelea kufanyika mara kwa mara na baada ya kukamilika malipo yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ilikuwa inahusu Ajira ndani ya Serikali. Waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Ruth Msafiri,

Mehimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Salum, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Frank Maghoba na Mheshimiwa Mwanri.

Hoja ya kwanza ilikuwa kuadimika kwa kada ya Matabibu. Serikali ilikwishatoa mwongozo kuwa mkakati uliotumika kuwapata Walimu nao vilevile utatumika kuwapata Matabibu kuanzia Julai Mosi mwaka huu 2005. Kwa hiyo, ndani ya Sekta ya Afya vilevile tutaangalia ni namna gani tutapunguza matatizo ya kutokuwa na Matabibu na Madaktari. Lakini ni kweli kwamba watumishi ndani ya Sekta ya Afya ni wachache hasa Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daktari wa Tanzania anatibu wagonjwa wengi sana na njia pekee ya kuondoa tatizo hili ni kuongeza watakaohitimu ili waende kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati. Hatuna njia ya mkato. Kwa hiyo, sina jibu ambalo nitalitoa la kuwaridhisha lakini Serikali inafanya kila linalowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge waliosema kiwango cha mshahara kima cha chini ni mdogo sana. Kama nilivyoeleza mishahara ya Serikali inatokana na mapato ya Serikali na ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, viwango vya mishahara yetu vinatokana na kiwango vya uchumi ndani ya nchi na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi kukataa kwenda kufanya kazi Mikoa ya pembezoni, Mtumishi kama binadamu mwingine yeyote hupenda kufanya kazi katika mazingira yenye kumrahishia maisha. Hivyo ni jukumu letu sote kuboresha mazingira ikiwa ni pamoja na urahisi wa mawasiliano, makazi bora na upatikanaji wa mahitaji muhimu katika sehemu zinazohusika ili kuwavutia watumishi kufanya kazi katika Mikoa ya pembezoni.

Waajiri washirikiane na jamii katika kujenga mazingira bora maeneo ya kazi ili kurahisisha upatikanaji wa watumishi. Ofisi yangu itatoa mwongozo kuhusu vivutio katika sehemu ambazo hazivutii watumishi kutokana na mazingira magumu kwa upande wa Serikali. Pia, Serikali kila inapopata uwezo inafanya hivyo kwa kutilia maanani kuwa mikoa bado haina teknolojia wala nyenzo za kusimamia udhibiti wa ajira inaonekana ni vyema vibali vya ajira viendelee kutolewa na Ofisi ya Rais Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Waraka Na.1 ya mwaka 1992 na Waraka wa mwaka 1994, Utumishi itaendelea kutoa vibali. Hata hivyo, Utumishi imeondoa vibali katika Sekta ya Afya na Elimu, lakini Waajiri wanapaswa kuhakikisha kwamba ikama zipo na vilevile bajeti ya kuwalipa hao watakaowaajiri ipo ama sivyo Serikali itapata malalamiko makubwa.

Kuhusu watumishi wa Serikali ambao wameishia Darasa la Saba wakiwemo madereva walioajiriwa kabla ya Sera mpya kuanza kutumika, suala hilo linafanyiwa kazi na tumesema kwamba wale ambao wako kwenye umri ambao wanasoma, wasome. Sababu kubwa ni kwamba wananchi wa Tanzania wanataka huduma bora na huduma bora inatokana na uwezo wa uzoefu na utaalam. Kwa hiyo, kwa wale ambao umri wao

umepiga hatua, tutawaangalia. Lakini vilevile suala la elimu ni muhimu na ninawaasa Watumishi wa Umma wajihangaishe wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza tija ndani ya Serikali, namna ya kuongeza tija ndani ya Serikali ninakubaliana na Mheshimiwa Frank Maghoba ni kuongeza bidii na kuheshimu saa za kazi. Lakini vilevile ilionekana uwajibikaji umekuwa mdogo sana ndani ya Utumishi wa Umma na kwa hiyo, kupitia Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 Serikali imeongeza uwajibikaji kwa wale wasimamizi wa kazi ili kupanga malengo na kuona kwamba malengo hayo yanatekelezwa na sasa tumeondokana na kuangalia ni namna gani Mtumishi wa Umma anafanya kazi peke yeke.

Vile vile, tutaangalia na matokeo ya kazi yake. Kama ni Bwana Shamba ameweza kuwaangalia wakulima wangapi, kwa hiyo, ataonyesha mavuno yameongezeka kiasi gani. Kama ni Daktari ameongeza bidii kuangalia wagonjwa, tutaangalia vifo vimepungua kiasi gani. Tukifikia hatua hiyo, nina hakika Utumishi wa Umma utakuwa umejitahidi katika kuongeza tija na ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya raslimali, Watumishi wengi wa Serikali wameonyesha uwezo mdogo wa utendaji kazi kwa sababu hawapewi mafunzo ya kutosha.

Ofisi yangu imetoa mwongozo kwamba kila Mwajiri lazima awe amebainisha maeneo ambayo yanataka mafunzo na kuweka bajeti ya mafunzo hayo. Tukifanya hivyo, nina hakika tutakuwa tumeongeza uwezo wa Watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maadili ya watumishi, ni kweli haitoshi tu kuwa mfanyakazi hodari. Mtumishi wa Umma lazima aonyeshe kwa maadili yake kwamba ni Mtumishi wa Umma. Kwa hiyo, tabia za ulevi, uzembe, ubadhirifu na mengineyo yote yasiyoendana na utamaduni wa Utumishi wa Umma hayatavumiliwa na maadili ya Utumishi wa Umma, yamekuwa sehemu ya Sheria au sehemu ya Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi walilalamikia usumbufu wa ulipaji wa mafao kwa wale waliostaafu. Kwa wale wanaostaafu, sasa hivi hakuna usumbufu kwa sababu kumbukumbu zimewekwa vizuri. Kwa wale ambao wamestaafu awali kuna usumbufu kwa sababu kumbukumbu haziko vizuri na tumeona ni vizuri pengine badala ya Hazina kuendelea kuwalipa mafao wastaafu hao, Kitengo kile kihamishiwe kwenye Kitengo cha Pensheni ya Watumishi wa Umma ili kadri walivyoweza kuboresha malipo ya sasa wajaribu kuona watatumia ubunifu gani ili kuboresha malipo ya wale waliostaafu awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI ni janga la Taifa na kwa vyovyote vile sisi kama Wabunge, Watumishi wa Umma na Viongozi lazima wote tuongeze elimu na njia mbalimbali za ubunifu za kutokomeza ugonjwa wa UKIMWI. Mheshimiwa Waziri wa Afya amesema vya kutosha, kwa hiyo na mimi naomba nisichukue muda mrefu. Vilevile,

napenda kuwapongeza na kuwashukuru sana wanawake wa Mikoa ya Arusha na Manyara kwa upendo na ushirikiano wao. *(Makofi)*

Uwakilishi wangu Bungeni kwa takribani miaka kumi, nimeingia Bungeni kwa kura zao nyingi, nimepata uzoefu kutoka kwao, ninawashukuru na Mungu awaongezee maisha marefu. Nina hakika nitaendelea kushirikiana nao na kwa muda huu unaokuja, nitajaribu kwenda Jimboni. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaji walionipa ni uzoefu, nina hakika utanipitisha katika Jimbo la Hanang. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa Mbunge wetu kwa miaka 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sumaye amekuwa Mbunge mahiri, amekuwa Waziri Mkuu hodari na amekuwa kiongozi wetu kwa muda mrefu na kwa hiyo, Mungu akinijalia nikipata Jimbo lile nina hakika nitakuta mazingira mazuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika mfululizo wa shukrani hizi, napenda niishukuru familia yangu akiwemo mume wangu, Profesa Joseph Nagu, haonekani mara nyingi, anafundisha Mzumbe, ameruhusu Mheshimiwa Mbunge kusema sauti yangu nzuri na ameruhusu vile vile Mheshimiwa N'hunga kila siku ananiambia niendelee kujibu maswali kwa sababu anapenda sauti yangu na ameniamini na kuniruhusu kujadiliana na ninyi mambo mengi bila kuwa na wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana majirani, ndugu na marafiki. Kuna wakati nilivyokuja mara ya kwanza Bungeni, mtoto wangu alikuwa na miaka miwili na nusu alipougua wakati sipo, ni majirani ndio walionisaidia. Kwa hiyo, nao nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Hanang, nina hakika hawataniangusha pindi nitakapokwenda kuomba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena sana na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na ninaomba mtuunge mkono kwa kutupa ruksa ya kutumia fedha hizi ili tuboreshe zaidi utumishi wa Umma na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtatambua kwamba hoja hii ina mafungu mengi sana, kama mlivyoona kwenye hotuba yake. Kwa hiyo, wale wanaopenda kuuliza watumie muda zaidi kwenye *vote* ya mshahara wa Waziri kuliko kwenda kwa Ofisi ya Rais, sijui wapi huko. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu, tuanze!

FUNGU 32 – Ofisi ya Rais Menejimenti ya
Utumishi wa Umma

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … ... Sh.3,808,488,200/=

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Programme* 10, *Administration*, S*ub-vote* 1001, *Administration and General*, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumthibitishia dada yangu Dr. Mary Nagu kwamba sina nia kabisa ya kuzuia mshahara wake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kupata ufafanuzi kwa mambo machache ambayo ningependa ndugu zetu walioko nje waweze kujua nini kinaendelea katika masuala yao.

Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi kwa Madaktari na Walimu, lakini pia wako wafanyakazi wengine kutoka Idara nyingine na wapo pia wafanyakazi waliopandishwa vyeo kuanzia Julai, 2004, lakini wamethibitishwa vyeo vyao mwaka huu 2005. Pamoja na kuthibitishwa kwenye vyeo hivyo bado hawajaweza kupewa ule mshahara wao mpaka sasa. Ningependa Mheshimiwa Waziri awaeleze watu hawa ni lini watalipwa *arrears* zao? Pia, wapo wengine ambao wamepandishwa vyeo lakini bado hawajapata barua zao za kuwathibitisha kwenye vyeo hivyo. Je, ni lini watathibitishwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Grace Kiwelu kwa kutaka ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mfano wa mishahara ya Walimu na Madaktari kama mfano tu kuonyesha kwamba na watumishi wengine nao wamefanyiwa vivyo hivyo kwa viwango tofauti. Kwa hiyo, ndani ya utumishi wa umma, hatuwabagui wengine wote tunawaona ni watoto wa mama mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wale waliopandishwa vyeo na kuthibitishwa bila kulipwa, napenda kusema kwamba mshahara ni haki ya mtumishi na kwa hiyo, wale ambao wamepandishwa vyeo na kuthibitishwa na hawakulipwa, sio rahisi sasa hivi kutoa jibu kwa sababu sijui ni mwajiri gani ambaye amepandisha vyeo na kutokulipa. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha Waajiri wote wale ambao wamepandisha vyeo watumishi na kuwathibitisha wawalipe na wale ambao wamewapandisha vyeo bila kuwathibitisha na wanastahili kuthibitishwa, basi wathibitishwe. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mimi napenda kufahamu kwenye mchango wangu kwa njia ya maandishi nilisema kwamba kauli ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kwamba wastaafu watakuwa wameongezewa posho kabla hajaondoka kwenye madaraka yake. Sasa hivi ni Sh.20,500/= anayoipata mstaafu aliyelitumikia Taifa hili, nalo linasemaje kwa sababu lazima tukumbuke kwamba ile ni kauli ya Mkuu wa Nchi alisema kwamba atakuwa amewaongezea angalau kima cha chini cha kwao kiwe kimepanda kutoka pale kilipo. Sasa sijui, maana nimetazama na huko nje wako wale wastaafu waliotumikia Taifa hili kwa muda mrefu, sasa tunawaacha na wao solemba na hii Sh.20,500/= kwa mwezi? Naomba majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mayonga ataniwia radhi kama sikujibu hoja yake kwa ufasaha kama alivyotegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba wakati nikitoa hotuba na sasa hivi nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge sijasema kima cha chini kitakuwa kiasi gani, sijasema mshahara wa wataalam au watumishi wengine utakuwa kiasi gani kwa sababu mipangilio hiyo itafuata baada ya bajeti kupitishwa na Bunge na wastaafu nao wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kima cha chini kilichokuwa kinalipwa wastaafu kilikuwa chini sana tukakifikisha Sh.20,000/= na tutafanya hivyo kila uwezo wa Serikali unapokuwepo na nina hakika mwaka huu nao tutaona tutakachoweza kufanya. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi ninataka kuhoji tu kidogo juu ya *Programme* ya 10, *Sub-vote* 1001, kifungu 250100, sina nia ya kusema matatizo lakini nitakuwa sijatimiza wajibu kama mstaafu kama sikuwasemea wastaafu wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 25 cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kuna uboreshaji wa kumbukumbu za watumishi. Hapa nataka nipate maelezo ya aina mbili. Kumbukumbu hizi zilizoboreshwa zitawahusu watumishi wanaoendelea hivi sasa au zimeboreshwa na za akina Kahumbi huku nyuma? Hilo moja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, juzi tu lilijibiwa swali hapa likitoa idadi ya wastaafu ambao hawajalipwa mafao yao kwa sababu ya upungufu wa nyaraka, tangu Wakoloni walituachia utaratibu wa kutunza kumbukumbu kwenye majalada binafsi. Ofisi huwa na majalada binafsi na Ofisi haihami, bali mtumishi anahama. Kwa hiyo, mtumishi anaweza akapoteza kumbukumbu katika harakati za kutoka hapa kwenda mahali pengine lakini Serikali na Ofisi haihamii.

Sasa nyaraka hizi zinapopungua, kwa nini analaumiwa mtumishi ambaye anahama, isilaumiwe Ofisi ambayo inakuwa na kumbukumbu toka barua ya kuajiriwa hata ile barua ya kwamba anastaafu inawekwa humo? Anapopoteza, kwa nini anapata adhabu mstaafu kama idadi iliyosemwa juzi hapa kwamba hawajalipwa kwa sababu

nyaraka zimepungua? Ningeomba nipate maelezo. Baada ya hapo, sina maneno mengi zaidi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na tatizo la kumbukumbu nzuri za watumishi na ucheleweshwaji wa malipo ya pensheni kwa wastaafu kabla ya mwaka 1999. Chini ya mfumo mpya wa kulipia pensheni, tatizo hilo halipo. Kwa hiyo kwa wastaafu wa siku za karibuni na watakaostaafu, hatuna tatizo nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lipo kwa wale waliostaafu zamani. Kwa hiyo, hatua zimepangwa na Serikali kuhamisha Kitengo cha Pensheni na Fedha kwenda *Public Service Pension Fund* ili kuondoa tatizo la watumishi wasio na kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Ofisi nyingi za Serikali kama sio zote, zina *Registry* na ni kweli kwamba watumishi wanapewa barua ya kuajiriwa ama ya nyongeza na vile vile ya *promotion*. Wale walio watumishi wengi watajua kwamba *original letters* zinazotolewa zinapewa mtumishi na kwa hiyo, kwa wale watunza fedha na Mdhibiti, kwa kawaida malipo yao wanataka kuyalipia kwa *original letters*.

Kwa hiyo, ninaomba watumishi bado waone umuhimu wa kubaki na nyaraka zao lakini wakati huo huo ninasema Serikali nayo ina jukumu la kuona kumbukumbu zinatunzwa na hatua zimekwishachukuliwa. Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Mzee Kahumbi na niwape pole kwa adha walizopata wastaafu, lakini Serikali inachukua hatua ya kuboresha pamoja na kwamba kwa muda kidogo pengine adha zitaendelea, lakini nategemea kwamba zitakwisha baada ya kuhamishia Kitengo hiki katika *Public Service Pension Fund* (Mfuko wa Pensheni).

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kifungu hicho hicho cha 32, *Programme* ya 10, *Subvote* 1001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, juzi tu wakati anatoa majibu ya nyongeza alisema wajibu wa kutunza kumbukumbu za mwajiriwa ni za mwajiri, lakini Serikali ilikuwa imetoa majibu kwamba watu zaidi ya 1000 hawajalipwa mafao kwa sababu hakuna kumbukumbu zilizokamilika. Swali langu ni dogo tu, hawa watu 1,043 ambao Serikali inatambua kwamba waliitumikia mpaka wakastaafu, watafanya nini ili wapate malipo yao? Ni swali langu hilo dogo. Je watalipwa? Kama watalipwa, watalipwa lini? Kwa sababu ni muda mrefu tangu wamezungushwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona suala la kumbukumbu za wastaafu ni jambo muhimu sana hasa ukizingatia ni Wabunge wengi wanazungumzia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena tamko langu kwamba Serikali ina wajibu wa kutunza kumbukumbu za watumishi, lakini hii haiondoi wajibu wa mtumishi kutunza kumbukumbu zake vile vile kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya kuhamishia Kitengo hiki katika Mfuko wa *Pension* ni kujaribu kuona ni ubunifu gani ambao utatumika ili kuona ni namna gani hawa ambao kumbukumbu zao hazionekani kwa sababu labda ya uhamisho au sababu nyingine zilizotokea hapo awali ili tuweze kupata utatuzi na nimeshaagiza Ofisi yangu kwamba waone ni namna gani tutapunguza adha hiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kumbukumbu zikipatikana watalipwa.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niko kwenye kifungu hicho hicho cha 1001, mshahara wa Waziri, nami niko katika pensheni lakini swali langu kidogo ni tofauti. Mheshimiwa Waziri tulipoanza tu mwezi Juni, 2005 walikuja hapa wastaafu wanasema ya kwamba wale waliorudishwa kwenye daftari wote wamerudishwa kwenye daftari na wote wanalipwa Sh.20,070/=. Sasa tatizo lipo hapa. Hapa kuna mtu ame-*retire* akiwa *Principal Secretary* analipwa Sh.20,070/= ame-*retire* akiwa *Secretary* analipwa hivyo hivyo, *Messenger* analipwa hivyo hivyo, wote wamerudishwa katika mfumo mmoja. Sasa sijui kama kuna ukweli na kama kuna ukweli sijui *formula* gani imetumika. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba, kwa hili swali la Mheshimiwa Simba itabidi niende nikaangalie kwa kweli ni vigezo gani na nitamletea majibu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 – *Finance and Accounts* … … … … … Sh. 99,596,300/=
Kif.2001 – *Policy Development* … … … … … …Sh. 276,394,900/=
Kif.2002 – *Management Services* … … … … … ... .Sh. 213,354,500/=
Kif.2003 – *Establishment* … … … … … … … … ... Sh. 314,606,100/=
Kif.2004 – *Ethics Division* … … … … … … … … …Sh. 108,645,700/=
Kif.3001 –*Human Resource Development* … … … …Sh. 273,488,400/=
Kif.3002 – *Civil Service Training Centre*… … … …Sh. 480,233,600/=
Kif.3003 – *Tabora Secretarial College* … … … … ...Sh. 52,454,300/=
Kif.3004 – *Gender*… … … … … … … … … … … Sh. 50,591,300/=
Kif.4002 – *Management Information System* … … Sh. 145,587,700/=
Kif.4003 – *National Archives* … … … … … … … ... Sh. 401,595,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 20 – Ikulu**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … … Sh.4,909,472,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif.1001 - *Administration and General* … … … … Sh. 77,244,556,600/=
Kif.1002 – *Finance and Accounts* … … … … … Sh. 653,520,500/=
Kif.2001 – *Cabinet Secretariat*… … … … … … Sh. 1,035,359,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … … Sh.1,161,680,400/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 94 – Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … … Sh.1,811,363,200/=

Kif.2001 – *Civil Service* … … … … … … … … … Sh. 667,173,000/=

Kif.2002 – *Local Government Service* … … … … … Sh. 683,602,000/=
Kif.2003 – *Teachers' Service* … … … … … … … Sh.2,283,664,000/=

Kif.2004 – *Fire and Immigration Service*… … … Sh. 481,073,600/=

Kif.2005 – *Health Service* … … … … … … … … Sh. 449,379,200/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … … Sh.58,097,143,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 32 – Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … Sh. 6,119,997,100/=

Kif.2001 – *Policy Development* … … … … … … Sh. 4,019,391,000/=

Kif.2002 – *Management Services* … … … … … Sh.14,157,072,000/=

Kif.2003 – *Establishment* … … … … … … … ... ... Sh. 1,007,618,000/=

Kif.2004 – *Ethics Division* … … … … … … … Sh. 1,094,465,400/=

Kif.3001 –*Human Resource Development* … … … Sh. 2,857,508,600/=

Kif.3002 – *Civil Service Training Centre* … … ... Sh. 1,089,173,800/=
Kif.3004 – *Gender* … … … … … … … … … … ... Sh. 1,167,110,000/=

Kif.4002 – *Management Information System*… … .. Sh.12,705,141,000/=

K if.4003 – *National Archives*… … … … … … … Sh. 4,722,523,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 94 – Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif.1001 – *Administration and General* … … … … … Sh.115,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi, limepitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejementi ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati sasa ipokelewe na makisio haya yapitishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani asubuhi Mheshimiwa Spika aliwatangazieni kwamba kesho kutakuwa na Semina ya Taarifa ya Kudurusu Sera ya Madini, lakini taarifa hii inaeleza kwamba makrabasha mliwahi kupewa sijui lini.

**WABUNGE FULANI:** Tunayo.

**MWENYEKITI:** Kama makabrasha hayo mnayo, basi kesho mje nayo. Semina itakuwa hapa kama kawaida saa tatu asubuhi.

Sasa naahirisha Kikao cha Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.24 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 4 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*